# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Sitini na Mbili – Tarehe 30 Juni, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2021]. (Makofi)*

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka *2021 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2021].*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Suma kwa niaba ya Mwenyekiti, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita sasa aulize swali lake.

Na. 519

**Hitaji la Madarasa ya Kidato cha Tano na Sita – Tarafa ya Bugando na Isulwabutundwe – Geita**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya Kidato cha Tano na Sita katika Shule ya Sekondari Bugando iliyopo Tarafa ya Bugando na Shule ya Sekondari ya Rubanga iliyopo Tarafa ya Isulwabutundwe?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Jimbo la Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Naibu Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Geita pamoja na wadau wa elimu imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya Kidato cha Tano na Sita katika Shule ya Sekondari Bugando iliyopo katika Kata ya Nzera, Tarafa ya Bugando katika Jimbo la Geita. Shule hii imepata kibali cha kuanzisha Kidato cha Tano na Sita mwaka 2021 kwa michepuo ya *PCM* na *PCB* na imepangiwa wanafunzi wa kiume 124 wataoanza kuripoti mnamo tarehe 03 Julai, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita inaendelea na upanuzi wa Shule ya Sekondari Lubanga iliyopo katika Kata ya Isulwabutundwe, Tarafa ya Bugando ili iweze kuwa na Kidato cha Tano na Sita. Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa upo katika hatua ya ukamilishaji na ujenzi wa matundu 12 ya vyoo unaendelea. Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa elimu inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa bweni.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imekamilisha ujenzi wa madarasa 4 na ununuzi wa viti 160 na meza 160 katika Shule ya Sekondari Kakubilo na inaendelea na ujenzi wa bweni na bwalo la chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya Shule za Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita na itazipatia kibali cha kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita mara baada ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu muhimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza, niishukuru sana Serikali kwa kutusaidia pesa na kuweza kumalizia ujenzi wa madarasa ya *Form Five* na *Six* pale Nzela.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, majibu ya Serikali kuhusiana na Shule ya Sekondari Lubanga hayajajitosheleza vizuri kwa kuwa tumekuwa tukisuasua, hata hayo madarasa mawili yamejengwa na Mbunge pamoja na nguvu za wananchi. Kwa sababu maombi nimeshaleta zaidi ya mara tano, ni lini Serikali mtatupatia pesa kwa ajili ya kujenga madarasa na mabweni kwa ajili ya *Form Five* na *Six* pale Lubanga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ili Mheshimiwa Naibu Waziri aone nachokiomba kina umuhimu, naomba *commitment* yake baada ya Bunge twende wote akaone

ule umbali wa kutoka Lubanga kwenda kwenye hiyo shule ya *Form Five* na *Six* ambayo itafunguliwa mwezi waliopanga, ni kilometa 105, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa tayari umeshauliza swali la pili. Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri Ofisi, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Jimbo la Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ametaka tu *commitment* ya Serikali kwamba ni lini sasa Shule ya Lubanga itapelekewa fedha ili yale madarasa mengine yakamilike na shule hii tuweze kuifungua kwa wakati.

Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tumelipokea suala hili, tutatafuta fedha na tutaziweka katika miradi ambayo inafuatia ili kuhakikisha katika mwaka wa fedha unaokuja shule hii iwe imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili alikuwa ananiomba tuweze kuongozana mara baada ya Bunge, nimpe taarifa kwamba nitakuwa na ziara katika Mkoa mzima wa Geita. Kwa hiyo, niseme tu kabisa kwamba nitakwenda pamoja naye mpaka katika eneo hili analolisema kujionea kwa pamoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma huwa anasema sana kuhusu Darasa la Saba lakini leo ameuliza maswali kuhusu elimu ya Kidato cha Tano na Sita. Maana yake hata yeye anapenda watoto wa Jimbo lake na Watanzania wote wasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa huwa Shule ya Sekondari Msalala tumeweza kujenga madarasa na miundombinu yote kwa ajili ya Kidato cha Tano na cha Sita na pia Kata ya Nyangh'wale tumeweza kukamilisha ujenzi huo.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa kibali ili tuweze kufungua shule hizo kwa Kata za Nyang'wale na Msalala? Tumeshakamilisha miundombinu, ni lini Serikali itatoa kibali ili tuweze kufungua shule hizo?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema katika eneo lao wameshamaliza ujenzi wa shule za sekondari katika Kata za Nyang'wale pamoja na Msalala na anachotaka kujua tu ni lini Serikali itatoa kibali. Kwa sababu ameshalizungumza hapa nitaagiza wataalam wangu waende wakafanye tathmini pale wajihakikishie kama miuondombinu yote imeshakamilika. Wakishajiridhisha na hilo maana yake tutatoa kibali mara moja na shule hiyo itafunguliwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, hizi shule zinazosajiliwa naamini katika wale walimu ambao mmewaajiri hivi karibuni mtazipa kipaumbele ili shule zisipewe kibali halafu kukawa hakuna walimu.

Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, sasa aulize swali lake.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Serikali ijibu swali la wananchi wa Jimbo la Hai, Na.520

Na. 520

**Kutekeleza Ahadi ya Ujenzi wa Barabara – Hai**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Ujenzi wa Barabara za Kwasadala – Jiweni, Mashua - Shirinjoro – Mijongweni, Kalali – Nronga, Arusha Road – Mlimashabaha – Sanya Stastesheni pamoja na Kwasadala – Uswaa?

**NAIBU SPIKA:** Uipitie Kanuni ya 49. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Kwasadala – Jiweni – Mshua, barabara ya Shirinjoro – Mijengweni, barabara ya Kalali – Nronga, Arusha Road - Mlima Shabaha – Sanya Stastesheni pamoja na Kwasadala – Uswa zimesajiliwa kwa majina ya Kwasadala - Mshua yenye urefu wa kilomita 35.06, barabara ya Shirinjoro - Mijongweni yenye urefu wa kilomita 12.71, barabara ya Kalali - Nronga yenye urefu wa kilomita 6.04, barabara ya Somali - Tindigani yenye urefu wa kilomita 12.00 na Barabara ya Kwasadala - Uswaa yenye urefu wa kilomita 9.87.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali kupitia *TARURA,* Halmashauri ya Wilaya ya Hai imezifanyia matengenezo barabara za Kwasadala -

Mashua kilomita 14, Shirinjoro - Mijongweni kilomita 5, Kalali - Nronga kilomita 5 na barabara ya Kwasadala - Uswaa kilomita 5 kwa gharama ya shilingi milioni 157.5. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga shilingi milioni 189.35 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Kwasadala - Mshua kilomita 17, Shirinjoro - Mijongweni kilomita 4, Kalali-Nronga kilomita 5 na barabara ya Kwasadala - Uswaa kilomita 9. Matengenezo ya barabara hizo yanaendelea na yanatarajiwa kukamilika ifikapo Agosti 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 barabara hizo zimetengewa shilingi milioni 123 kwa ajili ya matengenezo ya vipande vyenye jumla ya urefu wa kilomita 30.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kipande cha barabara ya Mashua – Jiweni ni kipande muhimu sana kwa sababu kinahudumia Kata tatu; Kata za Masama Kusini, Romu na Masama Magharibi lakini Vijiji vikubwa vya Lukani, Kiu, Lwasaa na Jiweni. Barabara hii kwa sasa haipitiki, je, Serikali haioni ipo haja ya kupeleka fedha za dharura ili barabara hii ambayo inatuletea mazao huku Dodoma, iweze kupitika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa tangia tumepata Uhuru, Jimbo la Hai hatujawahi kupata taa za barabarani, ni lini sasa Serikali itatuletea taa za barabarani kwenye Mji mkubwa unaokua wa Boma Ng'ombe, Maili Sita na Njia Panda ya kwenda Machame? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo

mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza hapa kwamba barabara ya Mashua mpaka Jiweni ambayo inahudumia Kata kubwa tatu haipitiki na ameomba fedha za dharura. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge tumelipokea ombi lake na tutakachokifanya sasa hivi tutatuma wataalam wakafanye tathmini na baada ya hapo tutatafuta fedha ili barabara hiyo iweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni lini sasa Serikali itapeleka taa za barabarani katika Miji Mikubwa ya Boma Ng'ombe, Njia Sita pamoja na Kata nyingine ambazo ameanisha hapa. Niseme tu najua jitihada kubwa za Mheshimiwa Mbunge kwa Jimbo la Hai na najua ana dhamira ya kweli ya kuwasaidia wananchi wake, kwa sababu ameleta ombi hili niseme na lenyewe tunalipokea kwa ajili ya kulifanyia kazi. Naamini kabisa kwa ufuatiliaji wake mzuri na fedha ikipatikana basi taa zitaletwa na Serikali kwa wakati kulingana na bajeti itakavyopatikana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kuniona. Nadhani mtakubaliana nami kwamba hizi barabara zinajengwa ili kuwapa watu urahisi wa maisha na kuwawezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kalali – Nronga ni barabara ambayo ina kona nyingi, ni ndefu na ina milima, ni chini tu ya Mlima Kilimanjaro. Huko Nronga ndiyo kwenye kile kiwanda kikubwa cha maziwa ya mgando ambayo pia yananywewa hapa Dodoma. Swali langu kwa Wizara, ni lini sasa barabara hiyo itaanza kutengenezwa kidogokidogo kwa lami ili wamama wale waweze kuteremsha maziwa yao mpaka mjini na kufika huku Dodoma kwa ajili ya afya za watu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachokieleza Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ya Kalali – Nronga ambayo inapita pembezoni mwa Mlima Kilimanjaro kule chini imeharibika na tunahitaji fedha ya kutosha kuendelea kuijenga na ombi la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba wanahitaji sasa ianze kujengwa polepole kwa kiwango cha lami. Niseme tu kwamba kulingana na bajeti yetu kadri itakavyoongezeka, tutalipokea na tutaliweka katika mipango yetu ya baadaye kuhakikisha barabara hii inatengenezeka ili iweze kutoa huduma kwa urahisi kwa wananchi wa eneo husika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda.

Na. 521

**Utoaji wa Namba Vijiji vya Jimbo la Ndanda**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itasaidia na kufanikisha kutoa namba kwa Vijiji vya Chipunda Kata ya Namatutwe, Mkalinga Kata ya Chikunja na Sululu ya Leo Kata ya Namatutwe vyenye Wakazi zaidi ya elfu kumi katika Jimbo la Ndanda?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Ndugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, namba za usajili wa vijiji hutolewa kupitia Hati za Usajili wa Vijiji kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 22 na 26 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287. Aidha, Vijiji hivyo hupaswa kuwa vimetangazwa kupitia Gazeti la Serikali kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 30 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chipunda na Mkalinga ni Vitongoji katika Kijiji cha Namatutwe na Napata na Sululu ya Leo ni eneo ndani ya Kitongoji cha Maleta katika Kijiji cha Namatutwe, Kata ya Namatutwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, hivyo maeneo hayo hayatambuliki kama Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wakazi wa maeneo hayo wameonesha uhitaji wa kuanzisha Vijiji ni vema wakaanzisha kusudio la kuyafanya maeneo hayo kuwa vijiji kwa kuzingatia sheria pamoja na Mwongozo wa Uanzishaji Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014 kupitia mikutano na vikao kwenye ngazi ya vijiji, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya, Kamati ya Ushauri ya Mkoa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil David Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, majibu ya Serikali ni mazuri hata hivyo majibu haya yanatofautiana na majibu ambayo Serikali hii ilijibu mwaka 2016. Wakati huo walisema kwamba wamesimamisha kutoa namba za maeneo ya utawala mpaka pale watakapokamilisha taratibu zote kwa maana ya kupata watendaji, ofisi na mahitaji muhimu ili kuweza kuwa

na vijiji. Leo Serikali inasema kwamba endapo watakamilisha taratibu hizi ambazo zilishakamilika zaidi ya miaka kumi, sasa swali langu kwa je, endapo nitaleta hizo *documents* zote zinazotoka kwenye Halmashauri ya Wilaya Masasi, Serikali itachukua muda gani kuhakikisha namba za vijiji hivi zinatolewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi katika maeneo mbalimbali kwa sababu Serikali imekuwa inatoa namba lakini baadaye maeneo mengine yanatangazwa kuwa ni hifadhi, maeneo mengine ni mipaka kati majeshi pamoja na vijiji mfano Kijiji cha Chingulungulu ambapo kuna Hifadhi ya Misinjesi lakini Kijiji cha Ngalole ambapo wanapakana na Magereza ya Namajani, Wilaya ya Masasi. Vijiji hivi vyote vina namba na Serikali ipo pale inasema kwamba na yenyewe pia ni maeneo yao.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya taasisi hizi kujiridhisha kwanza kabla ya kuamua kutwaa maeneo haya ili waweze kuwalipa fidia ama yachukuliwe na Serikali? *(Makofi)*

Swali la pili; kulikuwa na migogoro mingi katika maeneo mbalimbali ya ardhi, kwa sababu Serikali imekuwa inatoa namba lakini baadaye maeneo mengine yanatangazwa kuwa ni hifadhi na mengine ni mipaka kati ya majeshi pamoja na vijiji, kwa mfano Kijiji cha Chingulungulu ambapo kuna Hifadhi ya Misinjesi na Kijiji cha Ngalole ambako wanapakana na Magereza ya Namajani Wilaya ya Masasi; vijiji hivi vyote vina namba na Serikali iko pale inasema kwamba na yenyewe pia ni maeneo yao.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya taasisi hizi kujiridhisha kwanza kabla ya kutwaa maeneo haya ili waweze kuwalipa fidia kabla ama yachukuliwe na Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza la pili, nahisi ni la maliasili. Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa, Dkt. Festo Dugange. Majibu kwa swali la nyongeza la kwanza,

halafu swali la nyongeza la pili Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza, kwamba Serikali kwa kipindi kile cha mwaka 2016 kilikuwa kinafanya mapitio ya kukamilisha mfumo bora zaidi wa usajili wa maeneo mapya ya utawala. Kwa hiyo, tangazo na maelekezo yale ya Serikali yalikuwa sahihi na yalifanyika kwa wakati ule na ndiYo maana leo Serikali imetoa maelekezo kwamba sasa Halmashauri ya Ndanda pia tunaweza tukaanza utaratibu wa kusajili vijiji hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba akileta *documents* zinazohitajika, tutapitia taratibu husika na muda siyo mrefu sana, baada ya mamlaka kujiridhisha uhalali na vigezo vya vijiji vile, basi tutapata vijiji vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri; Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, naona unajibu kwa niaba ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano ya usajili wa vijiji; ili kiwe Kijiji ni lazima kipate Hati ambayo inatolewa na TAMISEMI. Hivi sasa vijiji vilivyosajiliwa kwa *record* yangu havipungui 12,319. Baada ya hapo kila Kijiji kinatakiwa kipate Cheti kutoka kwa Kamishna wa Ardhi ili kuonyesha mipaka ya Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila Kijiji Tanzania lazima kiwe na vyeti viwili; Hati ya kusajiliwa, ni Mamlaka ya Utawala kwamba sasa mnaweza kuchaguana, ni Serikali

kamili. Baada ya hapo inatakiwa Kijiji kipimwe ili kiweze kupata Hati, yaani Cheti kinachoonyesha sasa utawala wenu wa Serikali unamiliki ardhi kiasi gani. Kwa hiyo, hivi sasa kuna vijiji 1,557 ambavyo havijapata Hati au Vyeti vile vya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahisi namna ya kuondoa mgogoro huu wa Ndanda, kwanza ipatikane hiyo Hati ya kusajili Kijiji, halafu tukapime mipaka ya Kijiji kile. Siyo kweli kwamba Kijiji hakiwezi kuwa na msitu, kinaweza kuwa na msitu, lakini Cheti chenye heshima na kinachothaminiwa na kinachotakiwa kisheria ndani ya Kijiji ni Cheti cha umiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane kuhakiki kwenye vijiji vyetu kuhakikisha kila Kijiji kina vyeti viwili; kwanza, wana Hati ya kusajiliwa kama Serikali na pia vyeti vya kumiliki ardhi. Sasa ndani ya Kijiji kunaweza kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi unaoonyesha misitu, makazi, kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuongeza hilo, sikuwa namjibia Waziri wa Maliasili, lakini nilikuwa natoa ufafanuzi kwamba kila kijiji kinatakiwa kipimwe kipewe Cheti cha Ardhi ya Kijiji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa huo ufafanuzi. Nadhani hoja ya msingi ni kwamba Kijiji kinapopewa Hati lazima kuna vigezo ambavyo inatakiwa iwe navyo, ikiwa ni pamoja na ardhi na idadi ya watu. Kwa hiyo, Maliasili sasa wakienda pale, ile ardhi ambayo inajulikana ni ya Kijiji, halafu wao wakaweka hifadhi hapo, halafu na nyie mkaja mkakipunguza ukubwa kile Kijiji, nani anakuwa amekuja kwanza kabla ya hapo? Aliyemtangulia mwenzie ni nani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Maliasili hawawezi kupora ardhi kwenye vijiji, hawawezi. Kwanza Maliasili hawatoi Cheti, wala hawatoi Hati. Wao wanatengeneza *GN*. Msitu wa Maliasili unaweza kuwa sehemu ya ardhi ya Kijiji. Kikubwa

hapa ni Hati; Cheti kinachotawala ardhi ya Kijiji, lakini ndani mle kunaweza kuwa na shughuli mbalimbali hata za kibinadamu ndani ya Kijiji.

**NAIBU SPIKA:** Sawa, ahsante.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mnaweza kuwa na ardhi ya Serikali au ya watu binafsi ndani ya Kijiji, lakini Cheti cha Kijiji kinaonyesha mipaka ya utawala ya Kijiji kizima pamoja na ardhi iliyopo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kwa hiyo. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufafanuzi huu na kwa hoja ya Mheshimiwa Mwambe, nadhani Wizara hizi tatu, vinapoanzishwa vijiji lazima ziwepo ili isifikie mahali Kijiji kimepewa Hati ya Usajili, halafu kimepewa Hati Ardhi, halafu baadaye tena, Maliasili na yenyewe inakuwa na eneo kwenye hilo eneo la Kijiji. Nadhani hiyo ndiyo inayoleta mgogoro.

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala sasa aulize swali lake.

Na. 522

**Maeneo Yasiyoendelezwa Kurudishwa Halmashauri**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyarudisha kwenye Halmashauri maeneo yote yasiyoendelezwa na Mashirika ya Umma kwa zaidi ya miaka kumi ili Halmashauri zijenge miundombinu ya huduma za jamii.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, haki ya kumiliki ardhi hutolewa kwa mujibu wa Sheria za Ardhi. Hivyo zimeweka masharti ya umiliki wa ardhi ikiwa ni kufanya maendelezo ndani ya muda husika, pamoja na hatua za kuchukua endapo kuna ukiukwaji wa masharti hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baadhi ya Mashirika ya Umma yaliyomilikishwa ardhi katika maeneo mbalimbali nchini, hayajaendeleza ardhi zao. Katika kutatua changamoto hizo, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji, imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kushughulikia ardhi iliyomilikishwa na kuachwa bila kuendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Wizara imeanza kwa kufanya ukaguzi wa maeneo yaliyomilikishwa kwa watu binafsi, wawekezaji wakubwa na Mashirika ya Umma ili kubaini ukiukwaji wa masharti ya umiliki yaliyotolewa na hivyo kuanzisha taratibu za ubatilisho. Baada ya kubatilisha miliki za maeneo ambayo hayajaendelezwa, ardhi husika hupangwa na kupimwa upya kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uwekezaji, miundombinu ya huduma za jamii kwa kuzingatia mahitaji halisi ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kuendelea kufanya ukaguzi wa maeneo yaliyotolewa kwa Mashirika, Makampuni na watu binafsi na kuanzisha utaratibu wa ubatilisho endapo itabainika uwepo wa ukiukwaji wa masharti ya umiliki na kuwasilisha mapendekezo Wizarani kwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Abdallah Jafari Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri ndiyo Mamlaka za Upangaji: ni lini Wizara ya Ardhi itakabidhi viwanja vya mradi wa viwanja 20,000 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ili kuyapangia matumizi mengine maeneo yote ya Taasisi ambayo hayakuendelezwa katika Kata ya Tuangoma na Kibada hasa katika Kiwanja kilichopo Goroka *Block D, Block 10* Kiwanja Na. 219, Changanyikeni *Block 9* Kiwanja Na. 215, mashamba pori ya *NSSF* ya Mtaa wa Masuliza, Mwapemba, Vikunai na Changanyikeni? *(Makofi)*

Swali la pili: Je, ni lini Wizara ya Ardhi itaweka miundombinu ya barabara katika mradi wa viwanja 20,000 katika maeneo yote ya Kata ya Tuangoma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Lukuvi, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, nataka tu niwaeleze Waheshimiwa Wabunge, alichosema Mheshimiwa Chaurembo ni kweli kwamba kwa mujibu wa Sheria Mamlaka za Upangaji wa Ardhi ni Halmashauri. Kwa hiyo, sisi kama Madiwani ni sehemu ya Mamlaka ya Upangaji wa Ardhi. Kila Halmashauri inapanga yenyewe matumizi ya ardhi yake. Ingawa tunashirikiana katika kuthibitisha ule upangaji, lazima uthibitishwe na Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam kuna mradi ulianzishwa miaka ya nyuma ya viwanja 20,000. Sasa leo nataka niseme hapa mbele ya Mheshimiwa Mbunge, viwanja 20,000 vilivyopimwa katika Wilaya ya Temeke, kwa mfano hivi vya Tuangoma iliyokuwa miradi 20,000 na Kibada, nimeshaagiza na ninarudia tena kuagiza, Wizara ya Ardhi ikabidhi michoro ya viwanja hivi 20,000 kwa Manispaa ya Temeke na wiki hii lazima makabidhiano yafanyike ili

wananchi na Wilaya ya Kigamboni waweze kusimamia ipasavyo miradi hii ya viwanja 20,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulikuwa ni mradi ndani ya Wilaya ya Temeke, sasa michoro yote na taarifa zote za umiliki ziwe ni *open space,* maeneo ambayo hayajaendelezwa, Temeke liwe ni jukumu lao kufuatilia. Kama kuna watu hawajaendeleza Temeke ni Mamlaka halisi. Pekuweni tutoe *notice* kwa watu ambao hawajaendeleza tuchukue hatua mchukue ardhi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naagiza Kamishina wa Ardhi akabidhi michoro na taarifa zote. Kuanzia leo, eneo lote la Viwanja 20,000 la Kibada na Tuangoma lazima liwe chini ya Mamlaka ya Manispaa ya Temeke. Hayo mengine mtafanya wenyewe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 523

**Ujenzi wa Barabara ya Nangurukuru - Liwale**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Nangurukuru – Liwale yenye kilometa 258 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 25 inavyoelekeza?

**NAIBU SPIKA:** Baadaye uipitie Kanuni ya 49. Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Eng. Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa, Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa zabuni wa kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kwa ajili ya kuijenga Barabara ya Nangurukuru – Liwale yenye urefu wa kilometa 258 kwa kiwango cha lami umeshakamilika na mkataba wa kazi hii unatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa mwezi Juni, 2021. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi milioni 548.603 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Kazi ya usanifu itakapokamilika Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza, napenda kumwuliza Waziri wa Ujenzi kwamba, kwa kuwa katika mwaka 2019, Serikali ilichepusha katika Kijiji cha Njinjo, barabara ya Nangurukuru – Liwale na hivyo ililazimu kulipa fidia kwa baadhi ya wananchi ambao walikuwa na mali zao katika lile eneo ambalo limechepushwa barabara; lakini kuna wananchi wawili hadi kufikia sasa hawajalipwa fidia ya mali zao; nao ni Mama Mary Mahmoud Kiroboto pamoja na Ndugu Said Salum Karanje, ambao wanadai jumla ya shilingi 13,264,180/=. Napenda kujua: Je, Serikali ni lini itawalipa wananchi hawa wawili haki yao ya fidia kwa ajili ya kuchepusha kipande kile cha barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, napenda kumwuliza Waziri kwamba, kwa kuwa wakati wa maadhimisho ya Kumbukizi za Vita vya Majimaji ilipotimiza miaka 100 mwaka 2010, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete wakati ule, aliwaelekeza Wakala wa Barabara Tanzania Mkoa wa Lindi...

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali lako, Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nashukuru. Alitoa maelekezo wafungue barabara kati ya Nandete na Nyamwage: Je, mpango huu umefikia wapi wa kufungua barabara ile ya kipande cha Nyamwage kwenda Nandete? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, hili swali la nyongeza la kwanza, kama ulipata taarifa kabla ni sawa, lakini kama huna taarifa usilijibu kwa sababu linauliza kuhusu hao watu wawili mahususi. Sasa kama huna taarifa zao, hilo swali la kwanza utamtafutia majibu. Majibu kwa swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa, Francis Ndulane Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake amesema kwamba, kulitolewa ahadi na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu. Napenda tu nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa hii barabara ilitakiwa ifunguliwe maana yake haipo kwenye mtandao wa barabara za *TANROAD* wala za *TARURA*. Hivyo napenda nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imelichukua na tutawasiliana na Meneja wa *TANROAD* Mkoa wa Lindi ili tuweze kupata taarifa sahihi na ahadi hii ili tuweze kuanza kuitekeleza ama kama ilikwama tujue ni kwa nini ilikwama wakati ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili, kama ulivyotoa maelekezo, ni swali ambalo lipo *very specific* na kama watu hao wapo ni bora wakaandika barua rasmi kwa *TANROAD* Mkoa wa Lindi, wakupe *copy* na sisi watupe *copy*

ili tuweze kuliangalia, kwa sababu ni suala la watu wawili, tuweze kuliangalia kama lina changamoto gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Changamoto iliyopo kwenye barabara ya Liwale - Nangurukuru inafanana kabisa na changamoto iliyopo kwenye barabara ya Mtwara Pachani, Lusewa kwenda Nalasi mpaka Tunduru Mjini. Mwaka, 2015 aliyekuwa mgombea mwenza ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, alitoa ahadi barabara ile kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Nashukuru Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu mwaka jana 2020: Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa, Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI – (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mtwara - Pachani hadi Nalasi ni barabara ambayo tayari imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa hiyo, kinachosubiriwa sasa hivi ni Serikali kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga hii barabara. Kwa hiyo, tayari taratibu zimeshaanza, tunachosubiri tu ni fedha ipatikane. Katika Awamu hii ya miaka mitano, kama fedha itapatikana, basi itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kutekeleza hiyo ahadi ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nawaomba, kwa sababu wengi mnasimama kwa ajili ya maswali; maswali mnayafanya marefu. Nenda moja kwa

moja kwenye swali unalotaka lijibiwe na Serikali. Mheshimiwa, Mbunge wa Liwale, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Barabara ya Nangurukuru - Niwale ni mwaka wa tano inatengwa fedha kwa ajili upembuzi yakinifu na usanifu wa kina…

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali. Taja barabara unayotaka ijibiwe.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nangurukuru - Liwale, fedha hazijawahi kuletwa tangu zinatengwa miaka yote mitano.

**NAIBU SPIKA:** Swali lako ni nini?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Nangurukuru - Liwale? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la nyongeza la mheshiiwa Kuchauko ndiyo lilikuwa swali la msingi na Serikali imetenda shilingi milioni 548.603 na tumesema taratibu zote zimekamilika na muda wowote inatangazwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, lakini Mheshimiwa Husna kabla hujauliza swali lako, marekebisho kidogo ya Swali Na. 522 kwenye majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Tuangoma na Kibada ziko Temeke na siyo Kigamboni. Kwa

hiyo, Mheshimiwa Waziri amerekebisha hiyo, Makatibu Mezani pamoja na watu wa taarifa rasmi za Bunge, hizo zikae vizuri.

Mheshimiwa, Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 524

**Kuhamisha Dawati la Jinsia Kwenye Vituo vya Kutolea Huduma za Afya**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuhamisha Dawati la Kijinsia kutoka Jeshi la Polisi na kwenda kwenye Vituo vya kutolea Huduma za Afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Mwanaidi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Husna Sekiboko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria mbalimbali za Nchi. Jeshi la Polisi limepewa mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Fungu Na. 5, Kifungu kidogo cha (322) ya mwaka 1965 na kuboreshwa mwaka 2002 ya kulinda raia na mali zake na kupeleleza makosa mbalimbali. Hivyo, Dawati hilo ni vyema likaendelea kukaa lilipo sasa badala ya kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa waathirika wa vitendo vya ukatili wa kijinsia wanapatiwa huduma rafiki na za haraka, Dawati hili hushirikiana na Vituo vya Mkono kwa Mkono ambavyo viko kwenye Vituo vya Afya vikiwa na Wataalam wa Afya, Maafisa wa Jeshi la Polisi, Ustawi wa Jamii na Wanasheria kwa ajili ya utoaji wa huduma stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na majibu ya Serikali kwamba nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria mbalimbali. Swali la kwanza; kwa kuwa sheria hizi huwa zinafanyiwa marekebisho kadri uhitaji unavyotokea au wakati. Je ni lini sasa Serikali italeta marekebisho ya sheria hii ili kuwapa nafasi nzuri zaidi waathirika kuripoti haya matukio?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Vituo hivi vya Mkono kwa Mkono ni vichache, vinakadiriwa kuwa 14 nchini na uhitaji ni mkubwa kwa sababu tunahitaji kuwatunza wale waathirika kwenye vituo hivyo kabla ya mashauri kukamilika ili kulinda uchunguzi. Je Serikali ina mpango gani sasa kwa ajili ya kuongeza vituo hivi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Hamisi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Husna, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza kwa nini dawati hilo halishirikishwi na vituo vya hospitali; kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi dawati hili hushirikiana na Vituo vya Mkono kwa Mkono na pia hushirikiana na Jeshi la Polisi, huduma za afya pamoja na wanasheria ili kuhakikisha

kwamba waathirika wa vitendo vya ukatili wa kijinsia hupata huduma stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuongezea kwamba, sio kila wahanga waathirika wa vitendo vya ukatili wa jinsia, wanahitaji huduma za afya; waathirika wengine wanahitaji huduma za kisheria, unasihi, na msaada wa kisheria ili kuona kwamba wanapatiwa huduma stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, je ni lini sasa Serikali litaleta marekebisho hayo Bungeni. Napenda kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, hadi sasa hatujapata ugumu wa marekebisho ya sheria ya masuala ya ukatili wa kijinsia. Kwa hivyo nimwombe Mheshimiwa Husna atuletee marekebisho au maboresho ya dawati hili ili Serikali iweze kuangalia zaidi maboresho hayo na muathirika wa vitendo vya ukatili wa kijinsia aweze kupata huduma na kuweza kuleta malalamiko yake bila ya kuwa na hofu kwa kutumia sheria ambazo zimewekwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo Mbunge wa Arumeru Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 525

**Serikali Kuwasha Umeme Kwenye Vijiji ambavyo bado Havijawashwa**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawasha umeme kwenye Vijiji na Vitongoji vyote katika Jimbo la Arumeru Mashariki ambavyo umeme bado haujawashwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Byabato Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vyote ambavyo havijapata umeme katika katika Jimbo la Arumeru Mashariki vinapatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* awamu ya tatu, mzunguko wa pili ulioanza Mwezi Machi, 2021. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Disemba, 2022. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 2.07.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitongoji vya Jimbo la Arumeru Mashariki ambavyo havijafikiwa na umeme vitaendelea kupatiwa umeme kupitia mradi wa ujazilizi yaani *densification* unaotarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021. Aidha, kazi ya kupeleka umeme katika vitongoji ni endelevu, Serikali kupitia *TANESCO* na *REA* itaendelea kupeleka umeme katika vitongoji kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Danielson Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi. Kwanza niseme naishukuru sana Serikali na kuipongeza kwa kazi nzuri ambayo inafanya kwa kuhakikisha kwamba inawasha umeme kwa vijiji vyote na vitongoji nchi nzima. Hata hivyo, hivi karibuni tulipata orodha ya wakandarasi ambao wamekuja kwa ajili ya kufanya kazi ya kumalizia zoezi la kuwasha umeme *REA III*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Arusha Mkoani amekuja kandarasi mmoja tu na kule Longido, nakuwa na mashaka kwamba ahadi ya Serikali kwamba mwaka kesho watakuwa wametimiza ahadi yao ya vijiji vyote nchi nzima kuwa vimeshapata umeme; nakuwa na mashaka kwamba tutaweza kufanikisha hilo zoezi. Swali langu, je, wana mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanaongeza idadi ya

wakandarasi ili hiyo kazi na ahadi ya Serikali iwe ya kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kwa kutambua juhudi za Serikali za kuendelea kuwahudumia watanzania kwa kuwapelekea umeme katika maeneo yao na ni *commitment* ya Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwamba kufikia Disemba, 2022, tutakuwa tumekamilisha upelekaji wa umeme katika maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wiki kama mbili zilizopita Mradi wa *REA III, round II,* ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Waziri katika eneo la Longido na mkandarasi anayefanya kazi katika Mkoa wetu wa Arusha anaitwa *SAGEMCOM* na yuko kazini tayari na alikuwa amepewa maeneo matatu ya Longido, Karatu na Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upana wa Mkoa wa Arusha, Wizara imeona ni vema kuongeza mkandarasi mwingine, aende akafanye kazi katika Jimbo la Arumeru Mashariki, Mgharibi lakini pia na Ngorongoro. Kabla ya mwezi Julai haujaisha mkandarasi atakuwa ameripoti kazini kwa ajili ya kuendelea kufanya kazi ili ile ahadi iliyotolewa na Serikali ya kufikisha umeme kwa wananchi wote ifikapo Disemba mwakani iwe imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwa sababu baada ya hapa tunatawanyika kwenda kwenye maeneo yetu basi wakawe mkono wa kwanza kabisa wa kushirikiana na

wakandarasi kutimiza azma ya kupeleka umeme kwa wananchi kwa kuwasimamia kwa karibu na kuwa pamoja na sisi ili kuweza kufikisha hiyo ahadi. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika awamu hii ya *REA* kila kijiji kimepewa kilomita moja, nataka nifahamu hizi kilomita moja zinaanza kuhesabiwa wapi, ndani ya kijiji au nje kwa sababu kuna vijiji vingine vimeachana kilomita tatu, kutoka kijiji kimoja mpaka kufika kingine? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi.

Mheshimiwa Naibu Waziri basi naona Waziri amesimama. Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwenisongole kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa katika swali la msingi na swali la nyongeza la Mheshimiwa Pallangyo. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Mwenisongole kuuliza swali la msingi ambalo kimsingi linawahusu Wabunge wote katika majimbo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumetoa utaratibu mkandarasi anapoingia katika kijiji angalau atumie umbali wa kilometa moja kusambaza umeme tofauti na ilivyokuwa huko zamani ambapo ilikuwa ni wateja wawili watatu wanne. Jambo la msingi hapa ni kwamba ile kilometa moja tunayoitaja ni ndani ya kijiji, sio kati ya kijiji kimoja na kingine, ndani ya kijiji akishafika. Hata hivyo, hao ni wateja wa awali,

ataendelea kuunganisha wateja wengine kadri wateja wengine wanavyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, tusifungwe na kilometa moja, kilometa moja ni wateja wa kuanzia, badala ya kufunga *transformer* ukaiacha bila kuwa na mteja. Nimeona nitoe ufafanuzi wa jumla ili Waheshimiwa Wabunge wawe na imani na wateja wa kwanza wanaoanza na tuwaombe wananchi jirani na wateja wa kwanza wanaunganishwa waendelee kulipia umeme hili nao waendelee kuunganishiwa umeme. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na Kisiwa kikubwa cha Ukerewe kuwa kwenye matatizo ya umeme kwa takribani wiki tatu sasa, wananchi kwenye Visiwa vidogo vya Ilugwa na Ukara wamekuwa wananunua umeme, lakini hawapelekewi *token.* Je, nini kauli ya Serikali juu ya changamoto hii? Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mkundi, Mbunge wa Ukerewe. Kesi ya wananchi wa Ukerewe inafanana sana na maeneo mengi ya visiwa, ambapo wakandarasi binafsi ambao wanapeleka umeme kwa wananchi wanaozalisha, kwanza wanauza umeme kwa bei kubwa tofauti na maelekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wameanza pia mchezo, wanapopeleka kwa bei ya Serikali hupeleka kwa kiwango kidogo. Naomba nitoe tamko mbele ya Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe na Waheshimiwa Wabunge, mara baada ya Bunge tutatembelea maeneo

yote yenye kero ya namna hiyo na kutoa maelekezo kwa mameneja wetu kuwasimamia wakandarasi wa namna hiyo ili kupeleka umeme kwa bei elekekezi ya Serikali ya Sh.100 kwa *unit* na kuendelea kutoa umeme kwa wananchi kulingana na mikataba yao inavyowaelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitakwenda kwa Mheshimiwa Mkundi, Ukerewe. Pia nitatembelea Maisome na maeneo mengine ili kutoa maelekezo ya Serikali na namna ya kuyasimamia. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika Wilaya ya Karatu kuna Mji Mdogo wa Karatu, sasa huu Mradi wa *REA* umelenga sana kwenye vijiji na pale Mji wa Karatu wanasema ni mjini lakini ni bado vijijini sasa ni lini Serikali ina mpango gani katika ile miji midogo ambayo umeme huu wa *REA* haujapelekwa ili kuwasaidia wananchi wakiwemo wa Jimbo la Karatu wa Mji wa Karatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Awack, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli upelekaji wa umeme unaofanywa na Serikali uko katika picha na maeneo tofautitofauti; ziko hizo tunazoziita *REA* ambapo tumekuwa na awamu kadhaa, lakini iko miradi ya *densification,* inapeleka umeme kwenye vitongoji, lakini hiko miradi tunaita *peri-urban*.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya *peri urban* inapeleka umeme kwenye maeneo ya miji lakini ambayo bado yana asili ya vijiji, Jimbo la Bukoba Mjini likiwemo na kwa Karatu ikiwemo, maeneo ya Mwanza yakiwemo, Geita

ikiwemo, tutahakikisha kwamba kufikia mwezi Februari tumeanzisha huo mradi wa *peri-urban* unaoweza kupeleka umeme kwenye maeneo ambayo ni ya mijini lakini bado yana asili ya vijiji ili na sisi pia tuweze kunufaika na umeme huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anton Mwantona, swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni nini kauli ya Serikali kwenye Jimbo letu la Rungwe kuna vijiji 24 ambavyo vilikuwa kwenye *REA II* havijapatiwa umeme, lakini pia kwenye *REA III, round* ya pili vijiji tisa haviko kwenye orodha ya kupatiwa umeme katika hii *REA III, round* ya pili. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantona, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali la maeneo ambayo yalisahaulika. Tumeshatoa maelekezo na taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge, naomba tena nirudie tu. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge na kama kuna vijiji sita au tisa au vingapi ambavyo vilisahaulika tunaomba atuletee.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya utaratibu baada ya wiki mbili zilizopita, kupitia maeneo yote ya nchi nzima katika vijiji vilivyosahaulika na viko vingi. Kwa Mheshimiwa Lukuvi vilisahaulika vijiji viwili na maeneo mengine, tumepata vijiji 610 na vyote tumeviingiza kwenye mpango wa kutekelezwa na tuna shilingi bilioni 150 na wakandarasi tayari wameshapewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwape tu uhakikisho wananchi kupitia Bunge letu Tukufu kwamba kama

kuna Mbunge yeyote, kijiji chake kimesahaulika tunaomba sana atuletee, Mradi wa *REA III, round* ya pili ni mradi wa kumbakumba wa vijiji vyote. Kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge watuletee vijiji vyao vilivyosahaulika ili visisahaulike ili utekelezaji uende pamoja na maeneo yanayotekelezwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Swali langu pia lililenga hili ambalo limeulizwa na Mbunge wa Rungwe, lakini pia naomba basi niulize kwamba, kwa kuwa imekuwa ni tabia ya wakandarasi kuruka baadhi ya vitongoji, halafu wanapeleka sehemu ya mbele na vitongoji vingine ambavyo vimekatiwa miti yake havipewi. Je Serikali inasemaje kuhusu hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mlaghila kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na tumeshaongea naye kuhusu vijiji na vitongoji vilivyorukwa. Naomba pia nitumie nafasi kupitia Bunge lako Tukufu kuwakumbusha tu wakandarasi na tumetoa maelekezo haya mara kwa mara, kwamba mradi wa vijiji ambavyo tunakwenda kuutekeleza sasa ambao pia una miradi ya vitongoji na mitaa, hauzingatii na hautarajii kuruka kitongoji chochote.

Kwa hiyo niwakumbushe wakandarasi kutoruka sio kitongoji tu kutoruka kijiji, kitongoji, kaya na nyumba, haitegemei ni aina gani ya nyumba. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Rashidi Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 526

**Kupunguza Sehemu ya Hifadhi ya Taifa Mkomazi**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza: -

Hifadhi ya Taifa Mkomazi imebana sana maeneo ya wananchi na kusababisha kazi za kijamii katika Kata za Lunguza, Mng'aro na Mnazi kushindwa kufanyika:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kupunguza sehemu ya Hifadhi ya Mkomazi na kugawa kwa Serikali za Vijiji?

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya 49 inakuhusu wewe pia.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa Mkomazi imetokana na kupandishwa hadhi kwa lililokuwa Pori la Akiba la Mkomazi kupitia Tangazo la Serikali Namba 27 la mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** hifadhi hii ni sehemu ya mfumo wa ikolojia wa Tsavo-Mkomazi wenye wanyamapori wengi. Vilevile, ni maeneo ya mtawanyiko na shoroba za wanyamapori na tayari kumekuwa na changamoto nyingi za shughuli za binadamu katika maeneo hayo ambazo zimesababisha kuwepo na migongano kati ya wanyamapori wakali na waharibifu yaani tembo na wananchi wanaozunguka maeneo hayo ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** hivyo, Serikali haina mpango wa kumega eneo hilo kwani kuendelea kumega

eneo hilo ni kuendeleza migongano kati ya binadamu na wanyamapori waharibifu kama tembo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashidi Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ambayo siyo ya matumaini sana kwa wananchi wa Tarafa ya Umba, hasa Kata ya Mnazi na Lunguza, tunayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa shughuli za wananchi hawa wanaozungukwa na hifadhi ya Taifa Mkomazi sehemu yao kubwa ni ufugaji na eneo lao ni dogo, lakini uanzishwaji wa hifadhi haujawatendea haki kwa sababu hakuna mlango hata mmoja wa kuingilia hifadhini kutokea upande huu wa Lushoto.

Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga geti la kuingia Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi katika eneo la Kamakota, Kijiji cha Kivingo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa ukaribu huu wa Hifadhi na makazi ya watu unasababisha mara kwa mara wanyama waharibifu, hasa tembo, kuvamia mashamba katika Vijiji vya Mkundo- Mbaru, Mkundi-Mtae, kiasi kwamba zaidi ya ekari 3,000 za matikiti maji na mkonge zimeharibiwa vibaya na tembo.

Je, Waziri yuko tayari sasa kuwatembelea wananchi wale ili angalau akawaone na kuweza kuwafariji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Shangazi kwa kuendelea kuhamasisha utalii, hasa katika maeneo ya Jimbo lake la Mlalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Wilaya ya Lushoto ni eneo moja wapo ambalo linasaidia sana kuongeza mapato ya Serikali, hasa kisekta, na Mheshimiwa Shangazi amekuwa mara nyingi akitutembelea katika ofisi zetu kuelezea changamoto za maeneo hayo. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba Serikali inatambua mchango wkae, lakini pia tuko bega kwa bega kuhakikisha kwamba utalii unasonga mbele, ikiwemo eneo hili la Mlalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo ameomba kuhusu kuweka geti katika eneo la Kamakota, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti hii ambayo mmetupitishia, geti hili litafunguliwa ili kurahisisha watalii wanaoelekea maeneo ya Lushoto, hususan Mlalo, basi iwe rahisi sana kupita katika eneo hili la Kamakota.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utalii tutaufungua katika eneo hilo na tuna uhakika kwamba tutaweza kupata mapato mengi yanayotokana na Hifadhi yetu hii ya Mkomazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ameuliza kama Waziri yuko tayari; nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafika Mlalo, kama siyo basi atakuwa ni Waziri, kuongea na wananchi na kuendelea kuwapa pole hata wananchi wengine wenye maeneo ambayo wanakutana na changamoto hizi za wanyama wakali na waharibifu kama tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Mheshimiwa Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, sasa aulize swali lake.

Na. 527

**Ujenzi wa Majosho ya Mifugo Wilayani Igunga**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa majosho katika Wilaya ya Igunga, hususan Jimbo la Manonga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Igunga ina jumla ya majosho 20. Kati ya hayo majosho 12 yanafanyakazi na majosho nane ni mabovu na hayafanyi kazi na hivyo kuhitaji ukarabati.

Aidha, halmashauri hiyo inahitaji jumla ya majosho 36 na hivyo ina upungufu wa majosho mapya 16 yanayohitajika kujengwa. Kati ya majosho mabovu nane, majosho matatu yanakarabatiwa na josho jipya moja linajengwa na halmashauri yenyewe kwa kutumia vyanzo vyake vya fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 jumla ya majosho 10 yatajengwa katika Halmashauri ya Igunga yakiwemo majosho matatu katika Jimbo la Manonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ili kukabiliana na upungufu wa majosho, Halmashauri ya Igunga inashauriwa kuendelea kutenga asilimia 15 ya fedha inayokusanywa kutokana na mifugo kwa ajili ya kujenga na kukarabati majosho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Seif Gulamali, swali la nyongeza.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Igunga ni wilaya moja wapo inayoongoza kwa mifugo mingi sana hapa Tanzania, je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza idadi ya majosho, hasa Jimbo la Manonga, kutoka majosho matatu hata angalau kufika majosho kumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika siku 100 za Mheshimiwa Rais, mama Samia Hassan Suluhu, tumemuona akikutana na Mwanamfalme wa Saudi Arabia na wamejadili juu ya masuala ya mifugo, hasa kuuza mifugo lakini pia kuuza nyama nje ya nchi. Je, Wizara imejipangaje kutumia fursa hii; mkakati wake ni upi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, amjibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kuongeza idadi ya majosho katika Jimbo la Manonga. Naomba tu nipokee ombi hili la Mheshimiwa Mbunge na nimuahidi kwamba Wizara italifanyia kazi kwa kusudi la kuongeza idadi ya majosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni hili la mkakati wa Serikali juu ya kuongeza biashara ya nyama na mifugo nje ya nchi. Kwanza nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan; katika siku hizi 100 moja ya Wizara ambazo amezifanyia kazi kubwa ni hii Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi. Naomba tu nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Wizara imejipanga vyema kuhakikisha kwamba fursa hii ya kuuza nyama na mifugo nje inatumika na inatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni kwa kupunguza kodi mbalimbali ambazo zilikuwa ni kikwazo. Lakini pili, ni kuendelea kushirikiana vyema na sekta binafsi ili kuweza kushamirisha biashara ya mifugo. Na mwisho, mkakati wetu wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe, kopa mbuzi lipa mbuzi, tutaupa kipaumbele sana ili kuongeza uzalishaji katika nchi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Maji; Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 528

**Kuongeza Vituo vya Kuchotea Maji Mji Mdogo wa Gairo**

**MHE. DKT CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vituo vya kuchotea maji katika Mji Mdogo wa Gairo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Mji wa Gairo kwa sasa ni wastani wa asilimia 75. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Serikali imeendelea kuboresha huduma ya maji kwa wananchi kwa kufanya upanuzi wa mtandao wa maji katika Mji wa Gairo ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na ulazaji

wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa kilometa nane na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji vitano, hivyo vituo hivyo vya kuchotea maji kuongezeka kutoka vituo 70 na kufikia 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2021/2022, Serikali imepanga kuendelea kuboresha huduma ya maji safi na salama katika Mji wa Gairo ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilometa 21.8 ili kupeleka maji majumbani na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 40. Aidha, kwa lengo la kuongeza uzalishaji maji, Serikali imepanga kutekeleza Mradi wa Maji wa Chagongwe utakaonufaisha maeneo ya Mji wa Gairo na vijiji vya pembezoni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Licha ya majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwanza niishukuru Serikali, nina furaha sana kuona kuwa Mradi wa Chagongwe, ambao ni wa muda mrefu, unaanza. Je, mradi huu wa kutoka Milima ya Chagongwe na Nongwe utaanza kutekelezwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Manispaa ya Morogoro, nashukuru Serikali inaendesha miradi ya maji kwenye manispaa yetu, lakini hata hivyo bado tunapata maji ya mgao. Je, miradi hii, hasa mradi wa Bwawa letu lile la Mindu, ni lini hasa litakamilika na miradi mingine, ili wananchi wa manispaa waweze kupata maji kila siku na waondokane na maji ya mgao? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge mama yangu Dkt.

Christine Ishengoma ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kazi kubwa na nzuri na anatusimamia vizuri sana ili sisi Wizara kuhakikisha watu wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge, ambacho ninataka kukuhakikishia Mheshimiwa Mwenyekiti wetu ni kwamba eneo la Mradi huu wa Chagongwe, katika mwaka huu wa fedha tunaokwenda nao tumepata fedha ambazo ni za ziada za Mheshimiwa Rais, zaidi ya bilioni 207. Hili ni eneo ambalo tutalipa umuhimu mkubwa kuhakikisha katika mwaka huu unaoanza wa fedha, kwenda kuanza mradi huu na wananchi wa Gairo waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge ni kuhusu suala zima la maji katika eneo la Morogoro. Mji wa Morogoro uzalishaji wake ni lita milioni 35, lakini mahitaji yake kwa sasa ni lita milioni 67, kwa hiyo, kuna uhitaji mkubwa sana wa maji, kwa hiyo mkakati wa haraka katika siku 100 za Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan, ametupatia fedha zaidi ya bilioni nne kwa ajili ya kujenga mradi wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tumejenga tenki la lita milioni mbili eneo la Mgulu wa Ndege ambapo tutakwenda kutumia chanzo cha maji cha Mambogo ambao tumeweka maji katika tenki lile la Mgulu wa Ndege ambapo maji yale yatakwenda Kihonda, maji yale ambayo yatakwenda eneo la *SGR,* Lukobe na Mkundi katika ili kuhakikisha wananchi wa Morogoro wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkakati wa kumaliza kabisa tatizo la maji katika Mji wa Morogoro, tumepata fedha zaidi ya Euro milioni 70, ambapo tumekwishasaini mkataba na wahandisi washauri, mradi ule tunakwenda kuhakikisha unaanza kwa haraka ili wananchi wa Morogoro waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nami nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga na kuboresha miundombinu ya maji katika Jimbo la Muhambwe, hususan Kata za Kibondo Mjini, Bunyambo na Kitahana ili kukabiliana na uhaba mkubwa wa maji ulioko katika jimbo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe, nadhani mwezi mmoja ama miwili iliyopita, Mheshimiwa Mbunge wa Mihambwe ameingia katika Bunge hili. Amekuja ofisini, na jana tumekwisha mpa pesa, zaidi ya milioni 100 ili kuhakikisha kwamba wananchi wake wanakwenda kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii. Chanzo cha maji ya Mitema ambacho kipo katika Jimbo la Newala Vijijini kina maji ya kutosha kiasi kwamba kama uwekezaji wa fedha utakuwa wa kutosha, tatizo la maji katika Jimbo ya Newala Vijijini, Newala Mjini, Tandahimba na baadhi ya Kata za Nanyama zitaondokana na shida ya maji. Je, ni lini Serikali itawekeza fedha za kutosha katika chanzo cha maji cha Mitema ili kuondoa kadhia ya maji kwa wananchi wa maeneo tajwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Newala Vijijini.

Lakini pia nimpongeze sana, juzi tuliweza kukutana pia na Mheshimiwa Mbunge wa Newala Mjini, baba yangu, mzee wangu, Mheshimiwa Kapteni Mkuchika, juu ya Mradi huu wa Makonde. Ni mradi wa muda mrefu sana ambao umekuwa na maneno mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie nikiwa mwenye dhamana ya Wizara ya Maji, Mheshimiwa Rais ametupa maelekezo mahususi kwa ajili ya Watanzania, waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Juzi tumekaa kikao baada ya mazungumzo yale, maelekezo ambayo tumeyatoa ni kwamba mradi ule tunakwenda kuuanza, iwe jua iwe mvua, ili wananchi wa Newala waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamis Tabasam, swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema ni kwamba Sengerema tunadaiwa pesa, shilingi milioni 300 kwa ajili ya umeme, na hili deni limekuwa la muda mrefu. Nini kauli ya Waziri kuhusiana na deni hilo ili tuanze kuanza upya, kwa sababu tumepata meneja mpya Sengerema? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Sengerema kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Ni haki ya mwananchi kupatiwa huduma ya maji. Na mwenye wajibu na jukumu la kumpatia huduma ya maji ni Wizara ya Maji, kwa maana ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sengerema ni eneo ambalo lilikuwa na changamoto sana ya maji. Serikali kwa dhamira

njema imewekeza mradi wa zaidi ya bilioni 25 wananchi wa Sengerema waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Sasa ni jukumu la Mamlaka ya Maji ya Sengerema kuhakikisha kwamba inakusanya bili na kulipia umeme ili uendeshaji wake uwe vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tuna changamoto ya uendeshaji; Meneja, kwa maana ya Mkurugenzi wa mamlaka ile nimemuondoa, fedha hizi za deni tutazilipa, lakini kwa masharti ya kuhakikisha kwamba wanajitegemea na wanaendesha mamlaka ile vizuri na wananchi wa Sengerema wanapata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kumekuwepo na tatizo kubwa la kukatika sana kwa maji katika Mji wa Munze, Kishapu, Kata ya Mwadui Lohumbo, na Maganzo. Lakini Mheshimiwa Waziri aliwahi kujibu kwamba tatizo kubwa ni malipo ya madeni ya muda mrefu ya wateja, lakini wateja wamelipia madeni yao kwa wakati. na hili nimefuatilia mwenyewe nimeona kwamba kweli hawadaiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufika katika Jimbo la Kishapu kujionea na kutoa utatuzi wa kudumu juu ya tatizo la kukatika kwa maji katika Mji wa Munze na maeneo mengine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana kaka yangu, Mbunge wa Kishapu; kwa kweli unafanya kazi kubwa na nzuri sana katika jimbo lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke wazi kabisa maeneo ambapo Serikali imewekeza miradi mikubwa kwa

ajili ya wananchi waweze kupata huduma ya maji, na wananchi wanalipia bili za maji ili kuhakikisha kwamba mamlaka inajiendesha, maeneo ambayo wananchi wanalipia bili zile za maji lakini wakurugenzi ama watendaji ambao wanashindwa kuendesha mamlaka hizo, hakuna neno lingine zaidi ya kutupisha. Tutaweka watu ambao wataweza kutuendesha ili mamlaka zetu ziweze kwenda na Watanzania waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na majibu kutoka upande wa Serikali. Na sasa nilete matangazo tuliyonayo hapa mbele.

Kwanza ni tangazo la wageni. Tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika.

Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Spika, ambaye ni Ndg. Mathew Mclean. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huyu aliwahi kuwa Makamu wa Rais wa *Millennium Challenge Corporation,* lakini pia alikuwa Mkuu wa Utumishi wa Ikulu wakati wa uongozi wa Rais Clinton na Rais George W. Bush. Kwa hiyo ameshashika nyadhifa mbalimbali. Karibu sana, sijajua kama anaongea Kiswahili ama vipi. *You may now be seated, thank you for coming. (Makofi)*

Tunao wageni wengine watano wa Mheshimiwa Spika ambao ni Ndg. Sarah Mwaluko.

Waheshimiwa Wabunge, huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Spika ambaye amesaidiwa kulipiwa ada ya Chuo Kikuu na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. *(Makofi)*

Nilimwambia asimame ili Waheshimiwa Wabunge tuwe tunaiga mifano mizuri kutoka kwa kiongozi wetu. Alimuona kwenye *TV* huyu binti akiwa anaponda mawe akitafuta ada kwenye kipindi kinachoendeshwa na Joyce

Mwakalinga wa Azam *TV.* Na baada ya kumuona huyo binti, Mheshimiwa Spika akachukua hatua ya kumlipia ada ya chuo kikuu na leo amekuja kumtembelea Mheshimiwa Spika. Karibu sana Sarah, na tutakutakia kila la heri katika masomo yako.

Jambo hili limetangazwa hapa mahsusi kabisa Waheshimiwa Wabunge kwanza tujifunze kuangalia vipindi vya *TV* ili tuone matatizo yaliyopo kwenye jamii zetu. Ahsante sana Sara unaweza kukaa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Sara alionekana kwenye kipindi hicho cha *AZAM TV* kinachoonyeshwa na Joyce Mwakalinga, Joyce Mwakalinga pia yupo hapa leo, yupo wapi Joyce Mwakalinga? Sijui amekaa wapi, lakini alipaswa kuwepo yeye na watoto wake; Ndugu Jadriana Mwakalinga, Ndugu Jaden Mwakalinga, Ndugu Angel Mwakalinga na Ndugu Witness Mwakalinga. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Joyce Mwakalinga yupo kule kwa Waandishi wa Habari.

**NAIBU SPIKA:** Sasa hapa sioni vizuri, ahaa yupo kazini, *okay* sawa nimekuona. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema kipindi kilikuwa kinaongozwa naye na ni vizuri tutoe wito kwa Waandishi wengine wa Habari, wanapoyaona haya mambo kwenye jamii basi wafuatilie halafu hizo habari zikisikika sehemu kubwa watoto wetu wanaweza kusaidiwa, si lazima watoto, lakini wenye changamoto wapo wengi kwenye jamii, changamoto zao zikifahamika itatusaidia. Ahsante sana Joyce Mwakalinga kwa kazi nzuri na tunakutakia kila kheri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ambao ni Ndugu Moreen Choholo, Ndugu Abigael Choholo, Ndugu Queenmaria Kusiga na Ndugu Belinda Mmasi. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Khadija Taya, ambao ni viongozi wa CCM Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka mikoa tofauti wakiongozwa na Ndugu Mariam Mungula. Karibuni sana viongozi wetu. Sijayapata majina yao lakini wote ni viongozi. Nilikuwa najaribu kuangalia karibu kabisa hapa namfahamu mmoja nafikiri huyu anaitwa Mariam alikuwa Katibu wa Wanawake, Wilaya ya Mbeya Mjini, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni 51 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii na hawa ni wanafunzi wa Shule ya *St. Joseph's Millennium School* ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Aaron Albin. Karibuni sana, tunashukuru kwa kuja kututembelea. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambaye ni Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, hawa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Jimbo la Kigamboni, Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Josiah Mufungo. Naona wamekaa upande huu, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 28 wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambaye ni Waziri wa Maji na hawa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Jimbo la Pangani wakiongozwa na Ndugu Keya Machanos. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Watawala wa Kimila wa Jimbo la Ilemela na sehemu ya Nyamagana, Mkoani Mwanza wakiongozwa na Chief Aron Mikomangwa. Karibuni sana viongozi wetu kutoka Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Angeline Mabula anao pia wageni wengine wawili ambao ni wananchuo kutoka Chuo cha *DECCA* cha Jijini Dodoma na hawa ni Ndugu Glads Leonidas na Ndugu Diana Pendael. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutulie kidogo tukumbushane, ukiona jirani yako anaongea mkumbushe kwamba nimesimama nitamtaja hapa. Hata ukiwa wewe unaongeleshwa kataa kuongeleshwa nikiwa nimesimama kwa sababu nitakutaja. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 15 wa Mheshimwa Hussein Bashe ambaye ni Naibu Waziri wa Kilimo na hawa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Malewa Richard. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Stephen Byabato ambaye ni Naibu Waziri wa Nishati na hawa ni wajasiliamali kutoka Nachingwea, Mkoani Lindi; Ndugu Mohamed Hamis na Ndugu Abdulazaq Seleman. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Neema Lugangira, ambao ni AZAKI ya kupambana na ajira kwa watoto kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Ibrahim Samatta. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 6 wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Jimbo la Mbulu Vijijini, Mkoani Manyara wakiongozwa na Ndugu Paskal Torojiki. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 98 wa Mheshimiwa Salome Makamba ambao wanatoka Shule ya Ignatus *Pre & Primary School* ya Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 6 wa Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe ambao ni ndugu na marafiki zake kutoka Kyela, Mkoani Mbeya wakiongozwa na Ndugu Seth Mwaisaka. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Hussein Amar ambao ni rafiki zake waendesha bodaboda na bajaji kutoka Makole Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Eliah Elia. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi ambao ni Makocha wa Mpira wa Miguu kutoka mikoa mbalimbali nchini wakiongozwa na Mwalimu wao Ndugu Makunja Luhaga. Karibuni sana makocha wetu. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 2 wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ambao ni Viongozi wa Dini ya Kiislamu kutoka Hai, Mkoani Kilimanjaro na hawa ni Sheikh Athuman Mtavangu na Ndugu Abuu Mwasha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 4 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni viongozi wa Kamati ya Siasa kutoka Jimbo la Mbozi wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Mbozi Ndugu Simon Mboya. Karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni 6, sasa hapa Waheshimiwa Wabunge niwaombe mnapopeleka majina kule kwa Makatibu, sijajua kama ni Makatibu ndiyo wamekosea jina ama ni ninyi hamkuandika vizuri sasa, hapa kuna vijana wa UVCCM kutoka Tarime Mkoani Mara wakiongozwa na Ndugu Somo Chacha, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa hawa sijajua ni wageni wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara au ni wageni wa Mheshimiwa Michael Kembaki; sijajua ni wageni wa yupi kati ya hao. Naambiwa hawa ni wageni wa Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki. Karibuni sana vijana wa UVCCM. *(Makofi)*

Tunao wageni 5 wa Mheshimiwa Mussa Mussa ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Amani Zanzibar, wakiongozwa na Mheshimiwa Makame Ame. Karibuni sana ndugu zetu kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wageni 5 kutoka Jijini Dodoma ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake wakiongozwa na Ndugu Martha Joseph. Karibuni sana. *(Makofi)*

Naliona kundi moja la watu hapo juu lakini sasa sijapata taarifa zao nikizipata basi nitawatangaza.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka Wizara ya Maliasili na Utalii, mnakumbushwa kuhusu lile tangazo ambalo limeshawahi kutolewa hapa kuhusu kutumbelea eneo la Hifadhi la Ngorongoro kuanzia tarehe 30 Juni baada ya kumaliza Bunge hadi tarehe 2 Julai, 2021. Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kuendelea kujiandikisha kama ambavyo mlitangaziwa lakini pia safari ipo leo baada ya kuahirisha vikao vya Bunge. Mnaombwa wale ambao hawajajiandikisha bado basi wanaweza kufanya hivyo eneo la mapokezi ya Bunge kwa maana ya pale nje mkitoka na mwisho wa kujiandikisha, sasa tangazo hili nilatoka saa nne kwa hiyo itabidi tusogeze muda wa kujiandikisha labda iwe mwisho saa tano ili wale ambao hawajajiandikisha waweze kwenda kujiandikisha.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, mnatangaziwa kwamba kutakuwa na kwenda kupanda Mlima Kilimanjaro mwezi Agosti, 2021. Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi wa Bunge wenye nia ya kwenda kupanda Mlima wa Kilimanjaro mwezi Agosti mnaombwa kujiandikisha kwa barua pepe au kwa namba 0789-141711, barua pepe mtaletewa hili tangazo kwenye vishikwambi vyenu mtaweza kuisoma.

Waheshimiwa Wabunge wenye nia ya kwenda kupanda mlima huu basi muanze kufanya mazoezi sasa. Mmi nilishapanda ule mlima, sijapanda mwaka huu, lakini nilishapanda  kwa hiyo naweza kuwapa ushauri ikiwa ni pamoja na kula vizuri maana kufanya tu mazoezi haitoshi, lakini unatakiwa kuwa na chakula mwilini kidogo mambo yakae vizuri. Kwa hiyo, nawatakia kila kheri wale wenye mpango huo. (Makofi)

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge tena, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Watendaji wa Shirika la Ndege Tanzania yaani *ATCL*, wapo katika viwanja vya Bunge kwa ajili ya kutambulisha huduma yao

mpya ya *Frequently Flyer Programme,* inamaanisha wale ambao huwa wanasafiri kwa kutumia chombo chetu hiki cha *Air Tanzania* pamoja na kusikiliza maoni yenu, lakini hiki wanachotaka kukifanya ni kuwafanya Waheshimiwa Wabunge ujiandikishe ili unapofanya safari yako basi unapata faida zaidi ya ile safari tu. Kwa hiyo, muende pale mkajiandikishe na wengine mkapate huduma wale mnaotaka kusafiri lakini wanayo mambo mengi mazuri kwa hiyo twende tukawatembelee.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo Kumi na Tatu kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo *[A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws)***

**na**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 ili kuboresha Masharti ya Sheria hiyo kwa kuondoa changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wake *[A Bill for an Act to Amend The Road Traffic Act, Cap.168, in order to address challenges encountered in the course of its enforcement)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umesomwa kwa Mara ya Kwanza na kwa utaratibu wetu utapelekwa kwenye Kamati inayohusika baada ya hapo mtapata fursa ya kujua yaliyomo kwenye Muswada huo.

Maadam umeshatangazwa, tuendelee kuusoma Muswada huo ili tutoe maoni yetu kwenye Kamati na pia wakati wa mjadala hapa Bungeni. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2021]***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada unasomwa kwa Mara ya Pili, kwa utaratibu wetu nimwite Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Prof. Adelardus Kilangi aje atoe hoja yake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2021]* katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2020, naomba kutoa Hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2021]* kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho sasa usomwe Mara ya Pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe Muswada huu kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia neema zake na kutuwezesha kukutana tena katika

Mkutano huu wa Tatu wa Bunge ambao unakamilika leo. Naomba pia nichukue fursa hii kumshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2021].*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuendelea kuiongoza nchi kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Nampongeza pia Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, niwapongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, niwapongeze viongozi mbalimbali walioteuliwa na Mheshimiwa Rais pamoja na Wabunge wapya waliochaguliwa kuwakilisha wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungazo wa Tanzania, Viongozi na wananchi wote kwa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli

aliyefariki dunia mnamo tarehe 17 Machi, 2020 na pia aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad na aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi Mheshimiwa Balozi John Kijazi pamoja na viongozi wengine waliotutangulia mbele ya haki katika kipindi hiki. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika na wewe Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Naishukuru Ofisi ya Bunge na Wabunge wote kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nikianzia na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Evaristo Emanuel Longopa, kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu sana na Bwana Onorius Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2021]* ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, napenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga

(Mbunge wa Viti Maalum) pamoja na Wajumbe maalum walioteuliwa kuungana na Kamati hii kutoka Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu mbele ya Kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa umakini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu na Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho, kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu, tarehe 26 Mei, 2017 Serikali za Uganda na Tanzania zilisaini Mkataba *(Inter-Governmental Agreement)* kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi na Uendeshaji wa Bomba litakalosafirisha mafuta ghafi kutoka Wilaya ya Hoima, nchini Uganda hadi Chongoleani, Tanga - Tanzania. Kufuatia kutiwa saini kwa Mkataba huo, tarehe 20 Mei, 2021 Serikali ya Tanzania ilisaini Mkataba mwingine *(Host Government Agreement)* na Kampuni ya Bomba la mafuta ghafi *(EACOP)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, tarehe 11 Aprili, 2021 Serikali ya Uganda ilisaini Mkataba kama huu na Kampuni hiyo ambayo ndiyo itakayosimamia na kuendesha Mradi huo. Mikataba hii yote kwa pamoja imeainisha masharti ambayo yanazitaka nchi zote mbili kutunga sheria mpya au kuzifanyia marekebisho baadhi ya sheria zao kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa mikataba hiyo. Kwa msingi huo, marekebisho yanayopendekezwa katika Muswada huu yanalenga kuwezesha kuanza kwa kutekelezwa kwa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mazingira ya Tanzania na hasa uwezekano wa kuwepo kwa miradi mingine kama hii, Serikali imeona ni vyema kufanya marekebisho ya Sheria Mbalimbali, kuwezesha utekelezaji wa mkataba huo na mikataba mingine ya aina hiyo, ambayo itaingiwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati na ambayo Serikali kupitia Baraza la Mawaziri imeridhia masharti hayo yatumike. Marekebisho hayo pia yatasaidia kuepusha Serikali kuingia kwenye migogoro,

inayotokana na ukiukwaji wa mikataba iliyoingiwa baina ya Serikali na wawekezaji wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2021, *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 3 Act, 2021)*, unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Kumi na Nne, kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta pamoja na miradi mingine yenye mikataba ya aina hiyo, inayotekelezwa au inayokusudiwa kutekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na kuongeza vifungu na vifungu vidogo vipya katika sheria husika, kwa lengo la kukidhi malengo ya jumla yaliyoelezwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kupitia Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

1. Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306;
2. Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191;
3. Sheria ya Ushindani, Sura ya 285;
4. Sheria ya Mashauri ya Serikali, Sura ya 5;
5. Sheria ya Bima, Sura ya 394;
6. Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287;
7. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
8. Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Miji, Sura ya 288;
9. Sheria ya Mamlaka ya Nchi ya Utajiri Asili na Mali Asilia, Sura ya 449;
10. Sheria ya Mapitio na Majadiliano Mapya Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Utajiri Asili na Mali Asilia, Sura ya 450;
11. Sheria ya Petroli, Sura ya 392;
12. Sheria ya Reli, Sura ya 170;
13. Sheria ya Barabara, Sura ya 167; na
14. Sheria ya Ubia Kati ya Sekta Binafsi na Umma, Sura ya 103.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi na Tano, ambapo Sehemu ya Kwanza ya Muswada unaainisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na Jina la Sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya Sheria Mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 6 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura ya 306 kinachohusu utoaji wa leseni ya mawasiliano ili kuitaka mamlaka husika inaposhughulikia maombi ya leseni kuhusu mradi, isiathiri makubaliano ya Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu inapendekeza kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 katika Kifungu cha 57, kinachozuia shughuli za kibinadamu kufanyika sehemu ya eneo la mita 60 la hifadhi ili kuweka masharti yatakayoitaka mamlaka husika kuruhusu pale inapohitajika shughuli zinahusiana na miradi ambayo Serikali imesaini mikataba yenye masharti maalum kufanyika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushindani, Sura ya 285 kwa kuongeza kifungu kipya cha 11A. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha mamlaka ya Tume katika vifungu vya 10 na 11, yanayohusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko na uunganishwaji na utwaaji wa makampuni yatekelezwe bila kukwamisha utekelezaji wa mkataba wa mradi wa Bomba la Mafuta wa Afrika Mashariki pamoja na mikataba mingine ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Tume ya Ushindani mamlaka ya kuongeza muda wa msamaha kwa zaidi ya miaka mitano kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa mikataba yenye masharti maalum iliyoingiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 16 cha Sheria ya Mashauri ya Serikali, Sura ya 5, kwa lengo la kuruhusu utekelezaji wa hukumu za mahakama kwa kukamata mali zinazohusiana na miradi ambayo kampuni imewekeza kwa mujibu wa mikataba maalum iliyoingiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Bima, Sura ya 394, ambapo Kifungu cha 133 chenye masharti kuhusu bima za miradi inayofanyika Tanzania, kukatwa kutoka makampuni ya hapa nchini, kinafanyiwa marekebisho ili kuruhusu miradi yenye mikataba maalum na iliyoridhiwa na Serikali kukatiwa bima kutoka makampuni ya nje hasa pale ambapo makampuni ya ndani yamekosa uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba, Nane na Tisa, zinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria za Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 na Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Miji, Sura ya 288. Marekebisho katika sheria hizi yanazitaka Mamlaka ya Serikali za Mitaa, wakati zinapotekeleza majukumu yake kama vile udhibiti, ukaguzi na utoaji wa leseni, zisiathiri masharti ya mkataba ya miradi ambayo imeingiwa na Serikali na yenye masharti mahususi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi, Kumi na Moja na Kumi na Tano, zinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Nchi ya Utajiri Asili na Mali Asilia, Sura ya 449 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano ya Masharti Hasi Katika Mikataba ya Utajiri Asili na Mali Asilia, Sura ya 450 na Sheria ya Ubia kati ya Sekta Binafsi na Umma, Sura ya 103. Marekebisho katika Sheria hizi yanapendekeza kufanya mabadiliko katika vifungu vinavyohusu wigo wa matumizi ya Sheria hizo ili masharti yake yasitumike kwenye miradi inayohusu rasilimali ambazo siyo za Tanzania kama ilivyo kwa Mradi wa *(EACOP)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Petroli,

Sura ya 392 ambapo kifungu cha 140 kinafanyiwa marekebisho ili kuifanya *EWURA* iweze kutekeleza mamlaka ya kiudhibiti, bila kuathiri utekelezaji wa miradi ambayo Serikali imeingia ubia na ambayo ina masharti mahususi kuhusu utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu na Kumi na Nne, zinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Reli, Sura ya 170 na Sheria ya Barabara, Sura ya 167 ili kuwezesha mamlaka husika kutekeleza majukumu yake bila kuathiri utekelezaji wa miradi ambayo yana masharti mahsusi kuhusu utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka, 2021 *(The Written Laws, Miscellaneous Amendments (No*. 3) *Act, 2021)* na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. ADERLADUS L. KILANGI, THE ATTORNEY GENERAL AT THE FIRST READING OF THE BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2021**

*(Made under S.O 99(10))*

A Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2021" is amended as follows:

**A:** In Clause 27 by deleting the proposed section 257A and substituting for it the following:

"Application in relation to agreements involving Government

**257A.** Where an agreement provides for special arrangement relating to the implementation of sections 29, 130(1) and (2), 131, 143, 149(1) and (2), 166, 167, 170, 181, 182, 194, 223, 251 and 253, and the said arrangement has been approved by the Cabinet, the application of the provisions of such sections shall not prejudice such arrangement.".

**B:** In Clause 31, by-

(a) deleting the reference to subsection (5) and substituting for it subsection (4); and

(b) designating the content of the proposed subsection (6) as subsection (5)."

Dodoma,
……………………, 2021

**ALK**
AG

ISSN 0856 - 01001X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***No. 8*** ***3rd June, 2021***

***SPECIAL BILL SUPPLEMENT***

*To the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.8. Vol.101 dated 3rd June, 2021*
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2021

ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section* *Title*

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.
2. Amendment of certain written laws.

PART II
AMENDMENT OF THE ELECTRONIC AND POSTAL COMMUNICATIONS ACT,
(CAP. 306)

3. Construction.
4. Amendment of section 6.

PART III
AMENDMENT OF THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT ACT,
(CAP. 191)

5. Construction.
6. Amendment of section 57.

PART IV
AMENDMENT OF THE FAIR COMPETITION ACT,
(CAP. 285)

7. Construction.
8. Amendment of section 12.
9. Amendment of section 14.

PART V
AMENDMENT OF THE GOVERNMENT PROCEEDINGS ACT,
(CAP. 5)

10. Construction.
11. Amendment of section 16.

PART VI
AMENDMENT OF THE INSURANCE ACT,
(CAP. 394)

12. Construction.
13. Amendment of section 133.

PART VII
AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT (DISTRICT AUTHORITIES) ACT,
(CAP. 287)

14. Construction.
15. Amendment of section 122.

PART VIII
AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT FINANCES ACT,
(CAP. 290)

16. Construction.
17. Amendment of section 11.

PART IX
AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT (URBAN AUTHORITIES) ACT,
(CAP. 288)

18. Construction.
19. Amendment of section 62.

PART X
THE NATURAL WEALTH AND RESOURCES (PERMANENT SOVEREIGNTY) ACT, (CAP. 449)

20. Construction.
21. Amendment of section 2.

PART XI
THE NATURAL WEALTH AND RESOURCES CONTRACTS (REVIEW AND RE-NEGOTIATION OF UNCONSCIONABLE TERMS) ACT, (CAP. 450)

22. Construction.
23. Amendment of section 2.

PART XII
AMENDMENT OF THE PETROLEUM ACT, (CAP. 392)

24. Construction.
25. Amendment of section 140.
26. Amendment of section 141.
27. Addition of section 257A.

PART XIII
AMENDMENT OF THE RAILWAYS ACT, (CAP. 170)

28. Construction.
29. Amendment of section 24.

PART XIV AMENDMENT OF THE ROADS ACT, (CAP. 167)

30. Construction.
31. Amendment of section 29.

PART XV
THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP ACT,
(CAP. 103)

32. Construction.
33. Amendment of section 2.

## NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dodoma,
2nd June, 2021

HUSSEIN A. KATTANGA
*Secretary to the Cabinet*

## A Bill

*for*

**An Act to amend certain written laws in order to facilitate the implementation of provisions of agreements that involve the Government and provide for special arrangement.**

**ENACTED** by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I PRELIMINARY
PROVISIONS

Short title

**1**. This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2021.

Amendment of certain written laws

**2.** The written laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner specified in their respective Parts.

PART II
AMENDMENT OF THE ELECTRONIC AND POSTAL COMMUNICATIONS ACT,
(CAP. 306)

Construction
Cap. 306

**3**. This Part shall be read as one with the Electronic and Postal Communications Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of section 6

**4.** The principal Act is amended in section 6 by adding immediately after subsection (6) the following:

"(7) Where an agreement provides for special arrangement relating to the implementation of this section, and the said arrangement has been approved by the Cabinet, the application of the provisions of this section shall not prejudice the implementation of such agreement.".

PART III
AMENDMENT OF THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT ACT, (CAP. 191)

Construction Cap. 191

**5**. This Part shall be read as one with the Environmental Management Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 57

**6.** The principal Act is amended in section 57, by adding a proviso under subsection (1) as follows:

"Provided that where an agreement provides for special arrangement relating to the implementation of this provision, and the said arrangement has been approved by the Cabinet, the application of the provisions of this section shall not prejudice the implementation of such agreement."; and

PART IV
AMENDMENT OF THE FAIR COMPETITION ACT, (CAP. 285)

Construction Cap. 285

**7**. This Part shall be read as one with the Fair Competition Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 12

**8.** The principal Act is amended in section 12, by-

(a) deleting a full stop appearing at the end of subsection (3) and substituting for it a semi colon; and

(b) adding the following proviso immediately after subsection (3):

"Provided that in the case of an agreement that provides for special arrangement relating to the grant of exemption for an agreement and such arrangement has been approved by the Cabinet, the Commission may, upon application, grant a period of more than five years.".

Amendment of section 14

**9.** The principal Act is amended in section 14, by adding immediately after subsection (5) the following:

"(6) Where an agreement provides for special arrangement relating to the implementation of sections 10 and 11, and the said arrangement has been approved by the Cabinet, the application of the provisions of this section shall not prejudice the implementation of such agreement.".

PART V
AMENDMENT OF THE GOVERNMENT PROCEEDINGS ACT, (CAP. 5)

Construction Cap. 5

**10**. This Part shall be read as one with the Government Proceedings Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 16

**11.** The principal Act is amended in section 16 by adding immediately after subsection (3) the following:

"(4) Notwithstanding subsection (3), where there is an agreement that provides for special arrangement relating to the execution, attachment or similar process and such arrangement has been approved by the Cabinet, the Court may, in the enforcement of financial obligation arising out of such agreement, issue an order for execution, attachment or similar process:

Provided that, the execution, attachment, or similar process is issued against the property which is connected with such agreement.".

## PART VI
## AMENDMENT OF THE INSURANCE ACT, (CAP. 394)

Construction Cap. 394

**12**. This Part shall be read as one with the Insurance Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 133

**13.** The principal Act is amended in section 133 by-

(a) adding immediately after subsection (3) the following:

"(4) Where there is an agreement that provides for special arrangement relating to the implementation of this provision, and the said arrangement has been approved by the Cabinet, the application of the provisions of subsection (3) shall not prejudice the implementation of such agreement.".

(b) renumbering subsection (4) as subsection (5).

## PART VII
## AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT (DISTRICT AUTHORITIES) ACT, (CAP. 287)

Construction Cap. 287

**14.** This Part shall be read as one with the Local Government (District Authorities) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 122

**15.** The principal Act is amended in section 122 by adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) Where an agreement provides for special arrangement relating to the implementation of this provision, and the

said arrangement has been approved by the Cabinet, the application of the provisions of paragraphs (w) and (z) of subsection (2) shall not prejudice the implementation of such agreement.".

## PART VIII
## AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT FINANCES ACT, (CAP. 290)

Construction Cap. 290

**16**. This Part shall be read as one with the Local Government Finances Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 11

**17.** The principal Act is amended in section 11 by adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) Where an agreement provides for special arrangement relating to the implementation of this provision, and the said arrangement has been approved by the Cabinet, the application of the provisions of this section shall not prejudice the implementation of such agreement.".

## PART IX
## AMENDMENT OF THE LOCAL GOVERNMENT (URBAN AUTHORITIES) ACT, (CAP. 288)

Construction Cap. 288

**18.** This Part shall be read as one with the Local Government (Urban Authorities) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 62

**19.** The principal Act is amended in section 62, by-

(a) adding immediately after subsection (1) the following:

"(2) Where an agreement provides for special arrangement relating to the implementation of this provision, and the said arrangement has been approved by the

Cabinet, the application of the provisions of subsection (1)(m) shall not prejudice the implementation of such agreement."; and

(b) renumbering subsection (2) as subsection (3).

PART X
THE NATURAL WEALTH AND RESOURCES (PERMANENT SOVEREIGNTY) ACT, (CAP. 449)

Construction Cap. 449

**20**. This Part shall be read as one with the Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 2

**21.** The principal Act is amended in section 2, by-

(a) designating the content of section 2 as subsection (1); and

(b) adding immediately after subsection (1) as designated the following:

"(2) Without prejudice to subsection (1), this Act shall not apply to an agreement that provides for special arrangement relating to transportation of natural resources that are not exploited in the United Republic and such arrangement has been approved by the Cabinet.

PART XI
THE NATURAL WEALTH AND RESOURCES CONTRACTS (REVIEW AND RE-NEGOTIATION OF UNCONSCIONABLE TERMS) ACT, (CAP. 450)

Construction Cap. 450

**22**. This Part shall be read as one with the Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 2

**23.** The principal Act is amended in section 2, by-

(a) designating the content of section 2 as subsection (1); and

(b) adding immediately after subsection (1) as designated the following:

"(2) Without prejudice to subsection (1), this Act shall not apply to an agreement that provides for special arrangement relating to transportation of natural resources that are not exploited in the United Republic and such arrangement has been approved by the Cabinet.

PART XII
AMENDMENT OF THE PETROLEUM ACT,
(CAP. 392)

Construction
Cap. 392

**24.** This Part shall be read as one with the Petroleum Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 140

**25.** The principal Act is amended in section 140, by-

(a) deleting a full stop appearing at the end of subsection (1) and substituting for it a colon; and

(b) adding a proviso immediately after subsection (1) as follows:

"Provided that, the powers exercised by EWURA under this subsection shall not affect the terms and conditions of any agreement that provides for special arrangement relating to transportation of natural resources and such arrangement has been approved by the Cabinet.".

Amendment of section 141

**26.** The principal Act is amended in section 141, by-

(a) adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) Where an application for renewal of licence has been duly made and the licence expires before EWURA grants or refuses

to renew the licence, the licence shall be deemed to continue in force until the grant or refusal of the application.”; and

(b) renumbering subsection (3) as subsection (4).

Addition of section 257A

**27.** The principal Act is amended by adding immediately after section 257 the following:

“Application in relation to agreements involving Government

**257A.** Where an agreement provides for special arrangement relating to the implementation of this provision, and that arrangement has been approved by the Cabinet, application of the provisions of sections 29, 130(1) and (2), 131, 143, 149(1) and (2), 166, 167, 170, 181, 182, 194, 223, 251 and 253 shall not prejudice the implementation such agreement.”.

## PART XIII
## AMENDMENT OF THE RAILWAYS ACT, (CAP. 170)

Construction Cap. 170

**28**. This Part shall be read as one with the Railways Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of section 24

**29.** The principal Act is amended in section 24 by adding immediately after subsection (3) the following:

“(4) Where an agreement provides for special arrangement relating to the implementation of this provision, and the said arrangement has been approved by the Cabinet, the application of the provisions of this section shall not prejudice the implementation of such agreement.”.

## PART XIV AMENDMENT OF THE ROADS ACT, (CAP. 167)

Construction Cap. 167

**30**. This Part shall be read as one with the Roads Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 29

**31.** The principal Act is amended in section 29 by adding immediately after subsection (5) the following:

"(6) Where an agreement provides for special arrangement relating to the implementation of this provision, and the said arrangement has been approved by the Cabinet, the application of the provisions of this section shall not prejudice the implementation of such agreement.".

## PART XV AMENDMENT OF THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIP ACT, (CAP. 103)

Construction Cap. 103

**32**. This Part shall be read as one with the Public Private Partnership Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 2

**33.** The principal Act is amended in section 2, by-

(a) designating the content of section 2 as subsection (1); and

(b) adding immediately after subsection (1) as designated the following:

"(2) Without prejudice to subsection (1), this Act shall not apply to an agreement that provides for special arrangement relating to transportation of natural resources that are not exploited in the United Republic and such arrangement has been approved by the Cabinet.

## OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes amendments to fourteen written laws, namely, the Electronic and Postal Communication Act, (Cap. 306), the Environmental Management Act, (Cap. 191), the Fair Competition Act, (Cap. 285), the Government Proceedings Act (Cap. 5), the Insurance Act, (Cap. 394), the Local Government (District Authorities) Act, (Cap. 287), the Local Government Finances Act, (Cap. 290), the Local Government (Urban Authorities) Act, (Cap. 288), the Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449 ), the Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, (Cap. 450), the Petroleum Act, (Cap. 392), the Railways Act, (Cap. 167), the Roads Act, (Cap. 167) and Public Private Partnership Act, (Cap. 103).

This Bill is divided into fifteen Parts.

Part I deals with preliminary provisions which include the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended, are amended in their respective Parts.

Part II, III, VI, VII, VIII, IX, X, XI, XII, XIII, XIV and XV proposes to amend the Electronic and Postal Communication Act, Cap. 306 the Environmental Management Act, (Cap. 191), the Insurance Act, (Cap. 394), the Local Government (District Authorities) Act, (Cap. 287), the Local Government Finances Act, (Cap. 290), the Local Government (Urban Authorities) Act, (Cap. 288), the Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449 ), the Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, (Cap. 450), the Petroleum Act, (Cap. 392), the Railways Act, (Cap. 167), the Roads Act, (Cap. 167) and Public Private Partnership Act, (Cap. 103) respectively. The proposed amendments intend to provide for smooth and expeditious implementation of agreements entered by the Government that provides for the execution of special arrangements, and to create favourable conditions for performance of Government projects.

Part IV of the Bill proposes to amend the Fair Competition Act, Cap. 285, by adding section 11A in order to prevent the application of provisions of sections 10 and 11 which provides for misuse of market power and procedure for merger and acquisition in order to facilitate smooth operation of the EACOP Project and other projects of the Government. Further, a proviso is added to section 12 by empowering the Commission to grant exemption to contracts for a period longer than five years in order to facilitate and create favourable conditions for performance of Government projects that provides for special arrangements.

Part V of the Bill proposes to amend section 16 of the Government Proceedings Act, Cap. 5, in order to secure investors or parties to the agreements by allowing execution, attachment or similar process against the property which is connected with financial obligation arising out of, or in connection with an agreement involving the government.

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Kumi na Nne ambazo ni Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta, Sura ya 306, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, Sheria ya Ushindani, Sura ya 285, Sheria ya Mashauri ya Serikali, Sura ya 5, Sheria ya Bima, Sura ya 394, Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji, Sura ya 288, Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili za Nchi, Sura ya 449, Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba Inayohusu Maliasili za Nchi, Sura ya. 450, Sheria ya Petroli, Sura ya 392, Sheria ya Reli, Sura ya 170, Sheria ya Barabara, Sura ya 167 na Sheria ya Ubia kati ya Sekta Binafsi na Umma, Sura ya 103.

Muswada huu umegawayika katika Sehemu Kumi na Tano.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi na yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho zilivyoainishwa katika Sehemu husika ya Muswada.

Sehemu ya Pili, Tatu, Sita, Saba, Nane, Tisa, Kumi, Kumi na Moja, Kumi na Mbili, Kumi na Tatu, Kumi na Nne na Kumi na Tano za Muswada zinapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta, Sura ya 306, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, Sheria ya Bima, Sura ya 394, Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji, Sura ya 288, Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili za Nchi, Sura ya 449, Sheria ya Mapitio na Majadilioano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba Inayohusu Maliasili za Nchi, Sura ya 450, Sheria ya Petroli, Sura ya 392,-Sheria ya Reli, Sura ya 170, Sheria ya Barabara, Sura ya 167 na Sheria ya Ubia Kati ya Sekta Binafsi na Umma, Sura ya 103. Mapendekezo ya marekebisho katika Sheria hizi yanakusudia kuwezesha utekelezaji bora na wa ufanisi wa miradi mbalimbali ambayo Serikali imeingia na ambayo yana masharti maalum.

Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushindani, Sura ya 285 kwa kuongeza kifungu kipya cha 11A. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha mamlaka ya Tume katika vifungu vya 10 na 11 yanayohusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko na uunganishwaji na utwaaji wa makampuni yatekelezwe bila kukwamisha utekelezaji wa mkataba wa mradi wa Bomba la Mafuta wa Afrika Mashariki pamoja na mikataba mingine ya aina hiyo. Vilevile kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Tume ya Ushindani mamlaka ya kuongeza muda wa msamaha kwa zaidi ya miaka mitano kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa mikataba yenye masharti maalum iliyoingiwa na Serikali.

Sehemu ya Tano inapendekeza kurekebisha kifungu cha 16 cha Sheria ya Mashauri ya Serikali, Sura ya 5, kwa lengo la kuruhusu utekelezaji wa hukumu za mahakama kwa kukamata mali zinazohusiana na miradi ambayo kampuni imewekeza kwa mujibu wa mikataba yenye masharti maalum iliyoingiwa na Serikali.

Dodoma,
01 Juni, 2021

ADELARDUS L. KILANGI
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wetu wa Serikali. *(Makofi)*

Sasa kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati, wapo wageni mbalimbali ambao hawakupata nafasi ya kutambulishwa. Wapo wageni wa Mheshimiwa Husna Sekiboko; ambao ni mtoto wake na watoto wa ndugu zake. karibuni sana. Mtoto wake anaitwa Anwar Kibasa, karibu sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni nane wa Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, ambao ni watoto wake na watoto wa ndugu zake, sijui wamekaa upande gani? Haya naona ndio wanaingia, mwenyewe alikuwa hajajua bado. Karibuni sana Bungeni wageni wa Mheshimiwa Stella Fiyao. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Sylivia Sigula, sijui kama yupo humu ndani! Huyu ni dada yake anatoka Mwanza, karibu sana, sana. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, aje atusomee maoni kwa niaba yetu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabisa, naomba taarifa yote ya Kamati kama ilivyowasilishwa Mezani iingie kwenye *Hansard* au kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya Mwaka, 2021 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (Act, No. 3) of 2021)*, kwa mujibu ya Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulisomwa kwa Mara ya Kwanza hapa Bungeni tarehe 25 Juni, 2021, katika Kikao cha Hamsini na Tisa cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili. Muswada huo ulitakiwa ushughulikiwe kwa hatua zake zote kwa kuwa uliwasilishwa kwa Hati ya Dharura kwa mujibu wa Kanuni ya 93(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(16) na Kifungu cha 7(1) (b) na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huo uliletwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati iliujadili Muswada huu kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, kutokana na maudhui na umuhimu wa Muswada huu, uliwateua baadhi ya Wabunge kutoka kwenye Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kuwa Wajumbe waalikwa katika Vikao vya Kamati vya kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021, una lengo la kuzifanyia marekebisho Sheria Mbalimbali Kumi na Nne (14), ili kuwezesha utekelezaji wa mikataba inayohusiana na Mradi wa Ujenzi na Uendeshaji wa Bomba linalosafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima – Uganda hadi Chongoleani, Tanga – Tanzania na miradi mingine ya kimkakati. Miradi hiyo ni ile itakayotekelezwa na Serikali kwa ushirika au ubia na sekta binafsi au nchi nyingine. Orodha ya Sheria hizo zinazorekebishwa ni kama ilivyobainishwa kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo mantiki ya marekebisho yanayopendekezwa, naomba kueleza msingi wa marekebisho ya Sheria 14, kwa kila sheria inayoguswa na Muswada huu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta, Sura ya 306 *(The Electronic and Postal Communication Act, (Cap. 306))* Sheria hii iliyotungwa kwa lengo la kuweka masharti ya usimamizi wa sekta ya mawasiliano ya kielektoniki na posta nchini, kwa sasa Muswada huu unapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 6, ambacho kinahusu uombaji wa leseni ya kufanya shughuli za mawasiliano ya kielektoniki na posta nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufafanua madhumuni na marekebisho, naomba kueleza kwa ufupi, maudhui ya Kifungu cha 6 kinachofanyiwa marekebisho. Kifungu hiki kinaweka masharti kwa mtu yeyote anayetaka kufanya shughuli za mawasiliano ya kielectroniki, posta au kutoa huduma ya maudhui kuomba leseni kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania yaani *Tanzania Communications Regulatory Authority (TCRA)*. Fasili ya Pili ya Kifungu hicho cha 6(2) kinabainisha mahitaji yanayopaswa kuwasilishwa wakati wa maombi ya leseni kuwa ni Cheti cha Usajili wa Kampuni, Mpango wa Kazi wa Huduma Zinazotarajiwa Kutolewa, mkakati wa kitaalamu wa huduma hizo, muundo wa umiliki wa hisa, uzoefu, uthibitisho wa uwezo wa kifedha pamoja na taarifa nyingine kadri *TCRA* itakavyohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kifungu cha 6(3) kinaweka masharti mahususi yanayopaswa kuzingatiwa na mwombaji wa leseni ya mawasiliano ya kielektroniki. Pamoja na masharti ya kifungu hicho, Masharti ya Kifungu cha 6(4) na (5), yanataka mwombaji wa leseni kuwa na anuani ya makazi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuijulisha *TCRA* iwapo itatokea mabadiliko ya anuani hiyo. Vilevile, Kifungu cha 6(6) kinamtaka mwombaji wa leseni aliyekidhi masharti, kuwasilisha *TCRA* mpango mkakati wa uendeshaji na wa kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano, Kamati inakubaliana na mapendekezo na marekebisho katika kifungu hiki kwa kuwa yanakusudia kuongeza Kifungu kipya cha 6(7) ambacho kinaeleza kuwa, "endapo kuna mkataba ambao unaweka masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa Kifungu hiki cha 6 na pale ambapo mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu hiki hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 *(The Environmental Management Act, (Cap. 191))* ilitungwa kwa lengo la kuweka muundo wa kisheria na taasisi kwa ajili ya usimamizi endelevu wa mazingira katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira. Kifungu cha 57 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kinahusu uzuiaji wa shughuli za kibinadamu katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 57(1) kinaeleza kuwa, kwa kuzingatia Kifungu cha 57(2), hakutafanyika shughuli yoyote ya binadamu ya kudumu au ambayo kwa asili yake inaweza kuhatarisha na kuathiri vibaya ulinzi wa mazingira au utunzaji wa bahari au kingo za mto, bwawa, au miambao ya asili ya ziwa ndani ya mita sitini. Kifungu cha 57(2) kinaeleza kuwa Waziri mwenye dhamana ya mazingira anaweza kuweka, miongozo ya kuendesha shughuli za binadamu ndani ya maeneo yaliyoelezwa kwa mujibu wa Kifungu cha 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maudhui ya sheria hii na baada ya kupata ufafanuzi wa kina wa Serikali kuhusu mapendekezo na marekebisho, Kamati inakubaliana na mapendekezo katika kifungu hiki kwa kuwa yanakusudia kuongeza nyongeza katika Kifungu cha 57(1), inayoeleza kuwa, pale panapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki na mkataba huo ukiwa umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu hiki hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ushindani wa Biashara, Sura ya 285 *(The Fair Competition Act, (Cap. 289))* - kuwezesha ushindani wenye tija katika biashara, kuwalinda walaji pamoja na masuala ya kupambana na bidhaa bandia. Kifungu cha 12 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kipo katika Sehemu ya Pili ya Sheria hii, ambayo inahusu masuala mbalimbali yasiyoruhusiwa katika biashara. Mathalani, Kifungu cha 8 cha Sheria hii kinakataza utekelezaji wa mikataba inayozuia ushindani katika biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kifungu cha 12 kinaweka masharti ambayo mtu anaweza kuwasilisha maombi kwenye Tume ya Ushindani wa Biashara ili iweze kutoa ruhusa au msamaha *(exemption)* kwa mkataba ambao unaweza kuzuia kuwepo kwa ushindani wa kibiashara. Ruhusa au msamaha huo unaweza kuwa masharti au usiokuwa na masharti.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mambo yanayozingatiwa katika kutoa ruhusa hiyo, ni iwapo mkataba unaohusika unatoa manufaa makubwa zaidi kwa Umma kwa kuongeza tija kwenye uzalishaji, kuhamasisha maendeleo ya teknolojia na kiuchumi, kuongeza tija kwenye mgawanyo wa rasilimali au kutunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, marekebisho ya Kifungu cha 12(3) ambacho kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kinaeleza kuwa, Tume ya Ushindani wa Biashara inapokuwa inatoa ruhusa au msamaha kwenye mkataba kwa mujibu wa kifungu hiki, ruhusa au msamaha huu utakuwa ni kwa kipindi kisichozidi miaka mitano. Vile vile, kifungu cha 14 kinaweka masharti mengine, ambayo yanaweza kuzingatiwa katika kutoa ruhusa au misamaha ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Kamati inakubaliana na msingi wa mapendekezo ya marekebisho katika kifungu cha 12, kwa kuwa mapendekezo hayo yanakusudia kuweka nyongeza katika kifungu cha 12(3) kinachoeleza kwamba: “Pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki, na mkataba huo

umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, inapotokea kuna maombi yamewasilishwa, Tume ya Ushindani wa Biashara itatoa ruhusa au msamaha kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano."

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu kipya cha 14(6) kinachopendekezwa kuongezwa kinaeleza kuwa: "Pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalum kuhusu utekelezaji wa kifungu cha 10 kinachohusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko na kifungu cha 11 kinachohusu uunganishaji na utwaaji wa makampuni na pale ambapo mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu hiki hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mashauri ya Serikali, Sura ya 5 yaani *The Government Proceedings Act (Cap. 5).* Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuweka utaratibu wa kuzingatia katika mashauri ya madai yanayoihusu Serikali pamoja na haki nyingine za Serikali. Kifungu cha 16 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu utekelezaji wa amri za mahakama zinazotolewa dhidi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 16(1) kinaeleza kuwa: "Inapotokea mtu amepata amri ya mahakama ya kulipwa gharama na Serikali, anaweza kuiomba mahakama impatie hati yenye maelezo ya amri hiyo."

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu cha 16(2) kinaeleza kuwa: "Iwapo hati hiyo inaeleza gharama zinazohusika zitalipwa kwa madai kwa njia ya fedha taslimu au kwa nafuu nyingine, gharama hizo zitalipwa na Katibu Mkuu - Hazina au Afisa Masuuli mwingine wa Serikali."

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kifungu cha 16(3) kinaeleza kuwa: "Hakutakuwa na amri ya utekelezaji wa amri ya mahakama itakayotolewa nje ya mahakama kwa ajili ya kushinikiza malipo ya gharama zilizotajwa katika kifungu hiki kutoka Serikalini."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo na baada ya majadiliano ya kina kuhusu marekebisho ya yanayopendekezwa, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kifungu kidogo kipya cha 16(4) kinachopendekezwa kuongezwa na kinachoeleza kuwa: "Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 16(3), pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalum kuhusu utekelezaji wa amri ya mahakama au utaratibu mwingine wa kimahakama, na iwapo mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi mahakama inaweza, katika utekelezaji wa wajibu wa kulipa fedha unaotokana na mkataba huo, kuamuru utekelezaji wa amri ya mahakama au utaratibu mwingine wa kimahakama."

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, angalizo linapendekezwa katika Muswada huu kuwa, utekelezaji wa amri ya mahakama au ukamataji wa mali au utaratibu mwingine wa kimahakama uwe umetolewa dhidi ya mali ambayo inahusiana na mkataba tu na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Bima, Sura ya 394 yaani *The Insurance Act, (Cap. 394);* Sheria hii ilitungwa kwa ajili ya kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania yenye jukumu la kuratibu, kusimamia sera na mambo mengine yanayohusu bima nchini. Kifungu cha 133 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu bima zilizopo chini ya Kampuni ya Bima ya Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 133(1) kinaeleza kuwa: "Mkaazi wa Tanzania au kampuni ya Kitanzania inapotaka kuweka bima ya aina yoyote, ni lazima bima hiyo iwekwe na Kampuni ya Bima ya Kitanzania."

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 133(2) kinafafanua kuwa: "Iwapo hakuna Kampuni ya Bima ya Kitanzania inayoweza kuweka bima hiyo, basi bima hiyo inaweza kutolewa na Kampuni ya Bima ambayo siyo Tanzania mara baada ya kupata idhini ya Kamishna wa Mamlaka ya Bima nchini."

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kifungu cha 133(3) kinaeleza kuwa: "Kwa madhumuni ya masharti ya kifungu cha 133(1) na (2), bima ya mzigo unaoingizwa nchini kwa njia ya ardhi, maji au anga itawekwa na Kampuni ya Bima ya Kitanzania."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, kifungu kipya cha 133(4) kinachopendekezwa kuongezwa, kinaeleza kuwa: "Pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalum kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 133(3) hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287 yaani *The Local Government (District Authorities) Act, (Cap. 287);* Sheria hii ilitungwa kwa lengo la ugatuzi wa madaraka nchini na kuweka masharti bora ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya Nchini. Kifungu cha 122 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu masharti ya jumla kuhusu majukumu na kazi za Halmashauri za Wilaya Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 122(2)(w) kinazipa halmashauri za wilaya mamlaka ya kuweka utaratibu wa usimamizi, udhibiti, ukaguzi, ufuatiliaji na utoaji wa leseni za kumbi za masuala ya kijamii, starehe na maeneo mengine ya burudani. Aidha, kifungu cha 122(2)(z) kinazipa mamlaka halmashauri kutoa leseni, kusimamia na kufuatilia biashara na shughuli nyingine kwa kadri Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI atakavyoelekeza kupitia Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kifungu kipya cha 122(3) kinachopendekezwa kuongezwa, ambacho kinaeleza kuwa: "Pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalum kuhusu utekelezaji wa kifungu cha 122 na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 122(2)(w) na (z) hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 yaani *The Local Government Finances Act, Cap 290;* Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kubainisha vyanzo vya mapato vya Mamlaka za Serikali za Mitaa, usimamizi wa mapato hayo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kifungu cha 11 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kinahusu uteuzi wa mamlaka za utoaji wa leseni katika halmashauri kwa aina fulani ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 11(1) kinaziteua halmashauri kuwa mamlaka za utoaji wa leseni kwa biashara mbalimbali kama vile biashara za viwanda vidogo, biashara ya kupiga simu, wajasiriamali wadogo, madalali, migahawa, nyumba za kulala wageni na biashara nyinginezo. Kifungu cha 11(2) kinaeleza kuwa: "Fedha zinazokusanywa kwa mujibu wa kifungu hiki zitahesabiwa kuwa ni mapato ya halmashauri na matumizi yake yatakuwa ni kwa ajili ya halmashauri husika."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na kifungu kipya cha 11(3) kinachopendekezwa na kinachoeleza kuwa: "Pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalum kuhusu utekelezaji wa kifungu cha 11 na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu hicho hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji, Sura ya 288 yaani *The Local Government (Urban Authorities) Act, (Cap. 288);* Sheria hii ilitungwa kwa lengo la ugatuzi wa madaraka na kuweka masharti bora ya usimamizi wa Halmashauri za Miji Nchini. Kifungu cha 62 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu kazi za halmashauri hizo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 62(1)(m) kinazipa halmashauri hizo mamlaka ya kudhibiti biashara yoyote yenye kudhuru au hatarishi kwa afya ya umma au hatarishi kwa umma kwa ujumla au biashara ambayo maslahi ya umma yanahitaji idhibitiwe. Kifungu hiki pia kinazipa

mamlaka halmashauri, katika kufanya udhibiti wa biashara hizo, kutoa leseni au vibali na kuweka ada ya leseni au vibali hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na kifungu kipya cha 62(2) kinachoelekeza kuwa: "Pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalum kuhusu utekelezaji wa kifungu cha 62, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 62(1)(m) hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili za Nchi, Sura ya 449 yaani *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449);* Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuweka masharti yanayohusiana na misingi iliyomo katika mikataba na itifaki mbalimbali ambazo Tanzania imesaini na kuridhia. Kifungu cha 2 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu matumizi ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hicho kinaeleza kuwa, sheria hiyo itatumika katika pande zote za Muungano yaani Tanzania Bara na vile vile Tanzania Zanzibar, lakini pasipo kuathiri mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kumiliki na kusimamia rasilimali zake yenyewe kwa mujibu wa Katiba na sheria za Zanzibar kuhusu rasilimali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na kifungu kipya cha 2(2) kinachoeleza kuwa: "Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha (1), Sheria hii haitatumika pale ambapo kuna mkataba ambao una masharti maalum kuhusu usafirishaji wa rasilimali ambayo haivunwi ndani ya Jamhuri ya Muungano na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba Inayohusu Maliasili za Nchi, Sura ya 450 yaani *The Natural Wealth and*

*Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, (Cap. 450)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii ilitungwa kuweka utaratibu ambao wananchi kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaweza kupitia na kujadili makubaliano na mikataba yote inayohusu rasilimali za Nchi kwa lengo la kujiridhisha endapo mikataba hiyo haikinzani na maslahi ya Taifa. Kifungu cha 2 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu matumizi ya sheria hiyo kwa pande zote za Muungano na marekebisho yanayopendekezwa ni kama ilivyo katika Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili za Nchi, Sura ya 449 yaani *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Petroli, Sura ya 392 *yaani The Petroleum Act, (Cap. 392);* Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kusimamia mkondo wa juu, kati na chini wa shughuli za petroli nchini, kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu, kuanzisha Kampuni ya Taifa ya Mafuta pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 25 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 140 kinachohusu mabadiliko ya leseni. Kifungu cha 140(1) kinaipa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati *(The Energy and Water Utilities Regulatory Authority-EWURA*) uwezo wa kubadilisha vigezo na masharti ya leseni ya petroli kwa shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini kwa kuamua yenyewe au baada ya kupokea maombi. Pale inapotokea *EWURA* imeamua yenyewe kufanya mabadiliko, itapaswa kutoa taarifa ya nia hiyo kwa mwenye leseni kwa angalau siku sitini kabla ya mabadiliko hayo kwa mujibu wa kifungu cha 140(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na nyongeza inayopendekezwa katika kifungu cha 140(1), kinachoeleza kuwa, mamlaka ya *EWURA* chini

ya kifungu hiki hayataathiri vigezo na masharti vya mkataba wowote ambao una masharti maalum kuhusu usafirishaji wa rasilimali ambao umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri ili kuwezesha na kurahisisha upatikanaji wa leseni husika pale itakapohitajika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 26 inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 141. Kifungu hiki kinahusu uhuishaji wa leseni ambapo kifungu cha 141(1) kinamtaka mwenye leseni ya petroli ya shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini anayekusudia kuhuisha leseni yake kuwasilisha maombi yake kwa *EWURA* kwa angalau miaka miwili kabla leseni hiyo haijaisha muda wake. Kifungu cha 141(2) kinaeleza kuwa; "Leseni inaweza kuhuishwa kwa kipindi cha miaka kumi na tano au kwa muda mwingine ambao ni mrefu zaidi, kwa kadri itakavyoamuliwa na EWURA."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kifungu kipya cha 141(3) yanayoeleza kuwa: "Endapo maombi ya kuhuisha leseni yamefanyika ipasavyo na leseni ikawa inaisha muda wake kabla EWURA hawajafanya uamuzi wa kuihuisha au kukataa kuihuisha, leseni hiyo itachukuliwa kuwa inaendelea hadi pale uamuzi wa kuhuisha au kukataa kuhuisha utakapotolewa kwa kuwa yanalenga kuvutia wawekezaji na kutokwamisha utekelezaji wa miradi husika."

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 27 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 257A. Kifungu cha 257A kinachopendekezwa kuongezwa kinahusu utekelezaji wa baadhi ya masharti ya sheria pale kunapokuwa na mkataba unaoihusu Serikali. Kifungu hicho kinaeleza kuwa: "Endapo kuna mkataba ambao una masharti maalum kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, matumizi ya vifungu vifuatavyo hayataathiri utekelezaji wa mkataba huo. Vifungu vinavyoguswa na marekebisho hayo ni kama vilivyoainishwa na kubainishwa kwenye taarifa hii."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Reli, Sura ya 170 yaani *The Railways Act, (Cap. 167);* Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuanzisha Shirika la Reli nchini, madhumuni yake pamoja na majukumu yake ni pamoja na kusimamia, kuendeleza miundombinu ya reli na kutoa huduma za usafiri wa reli. Kifungu cha 24 kinahopendekezwa kufanyiwa marekebisho kinahusu usimamizi wa njia za reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 24(1) kinapiga marufuku kufanya shughuli za kibinadamu kama vile kuchunga mifugo, kulima au kujenga isipokuwa kwa kibali cha maandishi kutoka Shirika la Reli. Endapo mtu yeyote atafanya shughuli za kibinadamu bila kibali cha maandishi, Shirika linaweza kuujulisha umma kwa tangazo katika Gazeti la Serikali au katika gazeti linalosambazwa zaidi, kumpa mtu anayehusika notisi ya maandishi inayomtaka kubomoa au kurekebisha ujenzi huo ndani ya siku thelathini kwa mujibu wa kifungu cha 42(2). Kifungu cha 24(3) kinaeleza kuwa: “Endapo mtu hatabomoa alichokijenga katika njia ya reli ndani ya muda aliopewa, Shirika litabomoa na mtu anayehusika atawajibika kulipia gharama za ubomoaji.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na nyongeza ya kifungu kipya cha 24(4) kinachoeleza kuwa: “Pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalum kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 24 hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo.”

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Barabara, Sura ya 167 yaani *The Roads Act, (Cap. 167);* Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuweka utaratibu wa kugharamia barabara, kuziendeleza, kuzifanyia matengenezo na kuzisimamia. Kifungu cha 29 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kinahusu matumizi ya maeneo ya hifadhi ya barabara. Kifungu cha 29(1) kinaeleza kuwa: “Maeneo ya hifadhi za barabara ni mahsusi kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa barabara pekee au kwa matumizi ambayo yanahusiana na barabara.”

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mamlaka ya barabara inaweza kutoa kibali cha maandishi kwa mtu yeyote kutumia eneo la hifadhi ya barabara kwa muda mfupi kwa lengo la kutoa huduma kama vile kuweka taa za barabarani, matangazo, simu, usambazaji wa umeme na posta, mitaro ya maji pamoja na mabomba ya maji safi na maji taka pale ambapo huduma hizo hazitazuia matumizi ya baadaye ya barabara kwa mujibu wa kifungu cha 29(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 29(3) kinaeleza kuwa: "Mtumiaji wa maeneno ya hifadhi ya barabara ataruhusiwa kutumia maeneo hayo kwa vigezo na masharti ambayo yatawekwa na mamlaka inayosimamia barabara inayohusika."

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo itatokea eneo linalohusika linahitajika kwa ajili ya uendelezaji, matengezo au upanuzi barabara au mahitaji mengine yanayohusiana na barabara, mtumiaji huyo atapaswa kuondoa huduma hiyo kwa gharama zake na kulifanyia eneo linalohusika matengenezo na hakutakuwa na fidia. Aidha, endapo kutatokea uharibifu katika barabara au mazingira yanayolizunguka eneo la hifadhi ya barabara kutokana na matumizi yaliyoidhinishwa, mtu anayehusika na matumizi hayo yaliyoleta uharibifu atapaswa kurekebisha uharibifu uliojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na nyongeza ya kifungu kipya cha 29(6) kinachoeleza kuwa: "Pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalum kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 29 hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ubia kati ya Sekta Binafsi na Umma, Sura ya 103 yaani *Public Private Partnership Act, (Cap. 103)*; Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa mikataba ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miongozo na

taratibu za kusimamia mfumo huo, uendelezaji na utekelezaji wa mfumo wa PPP, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na mfumo huo. Kifungu cha 2 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kinahusu matumizi ya sheria hiyo ambapo imeelezwa kwamba sheria hiyo itatumika Tanzania Bara katika miradi ambayo inatekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika**,** kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kifungu kipya cha 2(2) kinachopendekezwa kuongezwa kinaeleza kuwa: “Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 2(1), sheria hii haitatumika katika mkataba ambao una masharti maalum ya usafirishaji wa rasilimali ambayo haivunwi ndani ya Jamhuri ya Muungano na mkataba huo uwe umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri.”

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati; kama nilivyoeleza katika sehemu ya Maudhui na Uchambuzi wa Muswada, Kamati inakubaliana na mependekezo yote ya marekebisho katika Muswada huu. Kamati imezingatia kuwa marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kuwezesha utekelezaji wa shughuli za kila siku za miradi ya kimkakati inayotekelezwa au inayokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa ubia na Sekta binafsi au mataifa mengine kwa kuzingatia makubaliano ya washirika au wabia katika mradi unaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati inashauri Ibara ya 25B inayopendekeza kuweka nyongeza katika kifungu cha 140(1) iboreshwe ili kuweka bayana kuwa rasilimali zinazohusika katika kifungu hicho ni zile ambazo hazivunwi ndani ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyo katika Ibara ya 21, Ibara ya 23 na Ibara ya 33 ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ukubwa na upekee wa mradi huu wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanzania, ni vema Serikali ikafanya utafiti na kutafakari endapo kuna umuhimu, kwa siku za mbeleni, Bunge lako

Tukufu kutunga sheria mahsusi itakayohusu usimamizi, udhibiti, ukaguzi, ufuatiliaji pamoja na mambo mengine yanayohusiana na mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe mwenye kunipa fursa hii, lakini pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika kwa kuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Katiba na Sheria, jukumu ambalo limetekelezwa na Kamati kwa wakati na kwa ufanisi uliokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheheshimiwa Profesa Aderladus Lubango Kilangi, Mbunge bila kumsahau Ndugu Onorius Njole Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali yaani *CPD* kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru Waziri na Naibu Waziri wa Nishati ambao ni Mheshimiwa Medard Kalemani na Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato na Watendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kwa maelezo ya ufafanuzi waliyoyatoa kwa Kamati. Maelezo yao yameisaidia sana Kamati kwa kutoa ufafanuzi wa hoja kwa Wajumbe wote wa kuweza kupata kuelewa nia ya Serikali juu ya umuhimu na mapendekezo ya marekebisho yaliyomo kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na wale wote ambao tulikuwa nao walioteuliwa na Mheshimiwa Spika. Naomba majina ya Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, kwa uongozi thabiti uliofanikisha uratibu wa shughuli za Kamati hii. Nawashukuru pia Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein;

Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald S. Magili; na Wanasheria wa Bunge, Ndugu Matamus Anangisye Fungo, Ndugu Stephano Seba Mbutu, Ndugu Mossy Lukuvi na Ndugu Rehema Lazarus Kipera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nawashukuru sana Makatibu wa Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Sheria Ndogo, ambao ni Ndugu Stanslaus Kagisa na Ndugu Mkuta Masoli, Ndugu Chacha Timasi Nyakega na Ndugu Eunike Shirima ambao ni Makatibu wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na Wasaidizi wa Kamati Ndugu Rachel Masima na Cletty Urassa waliofanikisha kazi ya uchambuzi, ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo yote Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kukubali kujadili na kupitisha Muswada huu kwa maslahi mapana ya Taifa pamoja na uchumi wa ukanda huu wa Afrika Mashariki kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, noamba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA. 3) WA MWAKA 2021 (*THE WRITTEN LAWS MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, (NO. 3) 2021)* – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, ***AWALI YA YOTE, NAOMBA TAARIFA YOTE YA KAMATI KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI IINGIZWE KWENYE TAARIFA RASMI ZA BUNGE (HANSARD).***

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa

Mwaka 2021 **(*The Written Laws Miscellaneous Amendments) Act, No.3 of 2021)***, kwa mujibu ya **Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.**

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 **(*The Written Laws Miscellaneous Amendments) Act, (No. 3)2021)* ulisomwa** Bungeni Mara ya Kwanza tarehe 25 Juni, 2021, katika Kikao cha Hamsini na Tisa (59) cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili. Muswada huo ulitakiwa kushughulikiwa kwa hatua zake zote kwa kuwa uliwasilishwa kwa Hati ya Dharura kwa mujibu wa **Kanuni ya 93(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.**

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya hatua hiyo, Muswada huo uliwasilishwa kwanza kwenye Kamati ya Uongozi ukiwa umeambatishwa na Hati ya Dharura. Kamati ya Uongozi ilijiridhisha kuwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 **(*The Written Laws Miscellaneous Amendments) Act, (No. 3)2021)*** unastahili kuwasilishwa kwa Hati ya Dharura kwa mujibu wa Kanuni ya 93(4) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa **Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge** uliuleta Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa mapema iwezekanavyo. ***Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Kamati iliujadili Muswada huu kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, kutokana na maudhui na umuhimu wa Muswada huo uliwateua baadhi ya Wabunge kutoka kwenye Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kuwa Wajumbe waalikwa katika Vikao vya Kamati vya kuchambua Muswada huu***.

### 1.1 SHERIA ZINAZOPENDEKEZWA KUFANYIWA MAREKEBISHO

**Mheshimiwa Spika,** Mtoa Hoja alieleza Kamati Kuwa, **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali**

**(Na. 3) wa Mwaka 2021 una lenga kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali Kumi na Nne(14) ili kuwezesha utekelezaji wa mikataba inayohusiana na Mradi wa Ujenzi na Uendeshaji wa Bomba litakalosafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima – Uganda hadi Chongoleani, Tanga – Tanzania na miradi mingine ya kimkakati.** Miradi hiyo ni ile itakayotekelezwa na Serikali kwa ushirika au ubia na sekta binafsi au nchi nyingine. Orodha ya Sheria hizo zinazorekebishwa ni kama ilivyobainishwa kwenye Taarifa hii.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Marekebisho yanayopendekezwa na Msingi wake

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo mantiki ya marekebisho yanayopendekezwa, naomba kueleza msingi wa marekebisho ya Sheria Kumi na nne (14), kwa kila Sheria inayoguswa na Muswada huu kama ifuatavyo:-

#### 2.1.1 Sheria ya Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta, Sura ya 306 *(The Electronic and Postal Communications Act, (Cap. 306)*

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuweka masharti ya usimamizi wa sekta ya mawasiliano ya kielektoniki na posta nchini. Kwasasa Muswada huu unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 6 ambacho kinahusu uombaji wa leseni ya kufanya shughuli za mawasiliano ya kielektoniki na posta nchini.

**Mheshimiwa Spika**, ili kufafanua madhumuni ya marekebisho naomba kueleza kwa kifupi maudhui ya Kifungu cha 6 kinachofanyiwa marekebisho. Kifungu hiki kinaweka masharti kwa mtu yeyote anayetaka kufanya shughuli za mawasiliano ya kielectroniki, posta au kutoa huduma ya maudhui kuomba leseni kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(Tanzania Communications Regulatory Authority – TCRA)*. Fasili ya Pili ya Kifungu hicho (cha 6(2)) kinabainisha mahitaji yanayopaswa kuwasilishwa wakati wa maombi ya leseni kuwa ni cheti cha usajili wa kampuni, mpango kazi wa

huduma zinazotarajiwa kutolewa, mkakati wa kitaalamu wa huduma hizo, muundo na umiliki wa hisa, uzoefu, uthibitisho wa uwezo wa kifedha pamoja na taarifa nyingine kadri *TCRA* itakavyohitaji.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kifungu cha 6(3) kinaweka masharti mahsusi yanayopaswa kuzingatiwa na muombaji wa leseni ya mawasiliano ya kielektroniki. Pamoja na masharti ya kifungu hicho, Masharti ya kifungu cha 6(4) na (5), yanataka muombaji wa leseni kuwa na anuani ya makazi ndani ya Jamhuri ya Muungano na kuijulisha *TCRA* iwapo itatokea mbadiliko ya anuani hiyo. Vilevile, kifungu cha 6(6) kinamtaka muombaji wa leseni aliyekidhi masharti kuwasilisha *TCRA* mpango mkakati wa uendeshaji na wa kitaalamu.

**Mheshimiwa Spika**, ***baada ya majadiliano Kamati inakubaliana na mapendekezo ya marekebisho katika kifungu hiki kwa kuwa yanakusudia kuongeza kifungu kipya cha 6(7) ambacho kinaeleza kuwa, endapo kuna mkataba ambao umeweka masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki cha 6, na pale ambapo mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu hiki hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo.***

**2.1.2 Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 *(The Environmental Management Act, (Cap. 191)***

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuweka muundo wa kisheria na taasisi kwa ajili ya usimamizi endelevu wa mazingira katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira. Kifungu cha 57 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kinahusu uzuiaji wa shughuli za binadamu katika baadhi ya maeneo.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 57(1) kinaeleza kuwa, kwa kuzingatia kifungu cha 57(2), hakutafanyika shughuli yoyote ya binadamu ya kudumu au ambayo kwa asili yake inaweza kuhatarisha au kuathiri vibaya ulinzi wa mazingira na, au utunzaji wa bahari au kingo za mto, bwawa, au miambao

ya asili ya ziwa ndani ya mita sitini. Kifungu cha 57(2) kinaeleza kuwa Waziri mwenye dhamana ya mazingira anaweza kuweka miongozo ya kuendesha shughuli za binadamu ndani ya maeneo yaliyoelezwa kwa mujibu wa kifungu cha (1).

**Mheshimiwa Spika,** ***hivyo, kutokana na maudhui ya sheria hii na baada ya kupata ufafanuzi wa kina wa Serikali kuhusu mapendekezo ya marekebisho, Kamati inakubaliana na mapendekezo katika kifungu hiki kwa kuwa yanakusudia kuweka nyongeza katika kifungu cha 57(1) inayoeleza kuwa, pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki, na mkataba huo ukiwa umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu hiki hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo***.

### 2.1.3 Sheria ya Ushindani wa Biashara, Sura ya 285 *(The Fair Competition Act, (Cap. 285)*

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuwezesha ushindani wenye tija katika biashara, kuwalinda walaji pamoja na masuala ya kupambana na bidhaa bandia. Kifungu cha 12 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kipo katika Sehemu ya Pili ya sheria hii ambayo inahusu masuala mbalimbali yasiyoruhusiwa katika biashara. Mathalani, kifungu cha 8 cha sheria hii kinakataza utekelezaji wa mikataba inayozuia ushindani katika biashara.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, kifungu cha 12 kinaweka masharti ambayo yanawezesha mtu kuwasilisha maombi kwenye Tume ya Ushindani wa Biashara ili iweze kutoa ruhusa au msamaha (*exemption)* kwa mkataba ambao unaweza kuzuia kuwepo kwa ushindani wa kibiashara. Ruhusa au msamaha huo unaweza kuwa wa masharti au usiyokuwa na masharti.

Miongoni mwa mambo yanayozingatiwa katika kutoa ruhusa hiyo ni iwapo mkataba inaohusika unatoa manufaa makubwa zaidi kwa umma kwa kuongeza tija kwenye uzalishaji, kuhamasisha maendeleo ya kiteknolojia na

kiuchumi, kuongeza tija kwenye mgawanyo wa rasilimali au kutunza mazingira. Aidha, kifungu cha 12(3) ambacho kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kinaeleza kuwa Tume ya Ushindani wa Biashara inapokuwa inatoa ruhusa au msamaha kwenye mkataba kwa mujibu wa kifungu hiki, ruhusa au msamaha huo utakuwa ni kwa kipindi kisichozidi miaka mitano. Vile vile, kifungu cha 14 kinaweka masharti mengine ambayo yanaweza kuzingatiwa katika kutoa ruhusa au msamaha ya mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, ***hivyo, Kamati inakubaliana na msingi wa mapendekezo ya marekebisho katika kifungu cha 12 kwa kuwa mapendekezo hayo yanakusudia kuweka nyongeza katika kifungu cha 12(3) inayoeleza kuwa, pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, inapotokea kuna maombi yamewasilishwa, Tume ya Ushindani wa Biashara itatoa ruhusa au msamaha kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano. Aidha, kifungu kipya cha 14(6) kinachopendekezwa kuongezwa kinaeleza kuwa, pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu cha 10 kinachohusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko na kifungu cha 11 kinachohusu uunganishaji na utwaaji wa makampuni, na pale ambapo mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu hiki hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo.***

### 2.1.4 Sheria ya Mashauri ya Serikali, Sura ya 5 *(The Government Proceedings Act (Cap. 5)*

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuweka utaratibu wa kuzingatia katika mashauri ya madai yanayoihusu Serikali pamoja na haki nyingine za Serikali. Kifungu cha 16 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu utekelezaji wa amri za mahakama zinazotolewa dhidi ya Serikali.

Kifungu cha 16(1) kinaeleza kuwa, inapotokea mtu amepata amri ya mahakama ya kulipwa gharama na Serikali, anaweza

kuiomba mahakama impatie hati yenye maelezo ya amri hiyo. Aidha, kifungu cha 16(2) kinaeleza kuwa iwapo hati hiyo inaeleza gharama zinazohusika zitalipwa kwa mdai kwa njia ya fedha taslimu au kwa nafuu nyingine, gharama hizo zitalipwa na Katibu Mkuu-Hazina au Afisa Masuuli mwingine wa Serikali.

Hata hivyo, kifungu cha 16(3) kinaeleza kuwa hakutakuwa na amri ya utekelezaji wa amri ya mahakama itakayotolewa nje ya mahakama kwa ajili ya kushinikiza malipo ya gharama zilizotajwa katika kifungu hiki kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, na baada ya majadiliano ya kina kuhusu marekebisho ya yanayopendekezwa, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kifungu kidogo kipya cha 16(4) kinachopendekezwa kuongezwa kinachoeleza kuwa, bila ya kujali masharti ya kifungu cha 16(3), pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa amri ya mahakama au au utaratibu mwingine wa kimahakama, na iwapo mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi mahakama inaweza, katika utekelezaji wa wajibu wa kulipa fedha unaotokana na mkataba huo, kuamuru utekelezaji wa amri ya mahakama au utaratibu mwingine wa kimahakama.**

***Hata hivyo, angalizo linapendekezwa katika Muswada huu kuwa, utekelezaji wa amri ya mahakama au ukamataji wa mali au utaratibu mwingine wa kimahakama uwe umetolewa dhidi ya mali ambayo inahusiana na mkataba tu na si vinginevyo.***

**2.1.5 Sheria ya Bima, Sura ya 394 *(The Insurance Act, (Cap. 394)***

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa ajili ya kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania yenye jukumu la kuratibu, kusimamia sera na mambo mengine yanayohusu bima nchini. Kifungu cha 133 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu bima zilizopo chini ya kampuni ya bima ya Kitanzania.

Kifungu cha 133(1) kinaeleza kuwa, mkaazi wa Tanzania au kampuni ya Kitanzania inapotaka kuweka bima ya aina yoyote, ni lazima bima hiyo iwekwe na kampuni ya bima ya Kitanzania. Kifungu cha 133(2) kinafafanua kuwa, iwapo hakuna kampuni ya bima ya kitanzania inayoweza kuweka bima hiyo, basi bima hiyo inaweza kutolewa na kampuni ya bima ambayo siyo Tanzania mara baada ya kupata idhini ya Kamishna wa Mamlaka ya Bima nchini. Aidha kifungu cha 133(3) kinaeleza kuwa, kwa madhumuni ya masharti ya kifungu cha 133(1) na (2), bima ya mzigo unaoingizwa nchini kwa njia ya ardhi, maji au anga itawekwa na kampuni ya bima ya Kitanzania.

**Mheshimiwa Spika,** ***kwa msingi huo, kifungu kipya cha 133(4) kinachopendekezwa kuongezwa kinaeleza kuwa, pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 133(3) hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo.***

### 2.1.6 Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287 *(The Local Government (District Authorities) Act, (Cap. 287)*

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa lengo la ugatuzi wa madaraka nchini na kuweka masharti bora ya usimamizi wa halmashauri za wilaya nchini. Kifungu cha 122 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu masharti ya jumla kuhusu majukumu na kazi za halmashauri za wilaya nchini.

Kifungu cha 122(2)(w) kinazipa halmashauri za wilaya mamlaka ya kuweka utaratibu wa usimamizi, udhibiti, ukaguzi, ufuatiliaji na utoaji wa leseni za kumbi za masuala ya kijamii, starehe na maeneo mengine ya burudani. Aidha, kifungu cha 122(2)(z) kinazipa mamlaka halmashauri kutoa leseni, kusimamia na kufuatilia biashara na shughuli nyingine kwa kadri Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI atakavyoelekeza kupitia Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** ***kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kifungu kipya cha 122(3) kinachopendekezwa kuongezwa ambacho kinaeleza kuwa, pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu cha 122, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 122(2)(w) na (z) hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo.***

**2.1.7 Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290** ***(The Local Government Finances Act, Cap 290)***

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa lengo la kubainisha vyanzo vya mapato vya mamlaka za serikali za mitaa, usimamizi vya mapato hayo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kifungu cha 11 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kinahusu uteuzi wa mamlaka za utoaji wa leseni katika halimashauri kwa aina fulani ya biashara.

Kifungu cha 11(1) kinaziteua halmashauri kuwa mamlaka za utoaji wa leseni kwa biashara mbalimbali kama vile biashara za viwanda vidogo, biashara ya kupiga simu, wajasiriamali wadogo, madalali, migahawa, nyumba za kulala wageni na biashara nyinginezo. Kifungu cha 11(2) kinaeleza kuwa fedha zinazokusanywa kwa mujibu wa kifungu hiki zitahesabiwa kuwa ni mapato ya halmashauri na matumizi yake yatakuwa ni kwa ajili ya halmashauri husika.

**Mheshimiwa Spika,** ***kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na kifungu kipya cha 11(3) kinachopendekezwa kinachoeleza kuwa, pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu cha 11, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu hicho hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo.***

**2.1.8 Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji, Sura ya 288** ***(The Local Government (Urban Authorities) Act, (Cap. 288)***

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa lengo la ugatuzi wa madaraka nchini na kuweka masharti bora ya usimamizi

wa halmashauri za miji nchini. Kifungu cha 62 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu na kazi za halmashauri hizo nchini.

Kifungu cha 62(1)(m) kinazipa halmashauri hizo mamlaka ya kudhibiti biashara yoyote yenye kudhuru au hatarishi kwa afya ya umma au hatarishi kwa umma kwa ujumla au biashara ambayo maslahi ya umma yanahitaji idhibitiwe. Kifungu hiki pia kinazipa mamlaka halmashauri, katika kufanya udhibiti wa biashara hizo, kutoa leseni au vibali na kuweka ada ya leseni au vibali hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** ***kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na kifungu kipya cha 62(2) kinachopendekezwa kinachoeleza kuwa, pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu cha 62, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 62(1)(m) hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo.***

**2.1.9 Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili za Nchi, Sura ya 449 *(The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449)***

**Mheshimiwa Spika;** Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuweka masharti yanayohusianisha misingi iliyomo katika mikataba na itifaki mbalimbali ambazo Tanzania imesaini na kuridhia. Kifungu cha 2 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu matumizi ya sheria hiyo.

Kifungu hicho kinaeleza kuwa, sheria hiyo itatumika katika pande zote za Muungano yaani Tanzania Bara na vile vile Tanzania Zanzibar lakini pasipo kuathiri mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kumiliki na kusimamia rasilimali zake yenyewe kwa mujibu wa Katiba na sheria za Zanzibar kuhusu rasilimali.

**Mheshimiwa Spika,** ***kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na kifungu kipya cha 2(2) kinachopendekezwa kinachoeleza kuwa, bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha (1), Sheria hii***

***haitatumika pale ambapo kuna mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu usafirishaji wa rasilimali ambayo haivunwi ndani ya Jamhuri ya Muungano, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri.***

**2.1.10 Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba Inayohusu Maliasili za Nchi, Sura ya 450 *(The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, (Cap. 450)***

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kuweka utaratibu ambapo wananchi kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaweza kupitia na kujadili makubaliano na mikataba yote inayohusu rasilimali za nchi kwa lengo la kujiridhisha endapo mikataba hiyo haikinzani na maslahi ya Taifa. Kifungu cha 2 kinachopendekezwa kurekebishwa kinahusu matumizi ya sheria hiyo kwa pande zote za Muungano na marekebisho yanayopendekezwa ni kama ilivyo katika Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili za Nchi, Sura ya 449 *(The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, (Cap. 449)*.

**2.1.11 Sheria ya Petroli, Sura ya 392 *(The Petroleum Act, (Cap. 392)***

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa lengo la kusimamia mkondo wa juu, kati na chini wa shughuli za petrol nchini, kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu, kuanzisha Kampuni ya Taifa ya Mafuta pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

**(d) Ibara ya 25 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 140 kinachohusu mabadiliko ya leseni**

Kifungu cha 140(1) kinaipa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati *(The Energy and Water Utilities Regulatory Authority-EWURA*) uwezo wa kubadilisha vigezo na masharti ya leseni ya petrol ya shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini kwa kuamua yenyewe au baada ya kupokea

maombi. Pale inapotokea EWURA imeamua yenyewe kufanya mabadiliko, itapaswa kutoa taarifa ya nia hiyo kwa mwenye leseni kwa angalau siku sitini kabla ya mabadiliko hayo kwa mujibu wa kifungu cha 140(2).

**Mheshimiwa Spika, *kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na nyongeza inayopendekezwa katika kifungu cha 140(1) kinachoeleza kuwa, mamlaka ya EWURA chini ya kifungu hiki hayataathiri vigezo na masharti vya mkataba wowote ambao una masharti maalumu kuhusu usafirishaji wa rasilimali ambao umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri ili kuwezesha na kurahisisha upatikanaji wa leseni husika pale itakapohitajika.***

**(e) Ibara ya 26 inayopendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 141**

Kifungu hiki kinahusu uhuishaji wa leseni ambapo kifungu cha 141(1) kinamtaka mwenye leseni ya petrol ya shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini anayekusudia kuhuisha leseni yake kuwasilisha maombi yake kwa EWURA kwa angalau miaka miwili kabla leseni hiyo haijaisha muda wake. Kifungu cha 141(2) kinaeleza kuwa, leseni inaweza kuhuishwa kwa kipindi cha miaka kumi na tano au kwa muda mwingine ambao ni mrefu zaidi, kwa kadri itakavyoamuliwa na EWURA.

**Mheshimiwa Spika, *kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kifungu kipya cha 141(3) yanayoeleza kuwa, endapo maombi ya kuhuisha leseni yamefanyika ipasavyo na leseni ikawa inaisha muda wake kabla EWURA hawajafanya uamuzi wa kuihuisha au kukataa kuihuisha, leseni hiyo itachukuliwa kuwa inaendelea hadi pale uamuzi wa kuhuisha au kukataa kuhuisha utakapotolewa kwa kuwa yanalenga kuvutia wawekezaji na kutokwamisha utekelezaji wa mradi husika.***

**(f) Ibara ya 27 inayopendekeza kuongeza kifungu kipya cha 257A**

Kifungu cha 257A kinachopendekezwa kuongezwa kinahusu utekelezaji wa baadhi ya masharti ya sheria pale

kunapokuwa na mkataba unaoihusu Serikali. Kifungu hicho kinaeleza kuwa, endapo kuna mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, matumizi ya vifungu vifutavyo hayataathiri utekelezaji wa mkataba huo. Vifungu vinavyoguswa na marekebisho hayo ni kama vilivyoainishwa na kubainishwa kwenye taarifa hii.

### 2.1.12 Sheria ya Reli, Sura ya 170 *(The Railways Act, (Cap. 167)*

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuanzisha Shirika la Reli nchini, madhumuni yake pamoja na majukumu yake ikiwa ni pamoja na kusimamia, kuendeleza miundombinu ya reli na kutoka huduma za usafiri wa reli. Kifungu cha 24 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kinahusu usimamizi wa njia za reli.

Kifungu cha 24(1) kinapiga marufuku kufanya shughuli za kibinadamu kama vile kuchunga mifugo, kulima au kujenga isipokuwa kwa kibali cha maandishi kutoka Shirika la Reli. Endapo mtu yeyote atafanya shughuli za kibinadamu bila kibali cha maandishi, Shirika linaweza kuujulisha umma kwa tangazo katika Gazeti la Serikali au katika gazeti linalosambazwa zaidi, kumpa mtu anayehusika notisi ya maandishi inayomtaka kubomoa au kurekebisha ujenzi huo ndani ya siku thelathini kwa mujibu wa kifungu cha 42(2).

Kifungu cha 24(3) kinaeleza kuwa endapo mtu hatabomoa alichokijenga katika njia ya reli ndani ya muda aliopewa, Shirika litabomoa na mtu anayehusika atawajibika kulipia gharama za ubomoaji.

**Mheshimiwa Spika,** ***kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na nyongeza ya kifungu kipya cha 24(4) kinachoeleza kuwa, pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 24 hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo***.

### 2.1.13 Sheria ya Barabara, Sura ya 167 *(The Roads Act, (Cap. 167)*

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuweka utaratibu wa kugharamia barabara, kuziendeleza, kuzifanyia matengenezo na kuzisimamia. Kifungu cha 29 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kinahusu matumizi ya maeneo ya hifadhi ya barabara.

Kifungu cha 29(1) kinaeleza kuwa, maeneo ya hifadhi za barabara ni mahsusi kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa barabara pekee au kwa matumizi ambayo yanahusiana na barabara. Hata hivyo, mamlaka ya barabara inaweza kutoa kibali cha maandishi kwa mtu yeyote kutumia eneo la hifadhi ya barabara kwa muda mfupi kwa lengo la kutoa huduma kama vile kuweka taa za barabarani, matangazo, simu, usambazaji wa umeme na posta, mitaro ya maji pamoja na mabomba ya maji safi na maji taka pale ambapo huduma hizo hazitazuia matumizi ya baadaye ya barabara kwa mujibu wa kifungu cha 29(2).

Kifungu cha 29(3) kinaeleza kuwa, mtumiaji wa maeneno ya hifadhi ya barabara ataruhusiwa kutumia maeneo hayo kwa vigezo na masharti ambayo yatawekwa na mamlaka inayosimamia barabara inayohusika. Endapo itatokea eneo linalohusika linahitajika kwa ajili ya uendelezaji, matengezo au upanuzi barabara au mahitaji mengine yanayohusiana na barabara, mtumiaji huyo atapaswa kuondoa huduma hiyo kwa gharama zake na kulifanyia eneo linalohusika matengenezo na hakutakuwa na fidia.

Aidha, endapo kutatokea uharibifu katika barabara au mazingira yanayolizunguka eneo la hifadhi ya barabara kutokana na matumizi yaliyoidhinishwa, mtu anayehusika na matumizi hayo yaliyoleta uharibifu atapaswa kurekebisha uharibifu uliojitokeza.

**Mheshimiwa Spika,** ***kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na nyongeza ya kifungu kipya cha 29(6) kinachoeleza kuwa, pale kunapokuwa na mkataba ambao una masharti***

***maalumu kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki, na mkataba huo umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri, basi utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 29 hautaathiri utekelezaji wa mkataba huo***.

### 2.1.14 Sheria ya Ubia kati ya Sekta Binafsi na Umma, Sura ya 103 *(Public Private Partnership Act, (Cap. 103)*

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa lengo la kuweka mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa mikataba ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miongozo na taratibu za kusimamia mfumo huo, uendelezaji na utekelezaji wa mfumo wa PPP pamoja na mambo mengine yanayohusiana na mfumo huo. Kifungu cha 2 kinachopendekezwa kufanyiwa marekebisho kinahusu matumizi ya sheria hiyo ambapo imeelezwa kwamba sheria hiyo itatumika Tanzania Bara katika miradi ambayo inatekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** ***kwa msingi huo, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya kifungu kipya cha 2(2) kinachopendekezwa kuongezwa kinaeleza kuwa, bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 2(1) sheria hii haitatumika katika mkataba ambao una masharti maalumu ya usafirishaji wa rasilimali ambayo haivunwi ndani ya Jamhuri ya Muungano, na mkataba huo uwe umeidhinishwa na Baraza la Mawaziri***.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza katika sehemu ya Maudhui na uchambuzi wa Muswada, Kamati inakubaliana na mependekezo yote ya marekebisho katika Muswada huu. Kamati imezingatia kuwa marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kuwezesha utekelezaji wa shughuli za kila siku za miradi ya kimkakati inayotekelezwa au inayokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa ubia na Sekta binafsi au mataifa mengine kwa kuzingatia makubaliano ya washirika au wabia katika mradi unaohusika.

***Hata hivyo, Kamati inashauri Ibara ya 25(b) inayopendekeza kuweka nyongeza katika kifungu cha 140(1) iboreshwe ili kuweka bayana kuwa rasilimali zinazohusika katika kifungu hicho ni zile ambazo hazivunwi ndani ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyo katika Ibara ya 21, Ibara ya 23 na Ibara ya 33 ya Muswada.***

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia ukubwa na upekee wa mradi huu wa bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanzania, ni vema Serikali ikafanya utafiti na kutafakari endapo kuna umuhimu, kwa siku za mbeleni, Bunge lako Tukufu kutunga sheria mahsusi itakayohusu usimamizi, udhibiti, ukaguzi, ufuatiliaji pamoja na mambo mengine yanayohusiana na mradi huo.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Katiba na Sheria ili iweze kuufanyia kazi, jukumu ambalo limetekelezwa na Kamati kwa wakati na kwa ufanisi uliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Prof. Aderladus Lubango Kilangi, Mb bila kumsahau Ndugu Onorius Njole Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwashukuru Waziri na Naibu Waziri wa Nishati ambao ni Mhe.Medard Kalemani (Mb) na Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato, (Mb) na Watendaji wa Wizara na Taasisi zilizochini ya Wizara hiyo kwa maelezo ya ufafanuzi waliyoyatoa kwa Kamati. Maelezo yao yameisaidia sana Kamati kwa kutoa ufafanuzi wa hoja za Wajumbe na hivyo kuwezesha kupata uelewa zaidi wa nia ya Serikali na umuhimu wa mapendekezo ya marekebisho yaliyomo kwenye Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na Wajumbe wengine uliowateua kuungana na Wajumbe wa Kamati kwa weledi, uvumilivu, umahiri na kujituma kwao wakati wa kuufanyia kazi Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. **NAOMBA MAJINA YAO YAINGIZWE KWENYE KUMBUKUMBU RASMI ZA BUNGE (HANSARD).**

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, kwa Uongozi thabiti uliofanikisha uratibu wa shughuli za Kamati hii. Nawashukuru pia Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald S.Magili, na Wanasheria wa Bunge, Ndg. Matamus Anangisye Fungo, Ndg. Stephano Seba Mbutu, Ndg. Mossy Lukuvi na Ndg. Rehema Lazarus Kipera.

Kipekee kabisa nawashukuru sana Makatibu wa Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Sheria Ndogo, ambao ni Ndg. Stanslaus Kagisa na Ndg.Mkuta Masoli, Ndg. Chacha Timasi Nyakega na Ndg. Eunike Shirima ambao ni Makatibu wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na Wasaidizi wa Kamati Ndg.Rachel Masima na Cletty Urassa waliofanikisha kazi ya uchambuzi, ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** ***baada ya maelezo yote hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuukubali, kuujadili na kuupitisha Muswada huu kwa maslahi mapana ya Taifa pamoja na uchumi wa ukanda huu wa Afrika Mashariki kwa ujumla.***

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Najma Murtaza Giga, Mb<br>
**MAKAMU MWENYEKITI**<br>
**KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**<br>
30 JUNI, 2021

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu kwa kazi nzuri mliyoifanya wewe pamoja na wajumbe wengine wa kamati na wajumbe wengine ambao Mheshimiwa Spika aliwapa kazi ya kushirikiana nanyi. Waheshimiwa Wabunge sasa kwa utaratibu wetu ninayo majina hapa ya Wabunge mbalimbali ambao wanataka kuchangia hoja hii, kwa hivyo tutaanza kuchangia halafu badaye tutaendelea na ratibu kwa kadri ya utaratibu wetu wa utungaji sheria. Tutaanza na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhani Suleiman Ramadhani, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kupata nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza wa Muswada huu. La kwanza niishukuru Serikali kwa hatua hii ambayo wamefikia katika mkataba huu muhimu kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu, nadhani hii ni hatua muhimu ya kuifungua nchi yetu kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassani amekuwa akisisitiza kwamba lazima tufungue nchi yetu ili tuweze kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hatua hii inatuma ujumbe mwafaka kabisa kwa Dunia kwamba Tanzania sasa haiko kwa ajili ya mikataba tu ya kuhifadhi ya wakimbizi na kusuluhisha migogoro ya kimataifa, tuko pia kwa ajili ya mikataba hii muhimu ya uchumi ambayo haigusi Tanzania peke yake lakini inagusa dunia pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa mfupi tu kama ambavyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amewasilisha kwa umarihiri kabisa kwamba hii ni *intergovernmental agreement* ambayo sisi siyo wa kwanza kuanza mkataba kama huu, mikataba kama hii iko sehemu nyingi duniani na hasa maeneo ya Asia. Nimejaribu kupitia *intergovernmental agreement* ya *dry ports* ambayo katika nchi za Asia na *Pacific* imehusisha nchi zaidi ya 16, halafu iko *intergovernmental agreement* ya Asia na *high way network* ambayo imehusisha nchi zaidi ya 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangali hii mikataba yote katika ibara ya ile ya tatu huwa liko sharti moja ambalo linaweka vitu inaita *options* mbili, ya kwanza ni kwamba nchi inayotia saini mkataba haina sheria au aijaingia kwenye mikataba mingine ambayo itazuia au kukwamisha utekelezaji wa mkataba husika *option* ya kwanza, na ya pili ni kwamba hatutatunga sheria au kuingia katika mikataba inayozuia utekelezaji wa mkataba huu. Sasa nadhani hili sasa kwa kuitikia hilo ndiyo maana Muswada huu ukawa umeletwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na tusingefanya hivyo hata wawekezaji tusingepata kwa sababu mkataba ambao haujazingatia hii Act 3 (3) unachukuliwa kwamba ni *low security agreement* yaani ni mkataba ambao una-*risk* kubwa kwa hiyo hauwi *bankable* hamuwezi kupata mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hii nzuri ambayo imefikiwa mimi labda nishauri kwa sababu mkataba unaweza mzuri sana na mara nyingi matatizo ya mkataba huwa hayaanzi mwanzoni, matatizo yanakuja baadaye wakati wa utekelezaji changamoto mbalimbali zinapoanza kutokeza au pengine hata faida zinapoanza kupatikana ndipo matatizo huwa yanaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali inahitaji kuwa na timu ya wataalamu kwa ajili ya usimamizi wa mkataba huu, katika hizi hii mikataba mingine miwili niliyoitaja ya kimataifa wana kitu kinaitwa *working group* ambayo siku zote iko pale kazi yake ni kutazama mkataba unavyo tekelezwa kila siku na kama kuna matatizo kutoa ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na timu hizi, sina mashaka juu ya wataalamu wetu kwa sababu hata waliokuja mbele ya kamati kwa kweli wamejieleza vizuri sana mpaka tukawaelewa. Lakini sasa utakuta watu hao hao ndiyo tunategemea kwenye mambo mengi kwa hiyo wako busy. Sasa kwa wenzetu huko Asia wanachofanya ni kwamba wanakuwa na timu ya wataalamu wabobevu kwenye lile

eneo ambalo ni wastaafu, ambao wanakaa pembeni kazi yao ni kuishauri hii *working group* ambayo iko kazini sasa hivi na kwa wenzetu kule mara nyingi huwa wanafanya bure au kwa lugha zile wanaita *pro bono,* wao kazi yao ni kutazama ule mkataba unavyoendelea kama kuna matatizo wanawashauri ile *working group* halafu inaleta mapendekezo ya marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kila mkataba wa namna hii unayo sehemu ya marekebisho na ambayo inataratibu zake na *timelines*, kwa hiyo ni vizuri kabisa kwamba pamoja na kusaini mkataba mzuri lakini tuwe macho sana katika usimamizi na ninasema hivyo. Kwa sababu, mkataba huu siyo mkataba mdogo tunaweza tukadhani labda tunasaini mkataba na *total* hii ya Ufaransa lakini katika *cooperate world* unaweza ukakuta hii *total* ya Ufaransa wanahisa wake wanatoka dunia nzima na ni makampuni makubwa na nyeti sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kila tunachokifanya dunia nzima inapata taarifa kwamba tumefanya nini? Na kama kuna ambao hawatutakii mema pia wanakuwa wanapata habari kwamba nini kinaendelea. Kwa hiyo, tunahitaji kuwa makini na pia ni jambo la kujivunia kwa sababu ukiangalia kwenye *shareholding* ya Total yako makampuni yanafanya mambo makubwa sana ya mazingira ya kidunia na hata *ku-sponsor* vitu vikubwa vikubwa kama mashindano ya Ragbi na kadhalika. Kwa hiyo, nadhani na sisi tunaenda kuwa sehumu ya mchakato huu mzuri yaani sehemu ya taasisi hizi ambazo zinafaida kubwa sana kwa dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama nilivyosema mkataba huu ulishasainiwa na pia niipongeze Bunge lako kwa sababu lilisha- *ratify* ule mkataba na sisi kazi yetu ni kusaidia tu ili malengo yake yaweze kukamilika na jambo ambalo linafanyika dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninashukuru sana kupewa nafasi hii ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, atafutiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, ajiandae.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kupata fursa hii ya kuchangia kwenye hoja iliyoletwa mezani na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye Muswada huu wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Namba 3 ya mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miongoni mwa wale *member* ambao waliongozwa na Mheshimiwa Spika kwenda kusaidia Kamati ya Katiba na Sheria kutoa maoni ambayo ndiyo yameletwa hapa mbele yetu leo. Kwa hiyo, tuliujadili kwenye kamati kwa kina sana, tukashauriana na mapendekezo yaliyoletwa mbele yako na maoni ya kamati ndiyo yale ambayo tulikubaliana sote kama wanakamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, kwenye huu Muswada kuna lugha inatumika kila kwenye kifungu kinachofanyiwa marekebisho ambacho kimeongozwa kwenye sheria zote 14 ambazo zimeombwa kufanyiwa marekebisho kwenye Muswada huu, kumefanyiwa marekebisho zaidi ya vifungu 30 vinafanyiwa marekebisho na kila kwenye kifungu chenye marekebisho kuna lugha imetumika. Hiyo lugha inasema Mkataba unamasharti kama itatokea mkataba una masharti maalum ya utekelezaji wa kifungu hiki na masharti hayo ikiwa yamekubaliwa na Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila kwenye kifungu kilichoombwa kufanyiwa marekebisho kwenye Muswada huu kimewekwa masharti yenye maneno haya; ikiwa kutakuwa na mkataba na mkataba una masharti maalum ya utekelezaji wa kifungu hiki, hicho kifungu kinachoombwa kufanyiwa marekebisho na masharti hayo ikiwa yamekubaliwa na Baraza la Mawaziri. Sasa hapa ndipo ninapotaka kushauri; maana yake tunaweka kwenye Muswada huu ambao baada ya kupita Muswada huu

itakuwa sheria *mandate* kwa Baraza la Mawaziri ili lipate kufanya maamuzi yanayogusa kwenye Mamlaka zingine zote ambazo zimeombwa kufanyiwa marekebisho 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wito wangu ni kwamba sheria hii haita-*apply* kwa mikataba yoyote ile ambayo maamuzi yake hayatakubaliwa na Baraza la Mawaziri hicho ndiyo kitu ambacho nataka nikiseme mbele ya Bunge hili, maamuzi yoyote yale ya mikataba yoyote ambayo itafanywa sehemu yoyote na mamlaka yoyote ya Serikali aidha Kuu au Serikali za Mitaa hayatafanyakazi ingawa kwenye mikataba yao hiyo watakubaliana huko kuweka masharti ambayo yataendana na vifungu vilivyofanyiwa marekebisho, mikataba hiyo haitafanya kazi ikiwa mikataba hiyo haikupata maamuzi na baraka za Baraza la Mawaziri, hicho ndicho ambacho nilitaka kukisema mbele ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, watu baada ya sheria hii kuanza kufanyakazi wasije wakajitoa ufahamu huko akaenda akafanya mkataba kwa mfano ambao utaathiri Sheria ya Mazingira kwa mfano kwa hiki kifungu cha (6) kilichoombwa kufanyiwa marekebisho, halafu akadhani mkataba huo utafanyakazi kwa masharti ya mabadiliko ya kifungu, lakini kama mkataba huo haukupitishwa na kupata baraka za Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ndiyo *alert* ambayo mimi nilitaka kuisema na ndiyo mchango wangu *all in all* Muswada huu ni mzuri na ukishakuwa sheria utatusaidia kwenye mradi wa mkakati huu ambao kwa asilimia 90 utatunufaisha sisi Tanzania kwenye kuendelea kukuza uchumi wa nchi yetu hii inayoendelea sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo yalikuwa maoni yangu na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia katika Muswada huu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kuipongeza Serikali yetu ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa *Project* hizi kubwa ya kimkakati ambazo zitasaidia sana katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu umekwisha sainiwa na Muswada huu ni moja tu ya takwa la mkataba huu ili kufanya sheria zetu ziendane na utekelezaji wa mkataba huu. Ni vyema pia watanzania wakifahamu kwamba katika *Project* hii ya Bomba la Mafuta, mafuta haya si ya kwetu Tanzania, sisi tunachotoa kama watanzania tunatoa *light of passage* maana yake tunatoa ardhi yetu ili bomba hili litoke Uganda kuja mpaka Tanga kwa ajili ya usafirishaji kwenda katika pande zote za dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafaida nyingi sana ambazo sisi vijana wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tutafaidika nazo ukiachana na kwamba rasilimali hii si ya kwetu. Kwanza kabisa tutapata ajira nyingi sana inakadiriwa ajira 6000 mpaka ajira 10,000 zitazalishwa katika bomba hili, lakini ifahamike wazi kwamba asilimia 80 ya bomba hili zipo Tanzania, maana yake ni kwamba hata zaidi ya asilimia 80 ya ajira hizi *possibly* tukisimama vizuri Serikali maana yake ajira hizi zitatoka kwa watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu katika mkataba huu basi Serikali yetu ihakikishe inasimamia sana sana *regulation* zetu za *Local Content* ili kuhakikisha watanzania ndiyo wafaidika wa kwanza wa ajira zote hizi. Fursa nyingi sana tutapata katika mkataba huu, tutapata nafasi za usafirishaji na kusafirisha watu na mizigo, ajira katika huduma za ulinzi, ajira katika kuzalisha na kuuza mazao ya vyakula na mifugo, huduma za kupika vyakula na kutoa vinywaji baridi, kuna huduma za malazi ya *hotel* na kuhifadhi wageni, kuna vifaa vya matumizi ya ofisini, kuna huduma za kuuza mafuta

ya *petrol* na *diesel* na nyingi nyingi hizi zote ni ajira ambazo vijana wa watanzania tutafaidika nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali katika mkataba huu niwaombe sana Serikali ili sisi vijana wa Tanzania tuweze kufaidika na fursa zote zitakazopatikana katika mradi huu, usimamizi madhubuti unatakiwa, maana yake Serikali ifanye juhudi ya makusudi ya kusimamia ikiwa ni pamoja na kuweka maelekezo kwamba watanzania wawe wanufaika wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu kuna marekebisho mengi sana ya Sheria ambayo yanatoa mwanya, kwa sababu Mkataba huu ni wa Kimataifa kwetu sisi watanzania kuweka *equal grounds* za *bargaining* za ajira kwetu sisi na watu wa Kimataifa. Lakini Serikali yetu ikisimama kidete maana yake watanzania kwa sababu bomba hili zaidi ya asilimia 80 ziko Tanzania maana yake tutakuwa wafaidika au wanufaika wakuu wa ajira zote zinazopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niiombe Serikali sisi, vijana wa Tanzania hatukuwepo wakati miradi kama *TAZARA* au *TAZAMA* inafanyika, maana yake ni kwamba hatuna *experience* ya kutosha ya miradi mikubwa yenye *nature* kama hii. Niiombe Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha inatumia mradi huu kuwa kama *ground* ya vijana kujifunza ili sisi tunapokuwa tunaendelea kama nchi kupata miradi mikubwa kama hii basi watanzania tusiwe nyuma tuwe tumekwisha jifunza tumepata uzoefu wa kutosha namna ya kusimamia namna ya kutekeleza miradi hii, ili tuendelee kutekeleza miradi yetu sisi wenyewe watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika suala zima la *CSR, CSR* si katika kujenga tu majengo ni pamoja na *technology* au *knowledge* ambayo watu hawa au kampuni hii inaweza ikatuachia vijana watanzania tukaendelea kurithishana vizazi na vizazi ili miradi hii ya kimkakati inapoendelea kufanyika basi tunaendelea kuisimamia kama wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata fursa ya kuchangia Muswada huu, na ni niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuchangia kwamba Muswada huu ni Muswada muhimu sana kwa Maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iingie kwenye kumbukumbu zako za Bunge kwamba Bunge lako limepitisha Miswada mingi sana muhimu kuwa Sheria ambayo imechangia sana ukuaji wa Uchumi wa Taifa letu. Lakini Muswada huu wa leo, Muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali namba tatu wa mwaka 2021 ni Muswada wa kipekee sana, kwa sababu unaenda ku-*trigger* kwa namna ya pekee sana ukuaji wa Uchumi wa Taifa letu, Muswada huu unaenda kufungua milango kwa uwekezaji mkubwa sana ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limetajwa hapa Bomba la Mafuta huu ni moja tu, katika miradi mikubwa ambayo itakuwa *accommodated* na mabadiliko au na maboresho ya sheria hii. Mheshimiwa Rais akiwa Mwanza aliongelea mradi wa Liganga na Mchuchuma ambao unaenda kuzalisha chuma ya kutosha kwa Maendeleo ya Taifa letu, marekebisho ya sheria hii yana- *accommodate* miradi ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini juzi tu Mheshimiwa Rais ameongelea uwezekano na utayari wa Tanzania kukaa chini na wawekezaji kuona namna gani miradi ambayo ilisimama ianze, ikiwemo na mradi mkubwa wa bilioni 10 dola, dola bilioni 10 wa Bagamoyo, aina hii ya Miswaada inaenda ku-*accommodate* aina hiyo ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema utangulizi huo nitumie fursa hii kumpongeza sana sana Mhehimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia kuleta mabadiliko haya ya Sheria ili kuruhusu uwekezaji mkubwa na wenye maslahi makubwa kwa Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iingie kwenye *record* za siku 100 za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan za utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi haya mabadiliko ya kiuchumi yatakayotokana na mabadiliko ya sheria zilizopendekezwa yatakuwa ni ya kujivunia kwa kizazi hiki na kwa kizazi kijacho cha watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo ya utangulizi nirudi kwenye muktadha wa sheria hii. Muktadha wa sheria hii wa mapendekezo haya unahusu miradi siyo mradi, inahusu miradi ambayo mikataba yake itakuwa na masharti maalum na itaridhiwa na Mabaraza la Mawaziri. Kwa hiyo, siyo mikataba bora mikataba ni mikataba yenye masharti maalum. Na nini kinapendekezwa na Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapendekeza kwamba miradi hii ambayo ina masharti maalum ambayo pia itakuwa imeridhiwa na Baraza la Mawaziri vifungu vilivyotajwa hapa kwenye Sheria 14 visihusike utekelezaji wake, utekelezaji wa vifungu hivi vilivyotajwa hapa kwenye hizi sheria 14 utekelezaji wake usiathiri utekelezaji wa miradi au mikataba hii mikubwa iliyotajwa na hiyo ndiyo mantiki na hiyo ndiyo adhma ya mapendekezo haya ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa miradi ya aina hii likiwemo pamoja na Bomba la Mafuta kutoka Hoima, naunga mkono kwa asilimia 100 mapendekezo yote yaliyoletwa na Serikali pamoja na marekebisho ya Kamati. Kwa vile muda unaniruhusu nataka nitaje maeneo matatu ambayo nadhani yanaweza kuchangia kuongeza uelewa wa Bunge lako Tukufu na Wabunge kuweza kupitisha sheria hii bila kuyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya mapendekezo ya Sheria zinazopendekezwa inahusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Sheria hii ya Mazingira ilikuwa inazuia kufanyika shughuli zozote za kibinadamu ndani ya mita 60 ambako kuna vyanzo vya maji, mito, mabwawa na kadhalika. Sheria hii kama ingebaki hivi kwa miradi mikubwa, ikiwemo kama hii ya Bomba la Mafuta ingetukwamisha. Kwa hiyo, mabadiliko na mapendekezo haya ni muhimu sana ili kufanikisha mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hii Sehemu ya Sita, Sheria ya Bima, Sura ya 394. Pamoja na kifungu cha 133 kutaka mkazi yeyote wa Tanzania au makampuni yote ya Tanzania yanapotaka kupata huduma ya bima lazima yapate bima kwa kupitia makampuni ya Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii ilikuwa inatukwamisha kwa sababu mradi huu pamoja na miradi ya aina hii ina masharti makubwa na ina gharama kubwa za bima, makampuni yetu ya ndani yanaweza yakakosa uwezo huo. Sheria hii inaruhusu kwa makampuni ambayo yatakuwa na sifa na masharti yaliyoelezwa hapa, tuweze kutumia hata bima za makampuni ambayo sio ya Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maslahi ya muda, nakushukuru sana na naunga mkono hoja na naomba Watanzania na Wabunge wote tuunge mkono hoja hii ya Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete, ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2021].*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, *after 100 days* tangu Mheshimiwa Rais aingie madarakani, *these was one of the strategic projects* (hizi zilikuwa miongoni mwa miradi ya kimkakati) ambayo ilikuwepo na ameonyesha nia ya kuendelea kwenye yale ambayo yana faida kwenye nchi. Kwa kweli kwenye hili nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika ile hali ya kupenda nchi yetu kwenye jambo kama hili ambalo lina maslahi mapana ya Taifa kwa sababu, marekebisho ya sheria hizi yanatusaidia kwenda ku-*facilitate* (kuwezesha) uwepo wa mradi huu ambao ni mradi *actually* Wakenya wenzetu waliukosa kwa sababu kadhaa lakini sisi tumeupata. Kwa hiyo, ni kitu ambacho kwa kweli ni kikubwa kwa maana ya faida kwenye nchi kwa sababu tunaenda kuongeza pato la Taifa lakini pia, faida kwa vijana wa Tanzania ambapo kimsingi kuna ajira ambazo zinatarajiwa si chini ya 10,000 kwa Watanzania. Kwa kweli hili ni jambo kubwa sana. Pia, katika masuala ya diplomasia na ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na wenzetu Waganda, hili ni suala ambalo linaendelea kuimarisha ushirikiano wetu na wenzetu Waganda na Afrika Mashariki kwa ujumla pamoja na kwamba tumewawahi Wakenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunajua kuna faida kubwa kwenye mradi huu na tunaipenda nchi hii na tunatamani tufanikiwe, kuna mambo ambayo kimsingi ni lazima tuyashauri Serikalini. Marekebisho ya sheria 14 kwa ajili ya ku-*accommodate* Bomba la Mafuta, kuna tatizo moja ambalo naliona. Kwanza niseme kwamba mimi pia ni miongoni mwa walioteuliwa kwa ajili ya kuungana na timu ya Katiba na Sheria kwa ajili ya kushughulikia marekebisho haya na wenzangu wameshazungumza baadhi ya vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwajibikaji kisheria naliona linawekewa utaratibu kidogo ambao utatupa shida kwa sababu tunajua pia kuna masuala ya utawala bora lakini pia na uwajibikaji Kitaifa. Katika vifungu vilivyofanyiwa marekebisho kuna maneno yamerudiwa kutajwa mara

kadhaa na ambayo yanalipa sifa Baraza la Mawaziri na kuondoa *mandate* ya Bunge hili kuwa kwenye utaratibu mzuri. Tunafanya marekebisho ya sheria lakini bado kuna kifungu ambacho Bunge hili leo tukipitisha kama kilivyo, kinaenda kutoa madaraka makubwa kwa Baraza la Mawaziri na nina wasiwasi nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipengele ambacho *kina-support* kinasema: *"Where there is an agreement that provides for special arrangement relating to implementation of this provision, and the said agreement has been approved by the Cabinet, the application of the provision of this section, shall not prejudice the implementation of such agreement"*. Kwa maana kwamba kama kuna makubaliano yatahitaji utaratibu maalum kuhusiana na utekelezaji wa masharti ya sheria husika na kama utaratibu huo umepata kibali cha Baraza la Mawaziri basi masharti ya sheria husika hayatazuia au kuathiri utekelezaji wa makubaliano hayo. Kifungu hiki kinakwenda kutoa mwanya kwa Baraza la Mawaziri wakati mwingine kufanya vitu, kwa sababu hawa ni watu na tukitoa *mandate* kubwa kwenye jambo kama hili, inawezekana wakaingia makubaliano yasiyo na tija kwa wawekezaji ambao watakwenda kufanya uwekezaji kwenye ujenzi na ile *restructuring* ya Bomba zima la Mafuta. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hicho ulichosoma ni kufungu namba ngapi?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kurekebisha zile sheria 14 wametumia mara kadhaa maneno hayo, nimeya-*quote.* Ukisoma kwenye marekebisho utaona wameyatumia mara kadhaa na Mheshimiwa Ramadhan ambaye tupo kwenye Kamati moja pia ameyazungumzia. *Aim* ni kujenga wala hatuna nia mbaya kwa sababu hili ni jambo jema kwa kweli na mimi niseme naliunga mkono na naamini Wabunge wengi wanaunga mkono kwa sababu tunajua faida yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema athari yake ni kwamba inawezekana Baraza la Mawaziri wakati

wanatekeleza jambo hili wakaingia makubaliano na wawekezaji kwenye mradi huu ambayo yanaweza hayana tija kwenye nchi. Kwa ajili ya kuwasaidia nashauri badala ya kuweka kama ilivyo kwenye kutoa *authority* na *mandate* kwenye Bazara la Mawaziri, isomeke kwamba: "Makubalino yoyote yenye kuhitaji utaratibu maalum wa utekelezaji na ambayo yana kibali cha Bazara la Mawaziri hayatakuwa na sifa ya kuandaliwa utaratibu maalum wa utekelezaji, isipokuwa yatapitishwa na Bunge kupitia Kamati ya Bunge ya sekta husika kuwa yanahitaji kuandaliwa utaratibu maalum wa utekeelzaji". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nime-*propose* hivi kwa sababu Kamati za Bunge hili ni Kamati zinazoheshimiwa sana na Bunge hili na sisi tuna imani na Kamati hizo ndio maana wanakuja kusoma taarifa za Kamati. Kwa kweli mimi mwenyewe nilikuwepo kwenye Kamati na pia nakubalina na mapendekezo ya Kamati. Tukiweka hivi itatusaidia pia Bunge ku-*oversight* na ku-*oversee* kwenye masuala mbalimbali, pamoja na kwamba yatapitiwa kwenye Baraza la Mawaziri na Baraza la Mawaziri lita-*authorize,* lakini Kamati mahsusi za kisekta zitakuwa na mkono wake kwenye jambo hili. Wakati mtoa hoja anakuja kuhitimisha nashauri sana aangalie jambo hili upya na kwa ubora na kwa umakini zaidi. Tuone namna gani tunaweza kusaidia nchi yetu kwa sababu tumezungumza kwamba baadaye inaweza kutokea changamoto lakini kwa sasa hivi nashauri iwe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeshauri na mimi naendelea kushauri, wenzetu Waganda tayari wameshaanza maandalizi ya kutunga sheria mahsusi kwa ajili ya ku-*facilitate* Bomba hili. Sisi tunafanya marekebisho kwenye zile sheria 14 ambazo zinahusiana na Bomba hili lakini *in the future* tukiwa na sheria mahsusi ambapo Bunge tutajadili kwa upana wake kama ambavyo Waganda wenzetu wanatunga sheria mpya kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Bomba hili itakuwa vizuri sana. Nashauri pia Bunge letu Tukufu tutunge sheria hii mahususi, kwa ajili ya Bomba hili ambayo itatusaidia kuweka mambo mengi kwa upana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Miswada hii ya Marekebisho ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa sheria yoyote ile inayotungwa ni hasa pale inapokuwa na nia au dhamira njema. Kwa hiyo, marekebisho ya sheria hii naamini yana nia njema na yanalenga katika kuwezesha utekelezaji bora wa miradi mikubwa ya kimkakati na hivyo kuwezesha kutoa hali ya kuaminika baina ya nchi na nchi au wadau wanaoingia katika mikataba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika mradi huu unaotajwa wa Bomba la Mafuta, kimsingi una faida nyingi sana za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Kwa misingi hiyo, mradi huu ambao umeanza kujadiliwa toka mwaka 2016 kwa kumbukumbu zangu, kwa kweli sasa unastahili uwezeshwe ili uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa jitihada kubwa anayoifanya katika kuona kwamba taifa hili linaendelea kusonga mbele. Niseme tu kwamba binafsi kama ilivyo kawaida yangu napoziona sheria kama hizi zikija hasa zinapogusa maslahi mapana ya nchi yetu, nimekuwa nikiwa na jitihada sana za kutafuta huko na huko japo sio mwanasheria, hiki maana yake nini au hiki hakina athari? Niseme tu kwamba nimejiridhisha na dhamira njema iliyopo katika mabadiliko haya ya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi kama ambavyo wenzangu wamesema, hivi vifungu vilivyojirudia mara kwa mara kwamba mikataba hii ya kimkakati

itakapokuwa imeingiwa au kupitishwa na Baraza la Mawaziri, nikajiuliza Baraza la Mawaziri ni nani, nikakuta pale kuna Mawaziri lakini Mwenyekiti wake ni Rais wetu, Makamu wake na yeye pia ni kiongozi msaidizi katika Baraza hili. Kwa hiyo, nikajiridhisha kwamba kama Rais mwenyewe ndiye Mwenyekiti wa chombo hiki na huyu Rais pia ni sehemu ya Bunge lakini pia Katiba inatoa mamlaka kwa Bunge kwamba Rais akiwa ameenda tofauti, lakini hatua hiyo hatuitamani sana, kuweza kupiga hata kura ya kutokuwa na Imani, si ndiyo jamani, sasa nani ambaye anaweza kuwa ameshikilia majukumu haya mazito zaidi ya Mheshimiwa Rais? Kwa hiyo, mimi nimeona kwamba tuko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama ilivyo ni kwamba Rais ni taasisi na Baraza la Mawaziri halianzii hapo lina watendaji wake wanaoanzia toka huko kwenye sekta mpaka jambo linaweza kufika sasa kwenye Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, niombe wale wadau ambao wanahusika katika kuchakata mikataba hii wawe makini lakini wajitahidi kuwa na uzalendo kwa nchi yao. Wakishakuwa na uzalendo ina maana watachakata mikataba hiyo kwa uhalisia na tutahakikisha kwamba tunaingia kwenye mkataba ukiwa salama na nchi yetu inatendelea kwenda mbele vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu mkataba ni kitu kimoja na hii mikataba kwa sasa kama tulivyoipa mamlaka ina nguvu sana, sasa kama itakuwa haijachukua maslahi mapana ya wananchi, tumeshuhudia kuna nchi nyingi ambazo watu wananung'unika baadaye wanajikuta wameingia barabarani. Kwa misingi hiyo na kwa sababu marekebisho haya hayahusu huu mkataba mmoja tu ambao ni Bomba la Mafuta na mingine ambayo tutaingia, niombe sana Serikali kujipanga zaidi, kuwa na wataalamu ambao wamebobea katika maeneo hayo, tusomeshe watu wetu katika maeneo mbalimbali ili tuwe na watu ambao wanaweza kutoa ushauri mzuri zaidi. Ukiacha tu wale wanaoingia kwa nafasi zao za ki-cheo, tuweze kuwa na wataalamu wabobezi wazuri katika maeneo yetu. Naamini tukifanya hivyo nchi yetu itazidi kusonga mbele na tutakuwa tumenufaika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niseme tu kwamba kama ambavyo Mwenyekiti wetu wa Kamati ametoa maoni kuna umuhimu wa kuwa na sheria maalum kwa ajili ya hili Bomba la Mafuta. Hii ni kutokana na kwamba baadhi ya rasilimali tunazozizungumzia zinatofautiana sana kiasi kwamba hata sheria moja haiwezi kukidhi, pengine ipo haja ya kulipatia hili Bomba la Mafuta sheria yake maalumu ili iwe rahisi katika ufuatiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba mimi binafsi naunga mkono hoja, nikitegemea kwamba na mambo mengine yatakayoendelea katika mikataba mbalimbali yatakuwa yanaangalia maslahi mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, Mheshimiwa Prof. Adelardus Kilangi (mtoa hoja) ajiandae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja zote mbili; iliyotolewa na Kamati lakini pia ile iliyotolewa na Serikali kwa sababu ukizisoma unaona zote zinakwenda katika uelekeo mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, natambua kwamba sheria iliyoletwa mbele yako mbele ya Bunge hili, ni mwendelezo au ni hatua katika utekelezaji wa makubaliano yaliyosainiwa kimkataba baina ya nchi zetu mbili na washirika wengine tarehe 26 Mei, 2017 na kufuatiwa na mkataba mwingine au sehemu ya *Addendum* hizo iliyosainiwa tarehe 20 Mei, 2021 kule nchini Uganda na baadaye mkataba uliosainiwa Dar es Salaam na Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni na Mama yetu Samia Suluhu Hassan pale Ikulu Dar es Salaam mapema wiki tatu zilizopita. Mimi naanza kwa kuunga mkono hoja lakini kuunga mkono hoja inaweza ikawa

ni neno la Kiswahili kizuri lakini kwa lugha ya kisomi au lugha ya Kibunge nadhani ni vyema nikatumia nafasi hii kueleza ni kwa nini naunga mkono hoja hii. Yapo mambo ya msingi yaliyonisukuma kusimama mbele ya Bunge lako sio tu kuunga mkono lakini pia kuwashawishi Wabunge wenzangu tukubali kwa pamoja kuunga mkono hoja zilizowekwa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, ukisoma vizuri sheria iliyoletwa, kwanza ni sheria ambayo inakwenda kutafsiri makubaliano hayo. Kwa hiyo, kama tutafanya utaratibu wowote ule, Wabunge wenzangu naomba niwakumbushe kwamba vipengele vya kisheria vilivyowekwa ni vinakwenda kutafsiri makubaliano hayo. Hakuna kitu kipya ambacho sisi kama Wabunge tunaweza tukasema kwamba hiki labda kuna mtu amekichomeka au amekitohoa katika maeneo yake bila kuangalia masharti ya kimkataba. Hili la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni ukweli kwamba sheria hii inakwenda kuangalia jinsi gani mkataba huu unakwenda kuwa *implemented* au kuhakikishiwa utekelezaji wake bila ya kuwa na kigugumizi chochote. Kwa mfano, katika sheria zetu za halmashauri ambazo zimeelezwa katika mchango uliotolewa na Kamati lakini pia na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa *Attorney General*, sheria zetu za sasa ukizingalia kama zilivyo na ukaamua kuzisimamia maana yake utakwenda kupata shida mbele katika utekelezaji. Mapendekezo yaliyoletwa yanaondoa kigugumizi hicho na kutoa nafasi kwa Baraza la Mawaziri, ikiwa linasimama kwa niaba ya Serikali yake, ikiwa linasimama kwa niaba yetu sisi kufanya maamuzi yaliyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwakumbushe kwamba hili si jambo linalofanyika kwa mara ya kwanza. Kama mnakumbuka vizuri tulikuwa na mikataba ya madini na kama mnavyofahamu nchi yetu ina maeneo mbalimbali yanayotoa madini. Wenzetu wa Geita kule wanazo sehemu wanazochimba madini, wenzetu wa Kahama kwa maana Shinyanga wanazo sehemu wanazochimba madini, wenzetu

wa Mara kwa maana ya *North Mara* wanazo sehemu wanazochimba madini, kama Serikali hii isingefanya kama ambavyo inataka kufanya katika mkataba huu ikaziachia halmashauri husika au mikoa husika itunge sheria ili kuangalia jinsi gani mirabaha inapatikana katika maeneo yao, huenda mikataba ile isingefanyika kama ambavyo imefanyika sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Serikali zetu zilizopita zimefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba sheria zinasimamiwa na mirabaha ya wananchi inapatikana. Hili ndilo ambalo linaenda kufanyika katika upande huu wa kusimamia halmashauri zetu ili mambo yakae vizuri na halmashauri ziendee kupata kipato kinachotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni upande wa usimamizi wa rasilimali. Katika upande wa usimamizi wa rasilimali imeelezwa katika sheria ilivyo; kilichofanyika katika mapendekezo ya sheria hizi zinazotajwa ni kuhakikisha kwamba sasa katika maeneo ambayo bomba hili linapita, Serikali inakwenda kuangalia kwa niaba yetu jinsi gani rasilimali zetu zinaenda kusimamiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kipengele cha sheria siyo kwamba kinakwenda kubadilisha hayo ambayo yamesemwa isipokuwa kinatoa nafasi kwetu kuendelea kuona Serikali yetu ni kwa jinsi gani inaweza kusimamia mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Wabunge wenzangu na wananchi wenzangu wa Tanzania, tuiamini Serikali yetu chini ya Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais kwamba itakwenda kutufanyia haki na Baraza letu la Mawaziri litakwenda kusimamia yale ambayo yamekusudiwa kimkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo pia lipo jambo ambalo lilijadiliwa sana kwenye Kamati. Hili jambo kwa namna moja au nyingine baadhi ya Wabunge wamekuwa wakituuliza ni jinsi gani sheria hii au mkataba huu unakwenda

kusimamia mali za Serikali yetu bila ya kuathiri mambo ya kimkataba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwatoeni wasiwasi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba katika sheria ya mashauri ya Serikali inazungumza wazi kwamba yapo mambo ambayo huwezi kuyafanya bila sheria kuwa imekuruhusu kuyafanya. Mojawapo ni ukamataji wa mali za Serikali. Ila katika mkataba huu kinachozungumzwa, siyo mali zinazomilikiwa na Serikali ya Tanzani, ni zile mali ambazo zitaingizwa katika kile chombo au lile shirika linaloanzishwa ambalo kwa mujibu wa mkataba huu ni lile Shirika la *EACOP* ambalo linakwenda kusimamia mradi mzima wa mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishieni Watanzania wenzangu na Wabunge wenzangu kwamba tukubali kupitisha mkataba huu au sheria hii ili kuhakikisha sasa Serikali yetu au Serikali wanachama katika jambo hili la mafuta ya bomba linalotoka Hoima kwenda mpaka Chongoleani kule Tanga linakwenda kusimamiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa umuhimu wake, naomba sana Wabunge wenzangu na Wajumbe wenzangu waamini kwamba sheria hizi kama zilivyowekwa zinakwenda kuwahakikishia Watanzania mustakabali mzuri kama ambavyo wenzangu waliotangulia wamesema hasa katika eneo la ajira na ustawi mzuri wa maisha na maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani, atafuatiwa na mtoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kama ilivyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Napenda

kwa hatua ya awali kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan katika kuamua kutekeleza mradi huu tena kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka mradi umeanza takribani miaka mitatu iliyopita, lakini toka ameingia madarakani Mheshimiwa Rais, kazi kubwa pamoja na mambo mengine anayofanya ni kuusukuma na kuuwezesha utekelezaji wa mradi huu kwa kasi kubwa. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hoja zimeulizwa na Waheshimiwa Wabunge nami napenda nichangie, nitoe ufafanuzi walau kidogo kwa sababu ya muda. Katika kutekeleza mradi huu, jambo la kwanza ambalo litarahisisha sana usimamizi wa mradi huu ni kupitisha Muswada huu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao kimsingi ukishapitishwa unarahisisha sana usimamizi wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi mahususi kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamechangia, mradi huu kimsingi ni wa kimkakati na usimamizi wake ni lazima uwe wa kimkakati, kwa hiyo, hatua ya kwanza ambayo tumeifanya kwa upande wa Serikali, kwanza sisi Serikali kushiriki.

Mheshimiwa Nainu Spika, nirudie kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa sisi Serikali kuwa wadau na wabia wa mradi huu kwa asilimia 15, jambo ambalo linatupa fursa ya kusimamia kwa ukaribu kama sehemu ya utekelezaji wa mradi na pia tukiwa ndani ya Kampuni ya Usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wameuliza Waheshimiwa Wabunge, tumejipanga vipi katika usimamizi? Jambo la kwanza, tumeunda timu mahsusi; na napenda nitoe taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge kwamba tayari tumeshateua waratibu wa mradi huu ambao ni Watanzania, tena vijana wataalam waliobobea kwenye masuala ya mafuta hapa nchini. Kwa hiyo, tumejipanga vizuri katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, tunahusisha kila taasisi ya Serikali na sekta ambazo ni muhimu katika kusimamia ambazo zina utaalam uliobobea na wa hali ya juu wa ndani na wa Kimataifa kwa ajili ya kuratibu usimamizi wa mradi huu. Kwa hiyo, tuna timu mahususi ambayo imeundwa na imeshaanza kazi chini ya waratibu ambao tuliwatua miezi miwili iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Usimamizi, tumeunda chombo kinaitwa *Government Facilitation Team.* Badala ya kusubiri vibali mahali ambapo watahitaji vibali vya wataalam wakati wa utekelezaji wa mradi, tumeweka mamlaka kwa wenye mamlaka vibali kuteua wataalam waandamizi ili kusaidia katika uratibu wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani, labda kibali kinahitajika kutoa *exemption TRA,* tumemtaka na kumwomba Kamishna wa *TRA* kuteua afisa kama *Desk Officer* ili jambo likifika lisilale wala kuchelewa. Tumefanya hivyo kwenye sekta zote za Serikali. Hii inasaidia sana kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa mradi huu ili tuendane na wakati wa kuukamilisha kwa ajili ya manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kimuundo, nitumie nafasi hii pia kuwaomba, kwa umuhimu wa maradi huu; na huu mradi unapita karibu sehemu kubwa sana ya nchi yetu; asilimia 80 ya mradi huu upo kwetu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, Viongozi na wananchi kwa ujumla, mahali ambapo bomba litapita, sisi tuwe watu wa kwanza kulinda bomba; na ni sehemu ya usimamizi. Kwa hiyo, nawaomba sana katika eneo hilo, pia sisi kwa ujumla wetu tusaidiane kuusimamia mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyofahamu mradi utapita katika maeneo mengi. Kwa ujumla wake usimamizi wa mradi huu kama nilivyosema, kwa sababu unapita eneo kubwa, utawahusisha sana wananchi. Tumetaka sehemu ya kwanza hasa kwenye ulinzi wa bomba lazima zitumike kampuni za ndani ya nchi yetu kwa ajli ya kulinda usalama wa bomba lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wasimamizi, tumepitisha pia utaratibu ambao utapita karibu kila kata ambako mradi unapita. Viongozi wa Kata, viongozi wa Tarafa, Wakuu wa Wilaya na wengine watakuwa ni wasimamizi wa kwanza kuhakikisha vijana wenye uwezo wa kufanya kazi hizo maeneo yale, vijana wa maeneo hayo ndio wanapata ajira kwa fursa ya kwanza. Tumejipanga vizuri kwa upande huo na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutoa maelekezo ya awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *local content*, napenda nitoe taarifa kidogo, tumefanya maboresho. Siku ya nyuma tulikuwa tunawaruhusu Wakandarasi kutoa *tender* au matangazo ya kazi za ndani. Kwa hatua ya kwanza mwaka huu tumefanya marekebisho na Mheshimiwa Rais ametuelekeza vizuri sana, kwanza tumeanzisha kanzidata ambayo inasajili makampuni ya ndani ambayo yatafanya kazi zote za *supply,* ujenzi, kutoa huduma, kwa hiyo, yamesajiliwa *EWURA.*

Kwa hiyo, kila kampuni ya ndani ambayo itatakiwa kufanya kazi hii badala ya kutoa tangazo, Kampuni ya *SINO HYDRO* kwa mfano, ambayo ni ya China labda ndio Mkandarasi wa Kimataifa; akitoa tangazo kwa mfumo wa zamani, watu walikuwa wanaomba na wakajionesha kwao ni akina Masanja, akina Lugekingila, lakini ukiingia ndani, ni Wachina wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichofanya ni kusajili kampuni za ndani. Kwa hiyo, kampuni ikitaka kuajiri kampuni ya ndani tunaiambia lete fursa, tunamkabidhi makampuni ya ndani ambayo yamesajiliwa hapa, anachagua. Kama ni Makampuni mawili, anayachagua kati ya makampuni kumi yote ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatua nzuri sana ambayo itasaidia sana kujihakikishia kwamba makampuni yanayofanya kazi za kutoa huduma za kujenga, zote ni za ndani. Kwa hiyo, kuna kila namna ya kuipongeza Serikali yetu kwa hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitoe wito pia kwa wananchi na Waheshimiwa Wabunge, tutakaporudi katika maeneo yetu, tuwaambie wakandarasi wenye uwezo wale wa ndani waendelee kwenda kujisajili *EWURA* ili waweze kupata fursa ya kufanya kazi hizi wakati wa utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili tulilofanya ni kutoa fursa. Nampongeza sana Mheshimiwa Kamani, Mheshimiwa Mbunge kijana kwa niaba ya vijana; na tunasisitiza kweli asilimia kubwa ya kazi hizi zifanywe na vijana. Hatuna maana kwamba wengine wasifanye, lakini wanayo fursa kubwa sana. Mathalani tumetoa maeneo mengi na sasa tunaanza kutoa semina.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa, tarehe 3 tutakuwa na Semina ya *Tanzania Private Sector Foundation.* Ile taasisi *private* tunakaa nayo itupe mkakati na yenyewe wa namna ya kuchukua fursa hii. Tunafanya mkutano wa kwanza mkubwa ambao utakuwa eneo la Chongoleani kule Tanga tarehe 3 mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba sana vijana, kupitia *Tanzania Private Sector Foundation* na taasisi za vijana, mtumie *vehicle* hizo ili tuone, tuwasajili kwa nafasi mnazoweza kuzifanya, mzifanye wenyewe badala ya kuwapa vijana kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, yapo makampuni ya kigeni ambayo yanaweza kufanya kazi hizi ambazo ni za kitaalam zaidi. Kwa mujibu ya Sheria yetu ya Mafuta, imetoa utaratibu kwamba kampuni za ndani zote ambazo zitafanya kazi katika mradi huu, zitatakiwa kuwashirikisha Watanzania ndani ya makampuni hayo au Makampuni ya Kitanzania ambayo ushiriki wao usipingue asilimia 25 katika makampuni hayo. Huu ni udhibiti ambao utasaidia sana kuratibu Watanzania kupata fursa ya kujenga miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba niongelee kidogo kuhusu manufaa ya mradi huu. Manufaa ya mradi huu ni makubwa sana. Tumeeleza na kila mtu anafahamu kwamba ni takribani kilometa 1,145 zipo Tanzania na tunayo makambi 14 yatakayojengwa kwenye bomba hili. Pia kwenye makambi 14 hayo, makambi takribani 11 yapo Tanzania. Vilevile tutakuwa na vituo; kwa sababu bomba hili ni la kupasha joto, kutakuwa na vituo vya kupasha joto bomba 29 na vituo 22 vyote vipo Tanzania. Pia kuna mahali tu pa kufungulia *valve* ambavyo vipo vituo 76 vya kufungua *valve*. Vituo 53 vipo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna vituo sita vingine vya kusukuma na kupunguza mgandamizo na *speed* ya mafuta, vinne vipo Tanzania. Kutajengwa matenki takribani matano makubwa kule Chongoleani. Nafasi hizi zote ni fursa kwa Watanzania.

Mheshimwia Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwaomba sana Watanzania wachangamkie fursa. Ni zaidi ya asilimia 80 ya ajira zinatoka Tanzania. Tunatarajia vijana wetu na wafanyakazi wapatao 15,000 wakati wa ujenzi wa mradi huu wataajiriwa.

Kwa hiyo, nitoe wito kwa Watanzania wenye uwezo kwenda kuchangamkia fursa hizi; iwe mama ntilie, kampuni za ulinzi, iwe kampuni za ku-*supply,* vyote vitafanywa na Watanzania. Ila msisitizo mkubwa tunauweka zaidi kwamba vifaa vyote vya ujenzi wa bomba, iwe *cement,* iwe nondo au misumari, ni lazima vitokane na viwanda vyetu vya ndani. Huo ndiyo msisitizo tunaousisitiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono sana hoja hii, tena ikipita leo, haraka sana kwa sababu utekelezaji wa mradi umeshaanza ili iturahisishie kwenda kutekeleza mradi huu kwa kasi zaidi. Nimalizie kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, toka tulipoanza, hata Bunge lililopita kupitisha masuala yote yanayohusu utekelezaji wa bomba hili ili bomba hili likatekelezwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimwia Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimwite mtoa hoja, Mheshimiwa Profesa Adelardus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Act, 2021.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa michango yao mbalimbali na kwa kweli kwa kiasi kikubwa imeonesha kwamba wanaunga mkono na wanaelewa umuhimu wa marekebisho ambayo Serikali imeyaleta na kuyapendekeza. Pia wametoa maoni mbalimbali kadhaa ya kuboresha hapa na pale na nitaomba kwa haraka haraka kabisa nipitie maoni mbalimbali yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na panapohitaji kutoa maeleza au ufafanuzi kidogo, basi nitumie fursa hii kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemsikia Mheshimiwa Tadayo amezungumza juu ya umuhimu wa kuwepo kwa timu ya wataalam ya kusimamia mikataba kama hii. Mheshimiwa Waziri wa Nishati ameeleza vizuri lakini niongezee tu kwa kusema kwamba zitakuwepo timu mbili ambazo zitakuwa zinafanya kazi na Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza itakuwa ni timu ya wataalam ambayo kazi yake itakuwa ni kuangalia masharti mbalimbali ya Mkataba huu siku hadi siku na kuona kama kuna wajibu wowote kwa upande wa Serikali au nchi yetu ambao tunatakiwa kuutekeleza na utekelezwe ipasavyo na kwa wakati. Hiyo ni timu ya kwanza; na ya pili itakuwepo

timu ya washauri na litakuwa ni jopo la watu kadhaa ambao watampatia ushauri Mheshimiwa Waziri wa Nishati pale ambapo ataona anahitaji ushauri katika utekelezaji wa mradi huo. Kwa hiyo, jambo hilo limeshafanyiwa kazi tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kutoka kwa Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, ameeleza vizuri kwamba marekebisho haya yanahusu mikataba ambayo Baraza la Mawaziri limeidhinisha. Kwa hiyo, Serikali imeidhinisha na kwamba marekebisho haya yatagusa miradi yote ya kimkakati na siyo tu suala la huu mradi wa bomba la mafuta, lakini pia akaeleza vizuri kabisa kwamba nia kuu hapa ni kuweza kuoanisha sheria zetu na wajibu zilizoko katika mikataba mbalimbali ambayo pia kwa namna moja au nyingine tumeisaini au tumeiridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ng'wasi Kamani amezungumzia pia suala lile lile la lengo la Muswada la kuoanisha sheria na wajibu katika mikataba mbalimbali. Kuhusu masuala ya fursa Mheshimiwa Waziri wa Nishati amelieleza vizuri kabisa na nisingependa kuongezea zaidi hapo kwa sababu maelezo yake yanajitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mhagama ameeleza naye pia kwamba Muswada huu kwa kadri anavyoelewa hauhusu bomba la mafuta peke yake, bali inagusa na miradi mingine kama hiyo na huo ndiyo ukweli na ametoa mifano kadhaa hapo katika kujenga hoja yake na tunamshukuru sana kwa kutusaidia kuongeza ufafanuzi katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, kiujumla anaunga mkono marekebisho haya kwa sababu anafikiri yanaangalia maslahi mapana ya nchi. Hata hivyo ameonesha wasiwasi wake katika eneo la uwajibikaji kisheria na amekuwa na wasiwasi mkubwa sana kwamba marekebisho hayo pengine yataishia kulipa Baraza la Mawaziri mamlaka makubwa sana na kulinyima Bunge mamlaka yake kadri ya mujibu wa Katiba pamoja na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo hili, itanibidi kueleza kidogo kwa sababu wasiwasi huu ni mkubwa siyo mdogo. Nilitaka kuanza kueleza kwa kurejea Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba imelipatia Bunge mamlaka yake kuhusiana na mikataba kama hii. Ukisoma Ibara ya 63(3)(e) inaeleza waziwazi mamlaka ya Bunge na inasema, nitaisoma: "Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake, Bunge laweza (a) Kujaddili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa."

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine ni vema tukasoma pia nakala ya Kiingereza tuone nayo inatuelezaje kama hapo tutakuwa hatujaelewa vizuri. Nakala ya Kiingereza inasema: "*for the purposes of performing its functions the National Assembly may (e) deliberate upon and ratify all treaties and agreements to which the United Republic is a party and the provisions of which require ratification."*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ibara hii ya Katiba iko wazi kabisa na inajieleza, hii inahusu mikataba ya Kimataifa na katika nakala ya Kiingereza imezungumzia ku-*ratify* yaani kuridhia, lakini hili litatumika tu pale ambapo pia masharti ya mikataba ile yanataka uridhiwe na uubadilishe mkataba ule uwe sheria kwa kiingereza inasema: "*incorporation of the provisions of the treaty into our laws*" yaani kuubadilisha ule mkataba kuwa sheria zetu, ndiyo mara nyingi inafanyika hivyo, japokuwa Bunge linaweza tu likaridhia tu mkataba bila kuwa na haja ya kuibadilisha kuwa sheria yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotaka kusema ni kwamba mamlaka ya Bunge katika sehemu hiyo yapo na yanabaki kama yalivyoelezwa katika Katiba. Kwa taarifa tu, ule mkataba kati ya Tanzania na Uganda kuhusiana na bomba hili la mafuta, *inter-governmental agreement* ililetwa katika Bunge lako Tukufu na Bunge likaweza kufahamishwa juu ya uwepo wa mkataba huo. Kwa sababu masharti yake hayakuwa yanahitaji kuridhia kwa maana ya neno la

*ratification,* basi *ratification* haikufanyika kwa sababu haikuhitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nieleze pia kwamba katika sheria yetu ya *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act,* kifungu cha 12 kimeeleza na nitakisoma kwa sababu kinagusa mamlaka ya Bunge:

"*All arrangements or agreements entailing extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources may be reviewed by the National Assembly*."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie: "*All arrangements or agreements entailing extraction, exploitation or acquisition and use of natural wealth and resources may be reviewed by the National Assembly*."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mipango yote makubaliano yanayohusu kuchimba, kutumia hizi mali asilia yanaweza kurejelewa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo ni vema tukaeleza hapa na hili ni mojawapo ya mambo ambayo tumeyaleta kwenye mabadiliko. Sheria yetu hii ilikuwa haitofautishi kati ya maliasili zetu zinazochimbwa au zinazotokea Tanzania na zile ambazo zinatokea katika nchi nyingine na hapa kwetu zinapitishwa peke yake. Kwa hiyo nilichotaka kusema hapa ni kwamba japokuwa kifungu hiki cha sheria kipo lakini hakiwezi kikatumika sasa kwenye huu mradi tunaouzungumzia, kwa sababu mradi huu unahusu rasilimali ambazo zinatokea kwenye nchi nyingine, siyo za kwetu na hatuwezi tukatengenezea sheria kuzisimamia rasilimali za nchi nyingine. Sisi hapa kama alivyoeleza vizuri Mheshimiwa Kamani tunatoa tu njia ya kuzipitisha rasilimali hizo, lakini kwa ujumla mamlaka ya Bunge hayajaguswa, ndiyo hoja ya msingi niliyotaka kuizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Stella Manyanya pia ametoa mchango na kuunga mapendekezo

ya Serikali, namshukuru sana. Namshukuru sana pia Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, amefafanua kwa kina zaidi kwamba sheria hii au mabadiliko haya yana lengo la kutoa tafsiri na kuwezesha yale masharti ya kimkataba ambayo tumeshaingia. Mapendekezo haya ni kwa ajili ya nia ya kuondoa changamoto ya utekelezaji wa mikataba hiyo.

Pia namshukuru sana kwa ufafanuzi wake mahiri alioutoa kwenye eneo la ukamataji wa mali za Serikali kwamba, itahusu tu zile mali ambazo zinahusiana moja kwa moja na mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi naomba nihitimishe kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri, kama nilivyoeleza hapo awali tumepokea maoni mazuri ambayo yanalenga kuboresha Muswada na kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge, basi ni ushahidi kwamba Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako kwa ujumla linaunga mkono jitihada za Serikali za kuwezesha miradi yenye maslahi mapana kama ule Mradi wa Bomba la Mafuta kwa ajili ya kuweza kutekelezwa na nchi bila vikwazo vyovyote vya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Tunashukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Sasa tunaendelea na utaratibu wetu kwa hatua zinazofuata. Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI - KATIBU WA BUNGE:** Kamati ya Bunge Zima.

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Bunge Zima

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2021)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 31

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 32
Kifungu cha 33

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2020, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya

Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2021*) Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya sheria mbalimbali (Na. 3) mwaka 2021 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Act. 2021)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusu hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2021 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2021*).

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

***Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo Kumi na Nne kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo (A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada wetu kwa sehemu ile ambayo Wabunge ndiyo tunatakiwa kuifanya na leo tumehitimisha, umeshapitishwa na Bunge Muswada huu.

Sasa kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 97 atapelekewa Mheshimiwa Rais kama sehemu ya Bunge aweze kuukubali huo Muswada, akiukataa ni mambo mengine, lakini tunaamini Mheshimiwa Rais ataukubali halafu utakuwa sheria kamili na itaanza kutekelezwa.

Kwa fursa hii niwapongeze sana upande wa Serikali kwa maana ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu sana kwa Taifa letu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo italiletea tija Taifa letu. Tunawatakia utekelezaji mzuri wa hili bomba la mafuta kutoka Uganda mpaka Chongoleani kwa maana ya Tanga, Tanzania, lakini na miradi mingine mikubwa ambayo marekebisho haya yatasaidia kuipeleka haraka. Tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa sheria hii.

Waheshimiwa Wabunge, nifanye marekebisho kidogo, wakati Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali akihitimisha hoja yake alimtaja Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje kama Mariam Shaaban, sasa nadhani lile jina la mwanzo lilikuwa kidogo limekosewa, sasa katika Taarifa Rasmi za Bunge zikae vizuri kwa sababu hakuna Mbunge anayeitwa Mariam Shaaban.

Kwa hatua hii anakuja Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nadhani atakuwa anakuja hapo ili sasa nimpishe aendelee na hatua iliyo mbele yetu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Katibu

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI,*ndc* - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 35(2), naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano wa Tatu wa Bunge sasa zimemalizika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mmeisikia hiyo taarifa, shughuli zote zimekamilika tena kwa wakati, tulipanga tarehe 30, tarehe 30 ndiyo hii, ndiyo maana huwa nawaambia katika taasisi *efficient,* Bunge ni mojawapo. *(Makofi)*

Basi kwa heshima na taarifa sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu ili, bado Katibu kwanza hebu nirudi kwako.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI - KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**SPIKA:** Hoja ya kuahirisha Bunge. Sasa nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aje atusomee hotuba muhimu sana katika siku ya leo na baadaye aweze kutoa hoja ya kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, shukrani. Leo Bunge lako Tukufu limehitimisha shughuli zote zilizokuwa zimepangwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa msingi huo, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya na uzima katika kipindi chote cha uhai wa Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa umahiri mkubwa mliouonesha katika kusimamia shughuli zote za Mkutano huu. Vilevile, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa

kushiriki kikamilifu katika Mkutano huu tangu ulipoanza tarehe 30 Machi, 2021. Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana nami kuwa kupitia Mkutano huu, tumeweza kutekeleza kikamilifu wajibu wetu wa Kikatiba kwa kupitia, kujadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/ 2022.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa upande wake itazingatia ushauri wote uliotolewa na Bunge kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa mipango na bajeti kwa manufaa ya Watanzania. Aidha, baada ya kushiriki vikao 62 vya Mkutano huu, nina hakika kila Mbunge hivi sasa atakuwa amejawa na tashwishwi ya kurejea Jimboni ili kushirikiana na wananchi tunaowawakilisha katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo pamoja na kuwajulisha kuhusu mambo mbalimbali tuliyoafikiana hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Salamu za Pole; kwa masikitiko makubwa naungana tena na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao na wengine kupata majeraha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo matukio ya ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nitoe pole kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na kwa familia ya Mheshimiwa Khatib Said Haji, aliyekuwa Mbunge wa Konde kupitia Chama cha *ACT* Wazalendo, ambaye alifariki dunia tarehe 20 Mei, 2021, katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili alikokuwa akipatiwa matibabu.

Mheshimiwa Spika, mwezi huu Juni pia, Taifa lilimpoteza mwanasiasa mkongwe, Dkt. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya ambaye alikuwa amelazwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Vilevile, nitoe pole kwa Viongozi na waumini wa Kanisa Katoliki kufuatia kifo cha Mhashamu Baba Askofu Alfred Leonard Maluma wa Jimbo Katoliki la Njombe, kilichotokea tarehe 6 Aprili, 2021. Tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahala pema. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kutuwakilisha kwenye taasisi mbalimbali ikiwemo Tume ya Utumishi wa Bunge, Bunge la Afrika, Jukwaa la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, Umoja wa Mabunge Duniani na Umoja wa Maziwa Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba wale wote waliopata fursa ya kutuwakilisha hususan huko nje wataendelea kutetea maslahi ya Tanzania, ikiwa ni pamoja na kulinda heshima ya Bunge letu na taswira ya nchi yetu. Aidha, Serikali kwa upande wake inaahidi kutoa ushirikiano wa kutosha katika kuhakikisha kuwa mnatekeleza majukumu yenu ipasavyo huko kwenye kazi yenu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu jumla ya maswali 528 ya msingi na mengine 1,468 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge pamoja na kujibiwa na Serikali. Aidha, jumla ya maswali 21 ya papo kwa papo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge pia walijadili na kupitisha maazimio mawili ya Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la kwanza ni azimio la Bunge la Kuutambua na Kuuenzi mchango wa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa utumishi wake uliotukuka; na Azimio la pili ni Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miswada ya Serikali, Bunge lako Tukufu limepokea, kujadili na kupitisha kwa hatua zote miswada ya sheria ifuatayo: -
(i) Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2021 ambao umepitishwa kwa hatua zake zote zilizotakiwa kufuatwa.

(ii) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021; na

(iii) Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria mbalimbali Na. 3 wa mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria mbalimbali Na. 4 wa mwaka 2021 na Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria ya Usalama Barabarani wa mwaka 2021 imesomwa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, naomba kueleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, mkutano huu wa Bunge ulijadili na kupitisha Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021/2022 – 2025/2026*.* Mpango huo, uliozinduliwa jana tarehe 29 Juni, 2021 una dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Vilevile, umejumuisha maeneo ya utekelezaji pamoja na miradi ambayo haikukamilika katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 umezingatia maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika mpango wa tatu ambayo ni pamoja na kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza biashara na uwekezaji, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha maisha ya watu, Serikali imedhamiria kuendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii hususan maji, elimu, afya, usafi wa mazingira na kinga ya jamii ikijumuisha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kupitia *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na mkutano huu, Bunge lako tukufu lilipokea kutoka kwenye Kamati za Kudumu za Bunge, taarifa kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 na uchambuzi wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na wajumbe wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri waliyoifanya na hivyo, kuwasilisha taarifa zilizosheheni maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa Serikali. Serikali imepokea mapendekezo hayo ya Kamati zote na itayazingatia wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022, ikumbukwe kwamba mkutano huu wa tatu wa Bunge la 12 ambao ni wa kwanza kwa Serikali ya Awamu ya Sita ulikuwa mahsusi kwa ajili ya kujadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, wahenga wamewahi kusema kuwa: "Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni". Ni ukweli usiopingika kuwa bajeti hii iliyopitishwa na Bunge lako tukufu ambayo ni ya kwanza kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imekuwa na mapokeo mazuri kwa makundi na rika mbalimbali za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako tukufu litakubaliana nami kuwa bajeti tuliyoipitisha inatoa matumaini makubwa kwa Watanzania na kuainisha mwelekeo mzuri wa uongozi wenye uthubutu, maono na utayari wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo hili lazima lipongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Watanzania tunaweza kutembea kifua mbele, kujiamini na kujivuna kuwa nchi yetu inao watu wenye uwezo na rasilimali za kutosha kujiletea maendeleo ikiwa ni pamoja na kulinda uhuru wa kujiamulia mambo yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itatekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 pamoja na maelekezo ya

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa tarehe 22 Aprili, 2021 wakati akihutubia Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itazingatia michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala kuhusu hoja ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika kuhakikisha tunawaletea maendeleo wananchi.

Aidha, niwakumbushe Waheshimiwa Mawaziri, wahakikishe wanatoa maelezo ya ufafanuzi kwa maandishi kwa zile hoja ambazo hazikujibiwa wakati wa kuhitimisha hoja za bajeti za wizara husika kutokana na ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akisisitiza umuhimu wa kila Mtanzania mwenye uwezo wa kufanya kazi, afanye kazi kwa bidii, kwa uadilifu, weledi na uaminifu. Mheshimiwa Rais ameendelea kukemea wizi, unyanyasaji, ubadhirifu na ufisadi wa mali na rasilimali za umma na nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maono na juhudi zote hizo za Mheshimiwa Rais zinajidhihirisha katika mwelekeo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022. Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022 inatoa ujumbe kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inatekeleza dhamira yake ya dhati ya kugusa maisha ya Watanzania kwa kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji, nishati, sambamba na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kijamii ikiwemo maji, umeme, afya na elimu ili kufikia azma ya Serikali ya kujenga uchumi imara, shindani na wenye kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 36.33. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 23.0 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 63. Aidha, shilingi trilioni 13.33, sawa

na asilimia 37 ya bajeti yote zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nitumie fursa hii tena kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kujadili na kupitisha bajeti hii nzuri ya Serikali. Nyote mtakubaliana nami kuwa bajeti hii kwa sehemu kubwa imewagusa wananchi wengi Pamoja na wale walio kwenye majimbo yetu kwa kuondoa yale yaliyoonekana kuwa ni vikwazo katika kufanya biashara na uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoanza utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022, nitoe wito kwa Watanzania wenzangu pamoja na washirika wa maendeleo kuiunga mkono Serikali katika kutekeleza vipaumbele ilivyojiwekea ili viweze kutoa mchango wa haraka katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na watu.

Mheshimiwa Spika, mengi yameelezwa na ufafanuzi wa kina umetolewa na Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Naibu Mawaziri wakati wakijibu maswali yao kuhusu utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2020/2021 sambamba na mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2021/2022. Hivyo basi, nitumie muda mfupi kutoa maelezo ya msisitizo kuhusu mwelekeo wa Serikali kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo ningependa kuyatilia mkazo ni pamoja na jitihada za kuvutia uwekezaji; upatikanaji wa ujuzi; sensa ya watu na makazi, vitambulisho vya wamachinga, udhibiti wa magonjwa ya mlipuko, upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, lakini pia Bima ya Afya kwa Wote na pia kuimarisha kilimo na hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kuvutia Uwekezaji, miongoni mwa mambo yaliyoibua hoja nzito kwenye mkutano huu wa tatu wa Bunge lako tukufu lilikuwa ni suala la kuvutia uwekezaji hususan vibali vya kazi kwa wageni. Hivyo basi, nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali inakamilisha

maboresho ya Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni (Sura 436) kwa kuainisha maeneo yaliyokuwa na changamoto za kiutendaji na kuathiri jitihada za kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imekwishaainisha maeneo yote yaliyohitaji marekebisho, imekutana na kupokea maoni ya wadau wa ndani na nje ikiwemo Chama cha Wafanyakazi, Chama cha Waajiri *(ATE),* Shirikisho la Wenye Viwanda *(CTI)* na Taasisi ya Sekta Binafsi pamoja na kuyajumuisha maoni hayo kwenye maboresho.

Mheshimiwa Spika, sambamba na marekebisho hayo ya sheria, tangu tarehe 23 Aprili, 2021 tumeanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa Kushughulikia Maombi ya Vibali vya Kazi kwa raia wa kigeni yaani *"Online Work Permit Application and Issuance System (OWAIS)",* katika hatua za majaribio ambapo tayari maombi zaidi ya 500 yameshughulikiwa kupitia mfumo huo. Hata hivyo, tunaendelea kupokea maoni kutoka kwa watumiaji wa mfumo kwa ajili ya maboresho. Aidha, matarajio ni kufanya uzinduzi rasmi wa mfumo huo mwezi Agosti 2021.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa manufaa yaliyopatikana kupitia matumizi ya mfumo huo ni kupungua kwa siku za kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kutoka siku 14 hadi siku tatu kwa sasa. Hali hii, pamoja na mambo mengine, imesaidia kupunguza malalamiko ya kuchelewa kupata majibu ya maombi ya vibali vya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tofauti na awali ambapo wawekezaji walilazimika kujaza fomu mbili sasa wanajaza fomu moja tu ambayo huwa na taarifa zote za kazi na ukaazi. Vilevile, vibali vya kazi vya sasa pia vipo kwenye mfumo wa kielektroniki yaani *smart card* yenye taarifa zote. Kwa hiyo, tumepunguza hatua za kuchakata maombi kutoka 33 za hapo awali hadi hatua saba tu kwa hivi sasa. Na hivi sasa, mwombaji halazimiki kuja Ofisi za Kazi kwani taarifa zote zinapatikana kwenye mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tumeondoa kigezo cha mwombaji kupata uthibitisho wa cheti kutoka NECTA, NACTE au TCU. Aidha, kwa wale waombaji wanaotekeleza miradi ya Serikali, tutaomba taasisi husika za Serikali ziwasilishe mapendekezo yao kuhusu wadau hao na tunafanya hivyo kwa lengo la kulinda ubora wa miradi hiyo na maslahi mapana ya nchi. Maboresho hayo, yanakwenda sambamba na uimarishaji wa mifumo mbalimbali ya kiutendaji ili kuwawezesha wawekezaji kufanya biashara kwa ufanisi na tija bila kuathiri matakwa ya sheria za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendesha Mkutano wa 12 wa Baraza la Taifa la Biashara *(TNDC)* tarehe 26 Juni, 2021. Mheshimiwa Rais alitumia fursa hiyo kusisitiza juu ya dira na dhamira ya Serikali ya kujenga mazingira wezeshi, imara, yanayotabirika na yenye kutoa fursa kubwa kwa sekta binafsi kuwekeza, kuzalisha na kufanya biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia hali ya upatikanaji wa ujuzi, eneo la upatikanaji ujuzi hususan katika kipindi hiki ambacho nchi yetu inapiga hatua kubwa kwenye maeneo ya viwanda nalo liliibuka na kugusa hisia za Waheshimiwa Wabunge wengi. Naomba nilifahamishe Bunge lako tukufu kuwa, Serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi nchini ambao utatoa taswira ya hali halisi ya ujuzi ikijumuisha viwango vya ujuzi wa chini, wa kati na wa juu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo rasmi ya utafiti huu yatatolewa mwezi Agosti, mwaka huu. Matokeo hayo, yatatuwezesha kufanya mlinganisho wa hali halisi ya ujuzi ilivyokuwa kwa mwaka 2014 wakati utafiti ulipofanyika na hivi sasa kwa kuzingatia afua mbalimbali zilizofanywa na Serikali pamoja na wadau kuhusu kukuza ujuzi wa nguvukazi ya nchi yetu. Kwa mfano, mwaka 2014 ujuzi wa juu ulikuwa ni asilimia 3.6 ya nguvu kazi; ujuzi wa kati asilimia 16.4 na ujuzi wa chini asilimia 80 ya nguvukazi yote.

Mheshimiwa Spika, utafiti huo pia, utatoa taarifa kuhusu soko la ajira ikiwemo hali ya ajira nchini katika sekta rasmi na isiyo rasmi; kipato kitokanacho na shughuli za kiuchumi; muda unaotumika kufanya kazi; hali ya hifadhi ya jamii; ajira mpya zinazozalishwa; ukosefu wa ajira na viwango vya ujuzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utafiti huo mkubwa unaosubiriwa kutoa matokeo husika, Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania imefanya utafiti mdogo katika sekta sita za kipaumbele nchini. Utafiti huu umeainisha baadhi ya ujuzi ambao waajiri wanauhitaji kama ifuatavyo: -

(i) Kilimo Biashara: Ujuzi kuhusu ufugaji, mbinu mbalimbali za kilimo na uendeshaji na utengenezaji wa mashine za kilimo;

(ii) Utalii na Ukarimu: Ujuzi katika mawasiliano ukijumuisha matumizi ya lugha mbalimbali, kuongoza watalii, utunzaji wa nyumba za kulala wageni na maeneo ya wageni;

(iii) Nishati: Ujuzi wa kutumia kompyuta katika masuala ya nishati, ujuzi wa masuala ya umeme na ujuzi wa masuala ya nishati jadidifu;

(iv) Sekta ya Ujenzi: Ujuzi wa uhandisi ujenzi, usanifu majengo na uendeshaji mitambo;

(v) Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA): Ujuzi wa kutengeneza na kutunza kanzi data, ujuzi wa mifumo na programu za kompyuta; na

(vi) Usafiri na usafirishaji: Ujuzi wa mawasiliano, matengenezo ya vyombo vya usafiri, TEHAMA katika mifumo ya usafiri na usafirishaji na ujuzi katika kuendesha mitambo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto za ujuzi na ajira, Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini kwa kuzingatia sekta hizo za

kipaumbele kama nilivyotangulia kuziorodhesha. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2020/2021, vijana wapatao 14,444 wanaendelea na mafunzo ya uanagenzi ili kupata ujuzi na stadi za kazi katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Kati ya vijana hao, vijana wenye ulemavu ni 349. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inaendelea na urasimishaji wa ujuzi kwa Watanzania 4,616 na kutoa mafunzo ya kilimo na mbinu za kilimo kupitia teknolojia ya kitalu-nyumba katika mikoa mitano ya Arusha, Dar es Salaam, Singida, Tabora na Pwani. Katika kutekeleza mafunzo hayo ambayo yanahusisha kikamilifu pia watu wenye ulemavu, Halmashauri 36 zitajengewa vitalu nyumba vya shamba darasa ili kuziwezesha kutoa mafunzo angalau kwa vijana 100 katika kila Halmashauri. Kadhalika, mafunzo ya utarajali (yaani *internship*) kwa wahitimu 2,591 yanaendelea katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi, Serikali pia imepanga kufanya Utafiti wa Rasilimali Watu Nchini *(National Manpower Survey)* katika mwaka 2021/2022 ili kupata taarifa za ujuzi uliopo kwa Watanzania ndani na nje ya nchi; mahitaji na sifa za ujuzi unaohitajika katika sekta mbalimbali nchini kwa sasa na baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya mwisho, utafiti huu ulifanyika mwaka 1986. Utafiti huo, pamoja na mambo mengine utatoa taarifa kuhusu idadi, sifa na mtawanyiko wa rasilimali watu; kubaini ujuzi au fani mpya zinazohitaji kuendelezwa kutokana na kukua kwa uchumi na teknolojia; nakisi na ziada ya rasilimali watu inayoongezeka kwa kila sekta; kuandaa makisio ya mahitaji ya rasilimali watu inayohitajika baadaye kwa fani; kubaini uwezo wa taasisi za mafunzo nchini kutoa ujuzi unaohitajika kwa sasa na baadaye; hali ya utumiaji wa rasilimali watu walioajiriwa na kuandaa kanzidata ya rasilimali watu kwa ajili ya kupanga na kufanya maamuzi ya kisera. Utafiti huu utahusisha waajiri, waajiriwa, taasisi za elimu na mafunzo, wahitimu wanaotafuta ajira pamoja na Watanzania waliopo nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaandaa mfumo wa kielektroniki wa taarifa za soko la ajira ili kuhakikisha taarifa hizo zinakusanywa, zinachakatwa na kutunzwa pamoja ili kuwezesha taasisi na watunga sera wote kupata taarifa husika kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, masuala ya Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2022, tarehe 22 Mei, 2021 nilizindua kitabu kuhusu Mkakati wa Usimamizi na Utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Tukio hilo, lilikuwa ni sehemu ya hatua za maandalizi kuelekea kufanyika kwa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya sensa hiyo yatasaidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wadau wengine kufuatilia na kufanya tathmini ya malengo yaliyofikiwa katika kutekeleza Mipango ya Maendeleo iliyokusudiwa kwa lengo la kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/2022) na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 pamoja na maandalizi ya Dira nyingine ya Taifa ambayo mchakato wake unaendelea ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, gharama nzima ya sensa ya watu na makazi imekadiriwa kuwa shilingi bilioni 328.2 ambazo zitatumika katika kipindi cha miaka minne (2021/2022 hadi 2024/2025) cha kukamilisha zoezi hili katika hatua za maandalizi, wakati wa kuhesabu, kuchakata taarifa za sensa na kutangaza matokeo katika ngazi ya Taifa hadi kitongoji kwa maeneo ya vijijini na mitaa kwa mijini.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri zote Tanzania Bara waendelee kuhamasisha wananchi kushiriki ipasavyo katika zoezi hili na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika kipindi hiki cha maandalizi. Aidha, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnaporudi majimboni kwenu msisahau kuhudhuria vikao vya sensa ya watu na makazi katika halmashauri zenu sambamba na kuhamasisha wananchi washiriki kutoa taarifa sahihi za

kiuchumi, kijamii na mazingira katika maeneo yao wanayoishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Vitambulisho vya Wajasiriamali Wadogo, Serikali imeendelea kuwatambua wafanyabiashara na watoa huduma wadogo nchini kwa kuwapatia vitambulisho na kuwawekea mazingira rafiki ya kufanya biashara. Tangu kuanza kwa zoezi la utoaji wa vitambulisho, jumla ya vitambulisho 2,335,711 vimegawiwa na kuwezesha kukusanya jumla ya shilingi bilioni 46.71.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa katika mwaka 2020/2021, Serikali iliamua kuboresha vitambulisho hivyo kwa kuweka picha na jina la mjasiriamali ili kuongeza udhibiti na kuwawezesha wajasiriamali kutumia vitambulisho hivyo kupata huduma za kibenki na bima ya afya. Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania itaendelea na uratibu wa kusajili wajasiriamali hao kwa kutumia mfumo, kuchapisha vitambulisho na kuvisambaza kwa Halmashauri husika kwa ajili ya kuvigawa.

Mheshimiwa Spika, suala la udhibiti wa magonjwa ya mlipuko. Serikali inachukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ikiwemo maambukizi ya *COVID-19*. Hatua hizo ni pamoja na kutoa miongozo zaidi ya 15 ya namna bora ya kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo na kusitisha safari za ndege zetu kwenda katika mataifa yaliyoathirika kwa kiasi kikubwa. Vilevile, Serikali imeimarisha ukaguzi wa wasafiri wote wanaoingia nchini kwa kuongeza wataalamu wa afya katika maeneo yote ya mipakani, kufunga vifaa vya kisasa vya kupima dalili za awali za ugonjwa huo, kuimarisha huduma za upimaji katika maeneo mbalimbali nchini na kuweka mfumo wa kielektroniki wa kupokea majibu ya vipimo ndani ya saa 24 baada ya kupima.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, tayari Serikali inafanyia kazi mapendekezo ya Kamati ya Wataalamu iliyoundwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tutaendelea

kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla hatua za utekelezaji wake. Kama ambavyo Mheshimiwa Rais alivyoelekeza kikamilifu, hali ya ugonjwa huu na tahadhari zake kupitia kikao chake na Wahariri wa Vyombo vya Habari, nami napenda nitumie fursa hii kuwakumbusha na kuwasisitiza wananchi wote wazingatie yafuatayo katika kujikinga na ugonjwa wa *COVID-19*. Kwanza, kuendeleza tabia ya kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni katika maeneo yote yenye mikusanyiko ikiwemo katika nyumba za ibada, masoko, vituo vya mabasi na daladala, lakini pia vyuo na shule na kwenye sherehe mbalimbali. Aidha, tunapokosa maji tiririka na sabuni, tutumie vitakasa mikono vinavyojulikana kwa jina la *sanitizer*.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, uvaaji wa barakoa safi na salama ambayo umetengeneza mwenyewe au umenunua kwa watengenezaji waliothibitishwa hapa nchini. Katika hili, nisisitize kwa wataalamu wa afya kutoa elimu juu ya uvaaji sahihi wa barakoa sambamba na kuhimiza matumizi ya barakoa kwenye maeneo yote yenye msongamano wa watu.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuepuka misongamano isiyo ya lazima ikiwemo kwenye vyombo vya usafiri, misiba, nyumba za ibada, mpirani na kuzingatia kukaa umbali wa mita moja au zaidi kutoka mtu mmoja hadi mwingine na kuhakikisha maeneo hayo yanakuwa na mzunguko wa hewa wa kutosha.  Nne, kujenga tabia ya kufanya mazoezi mara kwa mara, kulingana na hali ya afya ya mtu na mazingira aliyonayo kama vile kutembea kwa kasi kwa muda usiopungua dakika 30 au zaidi hadi kutoka jasho, kuruka kamba, kukimbia mwendo unaoona unakufaa au kucheza michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tano, kuzingatia lishe bora inayojumuisha matunda na mboga za majani kulingana na mazingira ya vyakula vya asili katika eneo analoishi mtu. Pia, kutumia bidhaa za tiba asili kama inavyoelimishwa na Wizara ya Afya kupitia Baraza la Tiba Asili. Sita, kwa wale wenye umri mkubwa, wenye uzito uliopitiliza na wenye magonjwa sugu

kama pumu, shinikizo la juu la damu, kisukari, magonjwa ya moyo na figo wachukue hatua madhubuti zaidi za kujikinga na maambukizi kama haya. Mwisho, ni kuwahi matibabu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya mara waonapo dalili za ugonjwa wa *COVID-19* kama mafua makali, maumivu ya koo, maumivu ya kichwa, uchovu wa mwili, kupumua kwa shida, kukosa hamu ya kula na kupoteza uwezo wa kunusa harufu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba tuzungumzie upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na vitendanishi kwenye maeneo yetu ya kutolea huduma. Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba nchini ambapo hadi kufikia Juni 2021, hali ya upatikanaji wa dawa muhimu aina 312 katika vituo vya huduma za afya imefikia asilimia 75.6. Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 191 kwa ajili ya ununuzi wa dawa ikiwa ni asilimia 95.5 ya bajeti iliyokuwa imepangwa.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa upatikanaji wa dawa endelevu katika vituo vya kutolea huduma unakwenda sambamba na uadilifu na uwajibikaji katika kusimamia mfumo wote wa mnyororo wa ugavi wa bidhaa za afya katika ngazi zote. Hivyo basi, Serikali imeendelea kufanya mabadiliko makubwa yenye lengo la kudhibiti changamoto zinazodidimiza mtaji wa dawa licha ya Serikali kuongeza mtaji huo mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali imetenga shilingi bilioni 248 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini vinavyomilikiwa na Serikali. Aidha, vituo vyote vya afya nchini vimeelekezwa kutenga asilimia 50 ya sehemu ya makusanyo wanayopata zitumike katika ununuzi wa dawa. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Mabaraza ya Madiwani mwende kusimamia kwa karibu bidhaa hizi za afya na kuifanya kuwa ajenda ya kudumu kwenye vikao vyote katika maeneo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa dawa ni moja ya nguzo za usalama wa Taifa lolote duniani. Hivyo,

nazielekeza Kamati zote za Ulinzi na Usalama kuanzia ngazi ya mkoa na wilaya kuifanya ajenda ya hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya kuwa ya kudumu katika vikao vyao. Serikali itaendelea kuwachukulia hatua watendaji ambao ni wadokozi wa dawa katika maeneo yote kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa gharama nafuu, Serikali imeendelea kurekebisha baadhi ya miongozo na taratibu ambazo zilikuwa ni kikwazo kwa wawekezaji wanapotaka kuwekeza katika eneo la viwanda vya dawa na vifaa tiba. Hali hii imeboresha mazingira ya uwekezaji, ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2021, idadi ya viwanda vinavyotengeneza dawa imeongezeka na kufikia 11 kutoka viwanda tisa kwa mwaka 2019/2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na viwanda hivyo 11 vilivyofikia hatua ya uzalishaji dawa, kuna viwanda 16 ambavyo bado vipo kwenye hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, viwanda vya ndani vya kutengeneza vifaa tiba vimeongezeka hadi kufikia viwanda 15 kutoka viwanda sita vilivyokuwepo mwaka 2019/2020. Vilevile, viwanda vidogo 181 vya vitakasa mikono, viwanda vidogo 77 vya barakoa na viwanda 23 vya majitiba vimeanzishwa na vinazalisha bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kubuni mikakati ya kuboresha upatikanaji wa bidhaa za afya, ikiwemo kuhakikisha hospitali zote za rufaa za mikoa nchini zinaanza kuzalisha bidhaa za afya hasa majitiba. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha viwanda vya kuzalisha dawa za vidonge na vimiminika katika eneo la viwanda lililopo Idofi, Wilayani Makambako, Mkoani Njombe ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa hizi kwa wakati na kwa bei nafuu unajitokeza. Kiwanda hiki kitaiwezesha Serikali kuokoa fedha za kigeni zaidi ya Dola za Marekani milioni 15.6 sawa na takriban shilingi bilioni 36 kwa mwaka ambazo zinatumika kwa sasa kununua bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, suala la Bima ya Afya kwa Wote. Mfumo wa Bima ya Afya ni mojawapo ya mifumo muhimu ya kuimarisha hifadhi ya jamii kwa kuimarisha uwekezaji katika rasilimali watu. Kwa hivi sasa, jumla ya wananchi 8,224,271 sawa na asilimia 14.7 ya Watanzania wote takriban milioni 59.4 ndiyo wanaonufaika na huduma za bima ya afya.

Mheshimiwa Spika, kati ya wananchi waliojiunga na mfumo wa bima ya afya, asilimia 8 wamesajiliwa na *NHIF*, asilimia 5.4 wanahudumiwa na Mfuko wa Afya ya Jamii Iliyoboresha *(iCHF),* asilimia 0.3 wanufaika na huduma kupita SHIB-NSSF na asilimia moja wakiwa wamejiunga na bima ya afya inayotolewa na makampuni ya bima binafsi za afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa wananchi wengi (takriban asilimia 85.3) wako nje ya mfumo wa bima ya afya na inaendelea na hatua za kukamilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga shilingi bilioni 149.7 kwa ajili ya kuwapatia bima za afya wananchi watakaokuwa wametambuliwa kutokuwa na uwezo wa kugharamia malipo ya bima.

Mheshimiwa Spika, Muswada huo unatarajiwa kuwasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu Septemba, 2021 ili kupata ridhaa ya kutungwa kwa sheria hiyo. Nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuiunga mkono Serikali pindi Muswada huo utakapowasilishwa Bungeni kwa maslahi mapana ya Watanzania kwani kutungwa kwa sheria hiyo kutamwezesha kila Mtanzania apate huduma za afya bila kipingamizi cha fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo, kwa mwaka 2020 uzalishaji wa mazao ya kilimo ndiyo shughuli iliyochangia kwa kiwango kikubwa katika pato la Taifa ikiongoza kwa kuwa na asilimia 15.4. Hata hivyo, licha ya mchango huo mkubwa wa sekta ya kilimo, bado sekta hiyo inakumbwa na changamoto kadhaa. Aidha, tumeona wakati wa mkutano huu kuwa hoja nyingi na hisia kubwa zilielekezwa kwenye sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu tarehe 22 Aprili, 2021, wakati akilihutubia Bunge lako Tukufu alitoa mwelekeo mpya katika sekta ya kilimo na kubainisha hitaji la kuongeza tija, kiwango cha mikopo, mauzo ya nje na mchango wa sekta ya kilimo kwenye pato la Taifa hadi kufikia asilimia 30 ifikapo mwaka 2025. Katika kutimiza azma hii, Mheshimiwa Rais kupitia bajeti ya 2021/ 2022 ameridhia masuala mbalimbali muhimu kwa lengo la kuimarisha masoko lakini pia, upatikanaji wa pembejeo na ugharamiaji wa shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, masuala hayo na kuongeza bajeti ya uzalishaji mbegu bora kutoka shilingi bilioni 5.4 hadi shilingi bilioni 40.6. Mbili, kuongeza bajeti ya upatikanaji wa huduma za ugani kutoka shilingi milioni 613 hadi shilingi bilioni 11.5 ambazo pamoja na masuala mengine zitawezesha ununuzi wa pikipiki 1,500 kwa ajili ya Maafisa Ugani kote nchini. Tatu kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Miradi ya Uwangiliaji (*Irrigation Development Fund*) ambayo itatumika pia kuboresha shughuli za umwagiliaji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imeweka mikakati madhubuti kushughulikia changamoto ya masoko kwa mazao ya wakulima. Tayari soko la soya limepatikana lenye mahitaji ya tani milioni 87 kwa mwaka kwa mkataba wa miaka mitatu na soko la nafaka nchini Sudan na mahindi ya njano nchini Misri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha upatikanaji wa mbegu, Serikali kwa sasa inatumia mfumo wa Muamala wa Mkopo *(Letter of Credit - LC)* kununua pembejeo katika mazao ya pamba, korosho na tumbaku. Katika mwaka 2021 pembejeo zilizosambazwa na mfumo huu ni za shilingi bilioni 130.5. Kupitia utaratibu huu Vyama vya Ushirika vitaimarishwa na kuingia makubaliano na watengenezaji pembejeo kuchukua pembejeo kwa mkopo kwa riba isiyozidi asilimia 2. Pembejeo zinazosambazwa sasa ni za zao la korosho ambazo

kufikia tarehe 15 Julai, 2021 zitakuwa zimewafikia wakulima wote kote wanakolima zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaimarisha ushirika wa wakulima kwa mazao mbalimbali ili kurahisisha kupatikana kwao, kuwahudumia na kuwafikia kwenye masoko ya pamoja. Lengo la Serikali ni kuongeza uzalishaji mazao ya kimkakati ya kibishara ili kupata ufanisi zaidi na tija kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tulikuwa na mazao matano ya kimkakati ambayo ni chai, kahawa, korosho, pamba na tumbaku. Hata hivyo, kuanzia Januari mwaka 2021, tumeongeza mazao mengine manne ambayo ni alizeti, chikichi, mkonge na zabibu inayolimwa Mkoani Dodoma pekee. Wiki ijayo tutakuwa na kikao cha wadau wa zao la zabibu kitakachohamasisha kilimo cha zabibu kote nchini. Kupitia mpango huu, tumedhamiria kupanua wigo wa kilimo cha mazao yanayotoa mafuta ya kula ikiwemo pamba, chikichi na alizeti pia karanga na ufuta ili kujitosheleza kwa mafuta ya kula hapa nchini badala ya kutegemea mafuta hayo kuyaagiza kutoka nje ambapo tunatumia zaidi ya shilingi Dola za Marekani Milioni 470. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, Serikali imeanzisha Mfuko wa Umwagiliaji kwa lengo la kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo inajiendesha wakati wote kwa kukabili mfumo wa ugharimiaji kilimo na kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 694,715 za sasa hadi hekta 1,200,000 mwaka 2025. Kwa hiyo, Wizara ya Kilimo simamieni mabadiliko ya Tume ya Umwagiliaji kutoka Tume kuwa Wakala sambamba na kuhakikisha kunakuwepo na vyanzo vya uhakika vya mapato. Wizara ya Kilimo hakikisheni Kamati ya Wataalamu kuhusu namna nzuri ya kugharamia kilimo nchini inaanza kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni Hifadhi ya Mazingira. Itakumbukwa kuwa tarehe 5 Juni, 2021 Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua Kampeni Kabambe ya Kitaifa ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira nchini. Kampeni hiyo inakwenda sambamba na Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Kitaifa kwa mwaka 2021 yenye kaulimbiu isemayo: "*Ecosystem Restoration*" ikiwa na maana "Kuongoa Mifumo ya Ikolojia". Kaulimbiu hii inazitaka nchi zote duniani kulinda na kuhifadhi mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu na ustawi wa jamii zao.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira nchini ya mwaka 2019, inaonesha kiwango cha uharibifu wa misitu na ukataji miti ni wastani wa hekta 373,000 kwa mwaka na unasababishwa na kiwango kikubwa na mahitaji ya nishati hususan ya mkaa na kuni. Hali hiyo, inatulazimu kuchukua hatua za makusudi ikiwemo kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 yenye azma ya kubuni na kuweka mikakati ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala hususan gesi na umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuthibiti Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji nchini vya mwaka 2019 mpaka 2024. Sambamba na hilo, Serikali itaendelea kutoa elimu ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira kuhusu hifadhi ya vyanzo vya maji na hivyo basi, Wizara ya Maji hakikisheni mnashirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia utekelezaji wa miradi inayolenga uhifadhi wa vyanzo vya maji. Kadhalika, endeleeni kuelimisha na kuhamasisha wananchi kote nchini kutumia nishati mbadala wa kuni na mkaa kwa lengo la kupunguza uharibifu wa misitu unaosababishwa na uzalishaji pamoja na matumizi ya kuni, mkaa kwa ajili ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo yamejadiliwa sana katika Bunge hili ni upatikanaji wa maji mpaka vijijini, upatikanaji wa umeme mpaka vijijini, ukarabati na ureshaji wa miundombinu ya barabara chini ya *TARURA* mpaka vijijini ili kujiridhisha kuwa huduma hii inawafikia Watanzania maeneo yote. Kwa kuwa eneo hili limejadiliwa

kwa kina na kutolewa ufafanuzi kwa kina na Waheshimiwa Mawaziri sitatumia muda huu kulizungumza tena bali nataka niwahakikishe Waheshimiwa Wabunge kwamba baada ya Bunge hili kukamilika leo hii Mawaziri wa sekta hizi wataendelea kusimamia kikamilifu kuhakikisha kwamba huduma hii inarejeshwa maeneo yote na inaboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022 unakwenda sambamba na mikakati ya Serikali katika kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, utendaji na uwajibikaji kwa viongozi na watendaji wote wa sekta ya umma. Hatua hizo, zinalenga kuhakikisha bajeti hii inatoa matokeo yaliyokusudiwa.

Katika kufikia azma hiyo, Serikali itaimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki ili kuongeza uwazi wa uwajibikaji na hivyo, udhibiti matumizi ya fedha za umma kwa kuepuka malipo hewa na manunuzi ya umma ya bidhaa na huduma zisizokidhi viwango vya ubora.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine litakalopewa msukumo wa kutosha ni katika kupokea, kusikiliza na kutatua kero na malalamiko ya wananchi. Kwa msingi huo, naagiza viongozi na watendaji wote Serikalini hususan wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wasikilize na washughulikie kero za wananchi kwa wakati ikiwa ni pamoja na kutenga siku maalum kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha uwepo wa thamani halisi ya matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki tena kwa wakati pale inapobainika kuwepo kwa ukiukwaji wa sheria, taratibu na kanuni za matumizi ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, wakati nikielekea kuhitimisha hotuba yangu na katika kuhimiza kuhusu masuala ya uwajibikaji na utatuzi wa kero za wananchi, napenda kusisitiza masuala machache kwa viongozi na watendaji wa Serikali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, Posho za Madaraka kwa Watendaji wa Kata na Vijiji. Katika hili, ninasisitiza kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wajipange vizuri na kuhakikisha suala la posho za madaraka kwa Watendaji wa Kata na Vijiji kupitia mpango wa Halmashauri zinasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, Mamlaka za Serikali za Mitaa hakikisheni mnatenga maeneo maalumu kwa ajili ya vijana, wafanyabiashara wadogo na watu wenye ulemavu, akina mama na kuwapatia elimu pamoja na kuwashirikisha katika kubaini maeneo yanayoendana na biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, Mamlaka za Serikali za Mitaa hakikisheni mnakamilisha maboma ya shule za msingi, sekondari, zahanati pamoja na kuanza ujenzi wa shule za sekondari za wasichana zitakazofundisha masomo ya sayansi ambazo zimeshapelekewa fedha katika kila halmashauri. Katika kutekeleza jukumu hili hakikisheni mnazingatia ujenzi fikivu ili kuwawezesha watu wenye ulemavu waweze kutumia miundombinu hiyo bila usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari shirikianeni na TAMISEMI kukamilisha mpango wa anwani za makazi na kurahisisha suala zima la utambuzi wa makazi ya wananchi ya wananchi unakamilika.

Mheshimiwa Spika, tano, nitoe wito kwa Watanzania kutumia vizuri mitandao ya kijamii kama chachu ya kuibua na kukuza fursa za kiuchumi sambamba na kuimarisha mawasiliano katika huduma mbalimbali. Aidha, Wizara na taasisi zote za Serikali hakikisheni mnaboresha huduma za wawekezaji na wafanyabiashara kwa wale ambao wamejikita katika mitandao na pia kusimamia changamoto za kisheria na kikanuni zifanyiwe kazi kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Spika, sita, licha ya changamoto za hapa na pale, mifumo ya ununuzi wa mazao hususan kupitia Stakabadhi Ghalani umekuwa na mafanikio makubwa kwa

baadhi ya maeneo. Tumeona manufaa hayo kwa zao la ufuta ambalo kwa sasa liko sokoni linauzwa kwa siyo chini ya shilingi 2,350/= na korosho hususan kwa Mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Kwa hiyo, niwaelekeze Wizara ya Kilimo iendelee kusimamia mifumo hiyo kwa maeneo hayo ambako imeonekana kufanya vizuri na kwa mikoa ile bado haijapata elimu ya kutosha, itolewe elimu ya mfumo huu ili uweze kuwasaidia katika kupata mapato yao halisi.

Mheshimiwa Spika, saba, upatikanaji wa pembejeo mapema kabla ya msimu mpya wa kilimo kuanza; Mfumo wa Ununuzi wa Pembejeo kwa pamoja umeonesha mafanikio makubwa kwa upatikaaji wa pembejeo kwa wakati kwa kumpunguzia mkulima mzigo hasa riba. Wizara ya Kilimo, simamieni kikamilifu mfumo huu na hakikisheni kuwa mnamaliza changamoto ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa msimu ujao wa kilimo. Matamanio yetu ni kuona kwamba wakulima wanapata pembejeo mwezi mmoja au miwili kabla ya kilimo cha zao lenyewe kuanza kulimwa, wakulima wawe wameshapata pembejeo zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nane, Kilimo cha Mkataba. Tumeamua kwenda na utaratibu huu kwa baadhi ya mazao ikiwemo alizeti, ngano, shayiri na soya ili kumpatia tija mkulima. Kwa upande wa soya, soko la uhakika la China lipo. Kwa msingi huo, nasisitiza kwamba Wizara ya Kilimo hakikisheni mikataba inayoingiwa na wakulima inakuwa wazi ikionesha bei na kiwango cha kuuza. Vilevile, simamieni mikataba baina ya wakulima na wanunuzi wakubwa bila kuwadhulumu wakulima wetu ili mkulima huyu mdogo mdogo anayelima mazao haya aweze kupata manufaa zaidi.

Mheshimiwa Spika, tisa, Wizara ya Kilimo simamieni upatikanaji wa mbegu bora katika kilimo cha ngano na zabibu ili watu wengi zaidi waweze kushiriki kwenye zao hili. Aidha, utoaji wa vibali kwa wanunuzi wa ngano na mchuzi wa zabibu ufanywe kwa kuzingatia wale ambao wanathibitisha kununua malighafi hizo ndani kwanza. Hakikisheni mnasimamia vizuri makubaliano kati ya wakulima

na wanunuzi wakubwa ili tusinunue bidhaa hizo kutoka nje ili bidhaa ya ndani ipate soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, kumi, Masoko ya Mazao, nafahamu kuwa tayari tupo kwenye msimu wa pamba. Ninasisitiza kuwa wakulima wa pamba wasikatwe gharama za pembejeo kwa kuwa tayari zipo kwenye mjengeko wa bei. Kwa hiyo, nitoe wito kwa wakulima kupeleka sasa pamba yao kwenye minada ili waweze kunufaika na bei ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa tumbaku, Wizara ya Kilimo shirikianeni na Wizara ya Fedha kukamilisha mazungumzo na wanunuzi wa zao hili hususan kipindi hiki ambacho bei ya tumbaku inaonekana kuimarika kwenye soko la dunia. Pia tafuteni masoko ya tumbaku ya moshi ili ipate soko la uhakika ili wakulima wanaolima aina hii ya tumbaku ya moshi waweze kupata soko la uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fursa mpya ya kilimo cha soya, Wizara ya Kilimo hakikisheni mnakuwa na mpango mzuri wa kuendeleza kilimo hicho kwa kuhakikisha kuwa wakulima wanapata mbegu tukianza na mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ambako huko awali zao hili lilikuwa linalimwa kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia kwa kuja na wazo la kuwa na maghala kwenye nchi zenye fursa ya masoko. Wafuateni wateja, msisubiri waje kwenu kwani biashara ni ushindani, nanyi muingie kwenye ushindani na Wizara ya Kilimo simamieni hayo. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, pia kilimo cha Umwagiliaji, Serikali imeanzisha Mfuko wa Umwagiliaji kwa lengo la kuhakikisha kuwa Sekta ya Kilimo inajiendesha kwa kubadilisha Mfumo wa Ughalimiaji kilimo na kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 69,4715 na hadi sasa milioni 1.2 ifikapo mwaka 2025. Kwa hiyo Wizara ya Kilimo tusimamie maelekezo yote ambayo nimeyatoa kuhusu Tume na Wakala wake ili iweze kuanza kazi mara moja na tupate matokeo mazuri. Nisisitize pia

kwamba Wizara ya Kilimo hakikisheni Kamati za Wataalamu zinapata fursa ya kusimamia kilimo kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuzipongeza Wizara za TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, kwa kuiratibu vizuri sana michezo ya mashule ya UMITASHUMTA na UMISETA ambayo inaendelea sasa kule Mkoani Mtwara. Tunashuhudia hamasa za wanafunzi kushiriki kwa ushindani wa hali ya juu, pia napongeza wakazi wa Mkoa wa Mtwara na wenyeji wa Mtwara Mjini kwa kujitokeza kwa wingi kushangilia vijana wetu. Ni matarajio yetu kuwa uratibu huo utaendelea pia kwa miaka ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Wizara husika na Michezo kutoa ratiba ya kila mwaka mapema ili kuonyesha kutoka maandalizi hadi mashindano ili kuwezesha Shule, Wilaya na Mikoa kuandaa timu zao kwa viwango zaidi ili mwakani tuweze kupata ushindani mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, wote tunatambua kwamba tarehe 3 Julai, 2021 ni siku inayongojwa kwa hamu na wanamichezo nchini, hasa wapenzi wa soka, siku ambayo vigogo wawili wa soka nchini watapambana katika Uwanja wa Taifa Jijini Dar es Salaam. Katika hili tunazitakia timu zote ushindi mnono kwenye mapambano hayo na tunaamini kila mmoja ataibuka akiwa mbabe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kusisitiza kuwa suala la kuwahudumia Watanzania na kuwaletea maendeleo halimo katika mikono ya Serikali pekee. Kwa lugha nyingine ni kwamba, kila mmoja wetu anao wajibu wa kushiriki kikamilifu kwenye utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi ili kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru tena wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge na Watumishi wa Bunge kwa huduma nzuri

mliotupatia wakati wote tukiwa hapa Bungeni. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wenzangu kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kujibu hoja, kufafanua hoja, kupitia maswali yote mliyoulizwa. Nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wenzangu pia na ninawatakia safari njema mnaporejea majimboni kwa kwenda kushirikiana na wananchi katika kutekeleza Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Watendaji wa Serikali walioshiriki katika kuwezesha Wizara na kupata majibu ya uhakika kutoka kwenye Wizara zao kwa shughuli zilizopangwa na Bunge hili kwa weledi mkubwa, uadilifu na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, siwezi pia kuwasahau wanahabari kwa uchambuzi wa habari zetu za hapa na kuwapelekea wananchi na kuwahabarisha Watanzania juu ya nini kinaendelea. Nawashukuru pia vyombo vya Ulinzi na Usalama, ambavyo pia vimewezesha Waheshimiwa Wabunge kukaa hapa na kuendesha shughuli zote kwa amani na utulivu; bila kuwasahau watu muhimu sana madereva na wahudumu waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana nami kwamba toka tumeanza Bunge hili na kurudi, tulipata tatizo moja tu la Mheshimiwa Ghati ambaye alipata ajali njiani, lakini vinginevyo Mwenyezi Mungu ameweza kuwalinda madereva wetu, ameweza kutulinda sisi sote na tunamaliza Bunge hili tukiwa salama. Kwa hiyo, madereva na wahudumu wote tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe

hadi tarehe 31 mwezi wa nane, 2021 siku ya Jumanne, saa 3.00 asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi/Vigelegele)*

Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Malalamiko hayo unayoyasikia, baada ya kutaja tarehe ya kukutana tena ndiyo zogo limeanza hapa. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ametoa hotuba ya kukamilika kwa shughuli za Mkutano wa Tatu wa Bunge kufuatana na Kanuni 35(3). Sasa kabla sijaendelea na matangazo tuiamulie hoja hiyo kwanza. Wanaoafiki kwamba Bunge hili liahirishwe hadi tarehe aliyoitaja Mheshimiwa Waziri Mkuu.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wasiotaka kuondoka hapa ni wale wanaoogopa kwenda kukutana na Wajumbe.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante kwa hotuba hiyo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na viongozi wote Serikalini katika ngazi zote.

Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Wenyeviti wa Kamati, Wabunge wote kupitia Kamati zetu mbalimbali, ni kwa pamoja tumeweza kufika mahali ambapo sasa tumehitimisha zoezi letu la kuipatia Serikali bajeti ambayo

tunatarajia, basi kesho tarehe 01 mwezi wa Saba inaweza ikaanza kutekelezwa. Tunasema ahsanteni sana wote.

Nami kipekee niwashukuru sana wasaidizi wangu, Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia, ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Azan Zungu nakushukuru sana, ahsante sana; Mheshimiwa Najma Giga, ahsante sana, Mheshimiwa David Kihenzile, nawashukuruni sana. Kwa pamoja tumesaidiana sana kuweka mambo sawa sawa kwenye Meza yetu hii kubwa. *(Makofi)*

Pia Katibu wa Bunge na timu yako yote na wafanyakazi wa Bunge wote, nawashukuruni sana, sana kwa utendaji uliotukuka. Watumishi hawa wa Bunge ni katika kada ya watumishi wanaochapa kazi sana. Wakati kama huu wa Bajeti kwa miezi yote hii mitatu, wanafika hapa asubuhi saa moja kamili au kabla ya hapo na wanaondoka baada ya saa mbili usiku kila siku. Tunawapongeza sana na ni wavumilivu sana. Natumaini wamewahudumia vizuri. *(Makofi)*

Sitaki kurudia maneno ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu bajeti hii ilivyo nzuri, tuwatakie tu kila la heri wenzetu ili itekelezwe inavyopasa.

Sasa Waheshimiwa Wabunge kama mnavyojua, leo ni siku ya Mabunge duniani. Leo ni siku yetu; katika siku yetu hiyo, niwaambie tu kidogo dondoo mbili, tatu; ni kwamba duniani kuna Mabunge katika nchi 193. Ukitaka hizo takwimu unaenda kwenye *website* ya *IPU - Internal Pariament Union.* Katika nchi hizo 193, nchi 79 tukiwemo sisi tuna *chamber* moja moja ya Bunge; na nchi 114 zina *chamber* mbili za Mabunge; Bunge kama hili la kwetu, halafu linakuwepo Bunge lingine dogo zaidi, wengine wanaita *Senate*, wengine wanaita jina lingine. Wale wanaosema katiba, katiba; nafikiri moja ya mijadala ya namna hiyo huko mbele ya safari ni kuangalia kama moja linatosha au kuna haja ya kuwa na lingine dogo tena huko juu kama nchi nyingine zilivyo.

Hapa Afrika Mashariki ni Rwanda wana *chamber* na Kenya, inawezekana na *South Sudan,* Burundi pia wana

chemba mbili. Tumebakia Uganda na Tanzania. Vile vile duniani hapa Rwanda ndiyo inaongoza kwa kuwa na Wabaunge wengi wanawake ndani ya Bunge. Asilimia 61 ya Wabunge ndani ya Bunge la Rwanda ni wanawake. Eti hiyo asilimia 61, ndiyo *fifty fifty.* Waheshimiwa Wanaume mwone hiyo, 61% ndiyo *fifty fifty* hiyo, lakini wanaongoza, hatuwalaumu wala nini. Ni mfano wa kuigwa. Bunge la Norway ndiyo linaongoza kwa kuwa na Wabunge vijana wengi wa chini ya miaka 30; yaani miaka 30 kushuka chini. Asilimia kama 14 ya Wabunge wao wana miaka 30 kushuka chini.

Bunge la kwetu tunashindwa kupiga hesabu vizuri, kwa sababu kuna Wabunge kadhaa ambao *consistently* hawatuambii habari ya umri wao, tunashindwa... *(Kicheko/ Makofi)*

Kwa wale ambao wametuambia, Bunge letu liko *medium,* liko kwenye miaka kati ya 40 – 45. Kwa hiyo, Bunge letu siyo kweli sana kwamba ni la vijana, wala siyo kwamba ni la wazee, liko hapo katikati sijui tunaita nini hapo. Umri ambao ni mzuri sana, wenye uzoefu wenye uwezo wa kutoa maamuzi mazuri, umri wa uchapakazi ndiyo Bunge letu lilipo hapo. *(Makofi)*

Wabunge duniani; maana Wabunge wanawakilisha watu karibu bilioni nane duniani. Kuna Wabunge kama 46,000 au na zaidi kidogo dunia nzima. Kwa hiyo, ni kikundi kidogo sana cha watu kinachofanya maamuzi makubwa sana ya watu wengi sana hapa duniani. *(Makofi)*

Sasa kwa ajili ya siku hiyo ya Mabunge duniani, tumepata salamu kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu salamu hizi ni zenu Waheshimiwa Wabunge basi nivumilieni nizisome ili ziwafikieni.

Ikiwa leo tarehe 30 Juni, 2021 ni Maadhimisho ya Siku ya Mabunge Duniani, Mheshimiwa Rais anasema: "napenda kutumia fursa hii kutuma salamu za pongezi kwako Mheshimiwa Spika na kupitia kwako kwa Bunge letu Tukufu

la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuisimamia Serikali. Aidha, Mheshimiwa Rais anapenda kutupongeza Wabunge wote kwa kujitoa kwetu katika kuwawakilisha wananchi kwa kuleta hoja na mapendekezo yanayolenga kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Pongezi nyingi zaidi ziwaendee wale waliochaguliwa kuliwakilisha Bunge la Tanzania katika Mabunge ya Kimataifa. Mheshimiwa Rais anasema, chini ya uongozi wako Mheshimiwa Spika, Bunge la Tanzania limekuwa ni kitovu cha demokrasia Barani Afrika, jambo ambalo limesababisha kuchaguliwa kuwa Makao Makuu ya Sekretarieti ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola Barani Afrika kuwa hapa. *(Makofi)*

Hali kadhalika, Mheshimiwa Rais anasema, napenda kulipongeza Bunge kwa kupiga hatua kubwa kuongeza uwakilishi wa makundi ya wanawake na vijana. Huu ni mwelekeo mzuri katika kuimarisha uwiano wa uwakilishi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Mheshimiwa Rais anamalizia, kwa kusema nalitakia kila heri Bunge letu katika kutimiza majukumu yake, Kazi iendelee. Kwa mkono wake mwenyewe amesaini hapa, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa niwape taarifa katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge, Bunge limepitisha Miswada miwili ya Sheria ya Serikali; mmoja ukiitwa Muswada wa Fedha za Matumizi, 2021 *(The Apropriation Bill,* 2021) na mwingine ni Muswada wa Sheria ya Fedha, 2021 *(The Finance Bill, 2021).* Kwa taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Miswada hiyo imeshapata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo sasa ni Sheria kamili za Nchi zinazoitwa; moja, Sheria ya Fedha za Matumizi, Na. 2 ya mwaka 2021 *(The Appropriation Act, No. 2 of 2021);* na mbili, Sheria ya Fedha, Na. 3 ya Mwaka 2021 *(The Finance Act, No. 3 of 2021). (Makofi)*

Kwa hiyo maana yake sasa ni kwamba, kila kitu kimekamilika, Serikali inaweza ikaanza na bajeti mpya kesho, kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uharaka na kutoa umuhimu wa kipekee kwa jambo hili la bajeti ambapo sasa kwa upande wake kwa kweli ameshatekeleza wajibu wake. Amekubaliana nasi kwamba bajeti tuliyoipitisha kwa kweli naye ameikubali, sasa twende kwa wananchi kwa nguvu moja. *(Makofi)*

Wataalam wetu wa Bunge wameandika kitabu cha Historia ya Bunge letu toka tulivyoanza enzi hizo za *LEGCO* mpaka sasa tulipofika. Kitabu hicho kitagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge, naomba kila mmoja wenu awe na nakala ili kuweza kujua tumetoka wapi na tupo wapi. *(Makofi)*

Pia kuna Gazeti moja linaitwa *Panorama* ambalo nilikwisharuhusu Katibu uwagawie Waheshimiwa Wabunge; sijaona wakigawiwa. Au mmewekewa kwenye *pigeon holes?* Basi mnapotoka pale wamejiandaa, vijana wetu watawapatia. Linahaririwa na aliyekuwa Katibu wetu wa Bunge, Dkt. Kashillilla, mliangalie.

Tunamshukuru sana kwa niaba yenu pia Dkt. Kashillila kwa juhudi kubwa ambayo anaifanya. Kama kutakuwa na *comments* zozote tutazipokea ili matoleo yanayofuata basi yaendelee kuwa bora na bora zaidi.

Baadhi ya wageni walipo Bungeni asubuhi hii ni Katibu Mkuu wa *African Continental Free Trade Area (ACFTA),* Mheshimiwa Wamkele Mene. *Can you stand up please; thank you very much. (Makofi)*

Huyu ni Katibu Mkuu *(General Secretary)* wa *African Continental Free Trade Area* na jana nilimwona kule Zanzibar kupitia vyombo vya habari na sasa yuko Dodoma, naamini kuonana na uongozi mzima wa Serikali, na sasa amekuja Bungeni hapa ambapo ataonana na baadhi yetu viongozi,

hasa Mwenyekiti wa *PIC,* Mwenyekiti wa Viwanda na Biashara na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Tunaye *Madam* Emilly Njeri-Ndoria, *Director of Trade in Services Investment and Intellectual Property Rights and DT;* karibu sana. *(Makofi)*

Yuko Dkt. Halima Moore Abdi, *Senior Trade Expert,* ni huyo hapo, ahsante. *(Makofi)*

Vilevile yupo *Madam* Grace Khoza, *Principal Communications Advisor;* ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Paul Okech, *Special Assistant; you're welcome* Okech. *(Makofi)*

*Madam* Zimkhita Tshosane, *Executive Assistant* na *Madam* Naa Odaaley Mills, *Protocol Assistant.* Ahsante sana. *(Makofi)*

Huu ni msafara unaofuatana na mgeni huyu maalum kabisa anayeshughulika na masuala haya ya *Free Trade Area* katika Bara letu la Afrika. *(Makofi)*

Wako wageni wawili wa Mheshimiwa Minza Simon Mjika; Ndugu Agnes na Ndugu Debora Mahulu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Minza amehakikisha wanatambulishwa hawa maana ni wifi zake. Kwa hiyo mawifi, Mheshimiwa yupo anaendelea vizuri hapa.

Katibu wa Bunge anatutangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba tarehe 18, Julai, 2021, kutakuwa na mbio za riadha zinazoitwa *Zanzibar International Marathon,* wakishirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Waheshimiwa Wabunge ambao mngependa kufanya hivyo siku hiyo basi mjiandikishe. Mbio hizi zitakuwa za kilometa 21, kilometa 10, kilometa tano na mita 700 kwa wazee na watoto.

Tunaombwa kuweza kushiriki mbio hizi, zimeandaliwa vizuri. Ni mbio muhimu.

Mheshimiwa Shally Raymond, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake anawaomba *TWPG* wote mkutane Msekwa baada ya kumaliza shughuli zetu hapa.

Wajumbe wa Tume ya Huduma za Bunge, kikao cha kwanza ni kesho saa nne kamili katika Ukumbi wa Spika. Tutawaomba wote muweze kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo na shukrani hizo, sasa Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE:**

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

**SPIKA:** Watumishi wetu wa Bunge sasa tunawaomba mtuimbie wimbo wetu wa Taifa.

*(Hapa Kwaya ya Bunge iliimba Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana kwaya. Tuwapigie makofi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tukiwa tumesimama, tulianza na Mungu na tumemaliza na Mungu. Nawatakieni wote mwende salama na Mungu awatangulie. Kwa siku ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameitaja, basi itabidi turudi tena hapa Bungeni, tuendelee na shughuli zetu.

Baada ya kusema hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge Rasmi. Ahsanteni sana.

*(Saa 7.50 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 31 Agosti, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*